

## BUNGE LA TANZANIA

### MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Hamsini – Tarehe 21 Juni, 2019

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Tulla Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:**

#### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, sasa aulize swali lake.

Na. 421

#### Udhibiti wa Watumishi Hewa

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Serikali ina Mkakati gani wa kuhakikisha kuwa watumishi hewa hawapo katika *payroll* ya Serikali:-

Je, Serikali inadhibiti vipi mishahara ya watumishi wasiostahili kulipwa kama wastaifu, waliofariki, walioacha kazi na waliofukuzwa kazi katika Halmashauri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHESHIMIWA JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani mwishoni mwa mwaka 2015 kumekuwepo na mkakati madhubuti wa kudhibiti uwepo wa watumishi hewa katika Mfumo wa Malipo ya Mishahara kwa Watumishi wa Umma nchini. Utekelezaji wa mkakati huo ulifanyika kuanzia mwaka 2016 kwa kuendesha zoezi la uhakiki wa vyeti vya watumishi wote walipo kwenye taasisi zote za Serikali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika uhakiki huo, watumishi wote ambao hawakuwa na sifa ya kulipwa mishahara waliondolewa mara moja katika Orodha ya Malipo ya Mishahara (*Payroll*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kudhibiti malipo ya mishahara kwa watumishi wasiostahili kulipwa kama vile wastaafuli, waliofariki na waliofukuzwa kazi, Serikali imekuwa ikisitisha mara moja malipo ya mishahara ya watumishi wa aina hiyo kupitia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi (*Human Capital Management Information System*) na Mfumo wa Malipo ya Mishahara (*Government Salary Payment Platform*) pindi tu wanapokosa sifa ya kuendelea na Utumishi wa Umma. Mifumo hii inatumika katika Taasisi zote za Serikali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna udhibiti ulivyo hivi sasa na ufuatiliaji unavyofanyika, hakuna mtumishi anayeweza kulipwa mshahara bila kustahili. Aidha, naomba kutoa wito kwa Maafisa Masuuli katika Taasisi zote za Umma kuendelea kusimamia kikamilifu udhibiti wa malipo ya mishahara kupitia mifumo iliyopo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah Jeramiah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali, bado malipo ya mishahara na makato kwa watu ambao sio Watumishi wa Umma bado yanaendelea kulipwa kulingana na hoja za Mkaguzi CAG. Kwa mfano 2017/2018 shilingi milioni 207.3 zilllipwa. Je, ni kwa nini Wizara ya Fedha inachelewa kukamata yaani ku-*hold* makato yaliyolipwa kwa Taasisi mbalimbali na kusimamisha makato ya mishahara kwa kiwango sawa na watumishi wasiostahili kulipwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; je, Serikali inachukua baada ya muda gani kuweza kuhuisha taarifa za watumishi ili waweze kushughulikiwa haraka kwa kuondolewa katika Mfumo wa Malipo ya Mishahara? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utumishi na Utawala Bora.

**NAIBU WAZIRI WA UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba nami njibui maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Leah Komanya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama Serikali tulifanya *HR Audit* kwa Watumishi wote wa Umma wakiwepo na hawa wa TAMISEMI zaidi ya 197,000 mwaka ule wa 2016, lakini watumishi wote wale wanaoacha kazi, waliofukuzwa kazi, waliofariki, hawasalii kabisa kwenye *Payroll* ya Serikali. Naomba niliambie Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kwamba kama Serikali sasa hivi tumeboresha Mfumo wa Utumishi na Mishahara kiasi cha kwamba hatutatumia tena ile *Lawson Version 9* ambayo tulikuwa tunatumia, tuna Mfumo wetu wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, taarifa zozote zinazotoka kwa waajiri wote, kama ziko sahihi zinatolewa

siku hiyo hiyo ikiwepo pamoja na malipo ya madai yote. Kwa hiyo, nawataka waajiri wote nchini kuhakikisha kwamba wanatuletea taarifa ambazo ni sahihi na kwa wakati na kutokana na mfumo wetu huu mpya ambao tunauanza mwezi ujao, basi taarifa za watumishi wote zitatolewa siku hiyo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Abdulrahaman Ghasia Mbunge wa Mtwara Vijijini, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Abdallah Chikota.

Na. 422

**Upungufu wa Madaktari Bingwa – Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ligula**

**MHE. HAWA A. GHASIA** aliuliza:-

Hospitali ya Mkoa wa Ligula inakabiliwa na upungufu wa Madaktari Bingwa:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa Hospitali ya Mkoa wa Mtwara Ligula inapata Madaktari Bingwa wa kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali ya Mheshimiwa Hawa Abdulrahmani Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara (Ligula) inahitaji kuwa na Madaktari Bingwa wa fani mbalimbali ili kuwezesha kutoa huduma za kibingwa. Aidha, Wizara inatambua kuwa, Hospitali hii kwa sasa ina

Madaktari Bingwa mmoja tu wa fani ya Uduktari Bingwa wa magonjwa ya uzazi na wakawake (*OBGY*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia uamuzi wa Serikali kuzihamishia Hospitali za Rufaa za Mikoa kuwa chini ya usimamizi wa moja kwa moja wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara imefanya tathmini ya kina kujua hali halisi ya mahitaji ya Madaktari Bingwa na fani zao katika Hospitali zote za Mikoa, Kanda, Maalum na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tathmini hii, itawezesha utekelezaji wa uamuzi wa kuwapanga upya Madaktari Bingwa kwa uwiano kulingana na mahitaji ya kila Hospitali ya Mko, kanda maalum na Taifa. Lengo ni kuwa, kila Hospitali ya Mkowa iwe na Madaktari Bingwa wa fani nane za kipaumbele ambazo ni Daktari Bingwa wa Uzazi na Wanawake, Daktari Bingwa wa Watoto, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani, Daktari Bingwa wa Upasuaji, Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Mifupa, Daktari Bingwa wa Huduma za Dharura na Magonjwa ya Ajali, Daktari Bingwa wa Huduma za Usingizi na Daktari Bingwa wa Huduma za Radiolojia katika Hospitali za Mikoa ikiwemo Hospitali ya Ligula.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara imewapeleka Madaktari Bingwa wa fani za Upasuaji wa kawaida na Upasuaji wa Mifupa 125 katika Chuo cha *MUHAS* amba wanatarajia kumaliza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021. Madaktari hawa watapangwa katika Hospitali ya Rufaa za Mikoa ikiwemo Ligula. Wizara itaendelea kutenga bajeti ya kuwasomesha Madaktari Bingwa wa fani mbalimbali ili kufikia azma ya Serikali ya kuhakikisha Hospitali zote za Rufaa zinakuwa na Madaktari Bingwa wa kutosha. Kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019 Serikali inagharimia masomo ya madaktari bingwa 127 katika Chuo cha *MUHAS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kipindi hiki cha mpito, Serikali imekuwa ikiendesha kambi za udaktari bingwa

ikiwa ni pamoja na upasuaji kwa lengo la kufikisha huduma za madaktari bingwa kwenye mikoa isiyokuwa na huduma hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Wizara, napongeza viongozi wa Wizara hii; Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, wamekuwa wakifanya safari nyingi kuja Mtwara ili kukabiliana na changamoto za hospitali hii. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa imeonekana hali ni tete kwa sababu hospitali yetu ya Rufaa ina Daktari Bingwa mmoja tu, sasa ningependa kujua kwamba: Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi kuhakikisha kwamba tunapata angalau Madaktari Bingwa watatu kwa kipindi hiki ambacho tunasubiri hao ambao wameenda vyuoni wahitimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri kama alivyojionea alivyotembelea hivi karibuni Ligula kwamba majengo mengi yamechakaa yanahitaji ukarabati: Je, Wizara ina mpango gani kuyakarabati majengo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Abdallah Chikota, Mbunge ambaye naye anatoka Mtwara kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya, lakini katika ufuatiliaji wa karibu katika masuala mbalimbali ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusudio la Serikali ni kuhakikisha kwamba tunatoa huduma bora za afya katika mikoa yote nchini na ndiyo maana Mheshimiwa Rais alifanya uamuzi wa kuhamisha Hospitali za Rufaa za Mikoa kuja chini ya Wizara ya ili ziweze kupata usimamizi wa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kujibu swali lake la kwanza, ni mikakati gani ambayo tunayo ya muda mfupi kuhakikisha kwamba tunapata hizi huduma za kibingwa, nimeeleza katika jibu langu la msingi kwamba katika hiki kipindi cha mpito, Wizara kwa kushirikiana na Mfumo wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*), wamekuwa wanaendesha kambi mbalimbali za huduma za udaktari bingwa katika baadhi ya mikoa na tumekuwa na mizunguko hiyo ili kuhakikisha kwamba yale maeneo ambayo hayana huduma hizo kwa sasa zinaweza kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, wale madaktari ambao wanamaliza sasa hivi, tumeweka utaratibu wa kuwafanya kitu kinaitwa *borning* kwamba daktari ambaye amesoma kwa fedha za Serikali, atapangwa pale ambapo Serikali itamhitaji kwa kuwa ametumia fedha za Serikali na kwa chini ya utaratibu huo, madaktari ambao tunawapanga sasa hivi kwa sababu tumefanya tathmini ya Ikama, basi tutawapeleka katika maeneo ambayo wanahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tumefanya tathmini ya kina ya miundombinu ya uchakavu wa majengo katika hospitali zote za Rufaa za Mikoa na sasa hivi tumeanza kujielekeza kama Wizara katupitishia fedha ambazo ziko kwenye bajeti kufanya ukarabati mkubwa, nami nilikuwa pale Ligula tunafanya ukarabati wa jengo la bima, tumefanya ukarabati wa *corridor*, tunataka tukamilishe ile wodi ya *grade one* na vile vile tunataka sasa kuhamisha ile majengo ya *theatre* ili wananchi wa Mkoa wa Mtwara waweze kupata huduma nzuri na yenyewe ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa ambalo tunataka tulifanye sasa Mtwara ili kufuta kilio cha wananchi

wa Mtwara cha muda mrefu, kusudio la Serikali ni kuanza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo tuna maswali mengi kuliko muda tulionao, nadhani mnaweza kuona kwenye *Order Paper*. Kwa hiyo, muda wetu wa saa moja hautatutosha.

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 423

### **Mazingira Magumu ya Biashara**

**MHE. RUKIA K. AHMED** aliuliza:-

Mazingira ya kufanya biashara nchini ni magumu na hii ni kwa wafanyabiashara wa ndani na wa nje:-

Je, ni lini Serikali itaondoa urasimu ili wananchi waweze kunufaika?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
(k.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikibuni na kutekeleza mikakati na mipango mbalimbali kwa kuhakikisha uwepo wa mazingira bora ya ufanyaji biashara nchini. Kwa mwaka 2017, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa Sekta binafsi ilifanya uchambuzi wa kina wa mazingira ya biashara nchini kwa sekta zote na kubaini changamoto mbalimbali zikiwemo mwingiliano wa sheria. Kufuatia changamoto hizo, Serikali iliandaa Mpango wa Kuboresha

Mfumo wa Udhibiti wa Mazingira ya Biashara Nchini (*Blue Print for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment for Tanzania*) ambao umeridhiwa na Baraza la Mawaziri kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huo utasaidia kuondoa mwingiliano wa sheria na kupunguza urasimu kwa wafanyabiashara wakati wa kupata huduma katika Taasisi mbalimbali za Serikali. Mpango wa Utekelezaji wa *Blue Print* umekamilika. Sambamba na hilo, Serikali tayari imetekeleza baadhi ya mapendekezo ambayo ni ya kiutawala na yasiyohitaji mabadiliko ya sheria. Mfano, katika Sekta ya Kilimo na Mifugo, jumla ya tozo 114 na tano za *OSHA* zimeondolewa na mapendekezo ya kuondolewa tozo nyingine kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2019 yameshawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mafanikio ya jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara ni kwa Tanzania kuendelea kuongoza kwa uwezo wa kuvutia mitaji kutoka nje (*Foreign Direct Investment*) katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki tangu mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya Uwekezaji ya Dunia (*World Investment Report*) inayotolewa na Shirika la Biashara na Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNCTAD*) ya mwaka 2018, Tanzania imeongoza katika nchi za Afrika ya Mashariki kwa kuvutia mitaji ya jumla ya Dola za Marekani 1,180 ikifuatiwa na nchi ya Uganda kwa Dola za Marekani 700. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha maboresho yanayofanyika yanadumishwa na kuendelea kubuni mikakati ya kuboresha zaidi mazingira ya kufanya biashara nchini. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, swali la nyongeza.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa

kuwa tatizo kubwa tulilonalo katika nchi yetu kwenye mazingira ya biashara ni mfumo wa kodi kuwa hauko wazi: Je, ni lini sasa Serikali itaandaa mfumo wa kodi ambaao utakuwa wazi katika mazingira haya ya ufanyaji biashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa sababu nchi yetu katika uwezeshaji ufanyaji wa biashara imeambiwa ni nchi ya 144, Rwanda ambayo ni nchi ndogo ni ya 29, Kenya ni nchi ya 40: Je, Serikali haioni kwamba tutapoteza wawekezaji katika halali hii ili tuweze kujirekebisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (k.n.y WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mazingira yetu ya kodi kuwa wazi, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imekuwa ikititia mazingira ya kodi kila wakati na ndiyo maana hata kwenye kila Bunge, mara nyingi tumekuwa tukipata mapitio ya kodi mbalimbali ili kuendelea kuboresha mazingira yetu ya kodi yaweze kuwa ya kishindani na yaweze kurahisisha biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na changamoto ambazo bado zipo, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali la pili la namna gani tunaweza tukaboresha mazingira yetu ya uwekezaji, kama nilivyosema kwenye jibu letu la msingi, Serikali imeshachukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kukaa na wafanyabiashara kujadiliana nao mazingira au changamoto wanazozipata. Ndiyo maana tumekuja na *Blue Print* kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kibiashara. Tutaendelea kufanya *reforms*; na ndiyo maana hata juzi Mheshimiwa Rais aliwaita wafanyabiashara akakaa nao mukutano wa masaa mengi akisikiliza kero zao. Lengo ni

kupata changamoto na mawazo yao ili kuboresha mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hili litaendelea na baada ya muda siyo mrefu, mazingira yetu yataboreka, yatakuwa mazuri na itaendelea kuvutia wawekezaji kutoka nje.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nami naomba kuongeza majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda katika swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Rukia Kassim kuhusiana na wepesi wa kufanya biashara. Kwanza kabisa nimhakikishie kwamba tutakapoenda katika mwaka ujao kwa nafasi ya Tanzania tutakuwa tumefanya vizuri zaidi. Changamoto ambayo tunayo ukizingatia na maboresho ambayo sasa hivi Serikali imeyafanya, huwa katika upimaji wa nafasi ya nchi katika wepesi wa kufanya biashara, kipimo chao *deadline* ni mwezi wa Tano wa kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa sasa Juni - Julai mambo mengi yamefanywa na Serikali. Juzi tu nilikuwa na mukutano pamoja na Benki ya Dunia Washington na Dar es Salaam, kuhakikisha kwamba tunawasilisha vielelezo vyta kuonyesha ni namna gani kama nchi tumefanya maboresho mbalimbali na tumepeiga hatua katika kuboresho viashiria vile 11 ambavyo vinatumika katika kupima wepesi wa kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kusema kwamba, tumepeata muda wa kuongezewa mpaka Ijumaa ijayo kuweza kuwasilisha vielelezo vingine vyta namna gani tumeweza kufanya makubwa na marekebisho katika mifumo

yetu ya kufanya biashara, ikiwemo kuanzisha biashara, ufungaji wa biashara, taratibu za biashara mipakani pamoja na nyininge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kusema kwamba tumepata muda wa kuongezewa mpaka Ijumaa ijayo kuweza kuwasilisha vielelezo vingine vya namna gani tumeweza kufanya maboresho makubwa na marekebisho katika mifumo yetu ya kufanya biashara ikiwemo kuanzisha biashara, ikiwemo ufungaji wa biashara, ikiwemo taratibu za biashara mipakani pamoja na nyininge. Kwa hiyo, niwatoe hofu Watanzania niwatoe hofu Wabunge kila mmoja atimize nafasi yake tujitahidi kuona ni kwa namna gani tunaboresha huduma hizi na ninaamini itakapofika mwaka 2020/2021 ripoti yetu na nafasi ya Tanzania tutaweza kufanya vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili tumepata pia utaratibu tutawaita wataalam wa Benki ya Dunia Makao Makuu pia waweze kuja ili kuweze kutoa mafunzo na kutoa maelekezo kwa wale viungo au *focal point* wa mazingira ya biashara ya kila Wizara na kila Taasisi maana yake tunao watu hawa, ili waweze kuona ni kwa namna gani watapaswa kufanya maboresho zaidi. Tunaamini tulishafanya kitu kama hiki mwaka 2016 na ilitusaidia sana kama nchi tuliweza kuvuka na kuimarika nafasi takribani saba. Kwa hiyo, tunaamini kati ya mwaka huu mpaka mwaka 2021 tutaweza kufanya vizuri zaidi, muhimu kila mmoja atimize wajibu yake. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma Mbunge wa Viti Maalum kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda.

Na. 424

#### **Kuandaa Wataalam katika Sekta ya Viwanda Nchini**

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA (K.n.y MHE. KITETO Z. KOSHUMA)** aliuliza:-

Ili kuelekea Tanzania ya viwanda, Watanzania wanapaswa kuandaliwa vema ili kushiriki kikamilifu katika viwanda vya ndani.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuandaa wataalam mbalimbali watakaotumika katika kuendesha viwanda nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016 Serikali kupitia Wizara Elimu, Sayansi na Teknolojia ikishirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na wadau wengine ikiwa ni pamoa na sekta binafsi na washirika wa maendeleo ilikamilisha na kuanza utekelezajji wa mkakati wa Taifa wa kukuza maarifa (*National Skills Development Strategy – NSDS 2016*). Mkakati huu ni wa kipindi cha miaka kumi na unaorodhesha mahitaji mbalimbali ya maarifa ambayo wataalam wake wanahitajika ili kuifikisha nchini yetu katika uchumi wa kati wa viwanda tunaokusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha Watanzania wanaandaliiwa vema kushiriki uchumi wa viwanda, Serikali inaendelea kutekeleza mipango mbalimbali ikiwemo kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kama vile ujenzi na ukarabati wa maiundombinu ya shule na kusambaza vifaa vya maabara na kemikali katika shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali inaendelea na mpango wa ukarabati, ujenzi wa miundombinu, ununuzi

wa vifaa vya kisasa vya kujifunzia na kufundishia na kuboresha mitaala katika vyuo na taasisi za elimu. Kwa mfano, ukarabati wa vyuo vya maendeleo ya wananchi, ujenzi na ukarabti wa vyuo vya VETA katika Mikoa na Wilaya pamoja na Vyuo Vikuu nchini. Aidha, katika mwaka 2019/2020 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknologia itaanza ujenzi wa chuo kipywa cha ufundi cha Dodoma (*Dodoma Technical College*) pamoja na kujenga vyuo vya ufundi stadi katika Wilaya 25 ili kuongeza udahili wa wanafunzi katika fani mbalimbali za ufundi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda swali la nyongeza.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ya maswali mawili ya ngongeza. Kwanza niipongeze Serikali kwa majibu mazuri na tunaona mikakati wa Serikali kuelekea Tanzania ya viwanda.

Swali la kwanza, tayari katika mikakati hiyo shule nyingi za sekondari zimejenga maabara ili kutengeza wataalam kwa ajili ya Tanzania ya viwanda, ni lini sasa Serikali watapeleka vifaa vya maabara katika shule za sekondari ambazo zimeshatekeleza ujenzi wa maabara?

Swali la pili, katika Wilaya Malindi tuna Chuo cha Maendeleo Sofi nashukuru Serikali wanakifanyia ukarabari chuo kile lakini kina uhaba mkubwa wa walimu. Je, ni lini Serikali itapeleka Walimu katika chuo cha Sofi ambapo ukarabati wake karibu unakamilika? Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknologia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ni lini Serikali itapeleka vifaa vya maabara katika maabara ambayo imekamilika naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumekuwa tukipeleka vifaa vya maabara mara kwa mara kadri

maabara zinapokamika. Naomba nimhakishie kwamba kwa shule zile ambazo sasa zimekamilisha Serikali inataendelea kupeleka vifaa vya maabara na hata kwenye bajeti ambayo Bunge hili imepitisha vilevile tumeweka fedha za maabara ili kuhakisha kwamba vifaa vinapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Sofi naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu ule wa kukarabati vyuo vya wananchi (*FDC's*), hauishii tu kwenye ukarabati vilevile inaenda kwenye mambo mengine ya kuboresha mazingira yote ya kujifunzia na kufundishia ikiwa ni pamoja na kuajiri walimu, wakufunzi lakini na wafanyakazi ili vyuo vile viweze kuendeshwa kwa uzuri zaidi ndiyo maana tulifanya kitu kinachoitwa *conditional survey* ya kujaribu kuangalia ni mahitaji yapi yanahitajika ili vyuo vyote viweze kupata mahitaji yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie kwamba tayari tulishafanya tathmini ya nini kinahitajika na punde ukarabati utakapokamilika vilevile nimhakikishie kwamba watapata wakufunzi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Stanslaus Shing'oma Mabula Mbunge wa Nyamagana sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Joseph Mkundi.

Na. 425

**Kutenga Maeneo Maalum ya Kutengeneza  
Magari ya Polisi**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI (K.n.y MHE. STANSLAUS S. MABULA)** aliuliza:-

Magari mengi ya Serikali yanafanyiwa *service* kwenye gereji kubwa hapa nchini hii imekuwa tofauti kwa magari yanayomilikiwa na Jeshi la Polisi:-

Je, Serikali haioni kuwa upo umuhimu wa kuwa na maeneo ya kutengeneza na kurekebisha magari ya Polisi ili kulii marishia vitendea kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linayo karakana kuu ya kutengeneza na kurekebisha magari yake iliyopo barabara ya Kilwa Jijini Dar es Salaam. Karakana hili ina matawi katika kila Mkoa nchini nzima, matawi hayo kufanya kazi kwa utaratibu wa Jeshi la Polisi chini ya Komandi ya karakana kuu iliyopo Dar es Salaam ambako kuna mafundi wenye ujuzi mkubwa. Aidha, Jeshi la Polisi kuitia makubaliano ya kimkataba kuna baadhi ya magari ya Jeshi la Polisi hutengenezwa katika karakana za wazabuni waliokubaliana baada ya kupata kibali cha TEMESA.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa dhati kabisa nitambue kazi nzuri na kubwa inayofanywa na Jeshi la Polisi nchini, lakini majibu haya haya hayaakisi hali halisi iliyopo kwenye maeneo yetu kule. Magari mengi ya Polisi yanapoharibika hutegemea zaidi hisani ya wadau mbalimbali hasa Wabunge kuweza kuyatengeneza. Jambo hili linaathiri sana utendaji wa Jeshi letu la Polisi.

Nini sasa mkakati wa Serikali kuhakikisha utaratibu huu unatekelezwa na magari ya Polisi yanatengenezwa katika mazingira mazuri kama utaratibu ulivyoelekezwa na Mheshimiwa Naibu Waziri?

Swali la pili; kama ilivyo kwa tatizo la magari vituo vyetu vya Polisi vinakabiliwa na upungufu mkubwa sana wa vitendea kazi vya kila siku kama mafuta ya magari, karatasi, wino na kadhalika. Jambo hili linaathiri sana utendaji wa kila siku wa Jeshi letu la Polisi lakini hata kuchelewesha haki za wananchi wa kawaida kule kwenye vituo vyetu vya Polisi.

Nini sasa Mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba inawezesha Jeshi letu kupata vifaa vya utendaji kazi vya kila siku kama hivi ili waweze kutimiza wajibu wao wa kila siku?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ambayo inagusa maeneo yote mawili aliyozungumza ni ufinyu wa bajeti. Uwezo wa Jeshi letu la Polisi kutengeneza magari kwa maana ya kiutalam tunao lakini wakati mwininge magari haya wanapohitaji kutengeneza yanahitaji ununuzi wa vipuli na matengenezo makubwa ambayo yanahitaji fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuwapongeza wadau wote mbalilmbali ikiwemo Waheshimiwa Wabunge ambao wameona changamoto hii na wameona umuhimu wa kusaidiana na Serikali kukabiliana na changamoto ya ubovu wa magari yetu katika Jeshi la Polisi. Ninawatia moyo waendelee hivyo nasi Serikali pamoja na Jeshi la Polisi mbali ya kuwa na Serikali inaendelea kuongeza bajeti la Jeshi la Polisi kadri ya hali inavyoruhusu lakini tumekuwa tukibuni mbinu mbalimbali za kuweza kuyarekebisha magari haya yaweze kuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna magari katika Mikoa mbalimbali ambayo tumefanya matengenezo kwa njia hii za ushirikishaji wa wadau. Hii inakwenda sambamba na hoja yake ya pili ambayo inahusu vitendea kazi kwa ajili ya Jeshi la Polisi nami nikuhakikishie kwamba kama ambavyo sote tunatambua jinsi ambavyo uchumi wetu unavyoendelea kukua vizuri hivyo Serikali kuongeza uwezo wa kuhudumia taasisi zake ni imani yangu kwamba changamoto hizi zitaendelea kupungua mwaka hadi mwaka. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Jastine Joseph Monko Mbunge wa Singida Kaskazini.

Na. 426

**Hitaji la Vituo Vya Polisi – Singida Kaskazini**

**MHE. JUSTIN J. MONKO** aliuliza:-

Kumekuwa na changamoto za kiusalama katika Jimbo la Singida Kaskazini kutokana na jiografia yake na rasilimali zilizopo:-

Je, ni lini Serikali itaongeza Vituo vya Polisi katika Kata ya Mughunga, Mgori na Merya ili kuimarisha usalama wa wananchi na mali zao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uhaba wa vituo vya Polisi nchini ikiwemo Kata za Mughunga, Mgori

na Merya. Hata hivyo huduma za kiusalama kwa wananchi wa Kata hizo zinatolewa na vituo vya Polisi vya Misange na Ngimwa kwa uratibu wa kituo cha Polisi cha Wilaya ya Singida Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ujenzi wa vituo vya Polisi kwa nchi nchi nzima unahitaji rasilimali fedha nyingi, Jeshi la Polisi limeweka vipaumbele vya kiusalama katika kutekeleza ujenzi wa vituo hivyo ikiwemo katika Kata ya Mughunga, Mgori na Merya na kadhalika kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwemo wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin Monko swalii la nyongeza.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, pamoja na majibu yake nina maswali mawili madogo ya nyongeza:

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo tumeayaombea vituo vya Polisi yapo mbali sana na vituo ambavyo Mheshimiwa Waziri amevisema ambavyo pia ni chakavu sana. Maeneo hayo ofisi ya *OCD* pia ina magari matatu tu ambayo inahudumia Halmashauri ya Singida *DC* pamoja na Manispaa. Je, Wizara ipo tayari sasa wakati tukisubiri ujenzi wa hivyo vituo kuongeza vitendeakazi magari pamoja na mafuta ili Askari wetu waweze kufanya kazi vizuri? (*Makofii*)

Swali la pili; Jeshi letu la Polisi hasa Singida lina watumishi wachache mno ambao wanatakiwa kutoa huduma katika Halmashauri zetu mbili. Je, Wizara ipo tayari sasa kuongeza idadi ya watumishi hasa Askari katika Ofisi ya *OCD* Singida ili waweze kutoa hudama bora kwa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kweli Jimbo la Singida Kaskazini linahudumiwa na *OCD* wa Singida Mjini na ni dhahili kabisa kwa maana hiyo naweza hoja ya Mheshimiwa Mbunge inahitaji kufuutiliwa na kufanyiwa kazi. Kwa sababu Majimbo mawili eneo lake la kijiografia ni kubwa kwa hiyo nimhakishie Mheshimiwa Mbunge tunalichukua kwa uzito ingawa hatuwezi kumuahidi sasa hivi kwamba tutampatia gari kwa sababu gari hizo hazipo lakini pale ambao zitapatikana tutazingatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili la kuongeza fedha kwa ajili ya huduma zingine ikiwemo mafuta, hili narudia kama ambavyo nimejibu swalii ambalo limepitia kwamba kadri ambavyo hali ya kibajeti itaruhusu basi bajeti ya Polisi ikiwemo huduma ya mafuta itaongezwa katika maeneo yote ni changamoto nchi nzima, ninaamini kabisa hilo Serikali tunalitambua na tumekuwa tukilifanyia kazi kwa kadri hali inavyoruhusu na ninaamini kabisa hali itakuwa nzuri zaidi siku zinavyokwenda mbele kutokana na hali ya uchumi wetu inavyokuwa vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Rashid Mohamed Chuachua Mbunge wa Masasi sasa aulize swalii lake.

Na. 427

#### **Mauaji ya Vijana Wa Bodaboda – Masasi**

**MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA** aliuliza:-

Mwaka 2017/2018 kulitokea mauaji ya vijana wa bodaboda katika Wilaya ya Masasi ambapo vijana wanaokaribia kuwa zaidi ya kumi wameuwawa kikatili na kunyang'anywa pikipiki:-

Je, nini kauli ya Serikali kuhusu matukio haya katika Wilaya ya Masasi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kweli kuwa kulikuwa na mauaji ya vijana zaidi ya 10 katika Wilaya Masasi. Kwa mwaka 2017/2018 kulikuwa na matukio manne ya mauaji yaliyotokea na kuripotiwa katika vituo vya Polisi Wilaya ya Masasi. Hata hivyo, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kutokomeza uhalifu huo kwa kuwakamata watuhumiwa wote ambao wamekuwa wakijihuisha na uhalifu wa aina mbalimbali ikiwemo mauaji. Hatua hizi ni pamoja na kufanya doria na misako ya mara kwa mara katika maeneo tofauti katika Wilaya ya Masasi kutoa elimu kwa waendesha bodaboda juu ya tahadhari ya kuwabeba abiria usiku na kushirikisha jamii yote katika kuwafichua wahalifu walio kati yao ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua swalii la nyongeza.

**MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii ni la muda mrefu na majibu pia ni ya zamani, lakini hali ya mauaji ya vijana wa bodaboda katika Wilaya Masasi bado inaendelea mpaka sasa. Hata wiki tatu zilizopita tumezika vijana wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba swalii la kwanza liwe Mheshimiwa Waziri atoe kauli sasa kwa kuwa Wasaidizi wake kule wameshindwa kudhibiti mauaji haya kauli yake ni ipi ili kuhakikisha kwamba vijana hawa hawapotezi maisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Mheshimiwa Waziri naomba atueleze ni watuhumiwa wangapi mpaka sasa wamekwishafikishwa Mahakamani kwa makosa haya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya Serikali kulingana na hoja ambayo ameizungumza ni kwamba tutaendelea kuhakikisha kwamba tunadhibiti mauaji nchi nzima, hata mimi na yeye Mheshimiwa Mbunge kwa sababu anaonekana kutokuridhika na takwimu ambazo mimi naamini ni sahihi za mauaji ya watu wanenye kwa mwaka 2018/2019, nitakuwa tayari tupange tuende katika Wilaya yake tuweze kuthibitisha hilo, nilifika katika Wilaya ya Masasi lakini tutakwenda tena kwa ajili ya suala hilli kwa sababu suala linahitajika kuchukuliwa kwa uzito unaostahiki. Kwa hiyo, ili kuweza kujua kama ana taarifa ambazo hazijafika katika Jeshi la Polisi tutazichukua na kuzifanya kazi kwa pamoja na Jeshi la Polisi katika eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhusiana na swali lake la kutaka kujua idadi ya watu ambao wamechukiliwa hatua, kwa wale watu wanenye ambao nimewazungumza tayari watu wawili wameshakamatwa na wapo katika hatua mbalimbali za kisheria. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareso, Mbunge wa Viti Malum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Joseph Roman Selasini.

Na. 428

**Mfumo wa *Vehicle Tracking System (VTS)***

**MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. CECILIA D. PARESSO)** aliuliza:-

Mfumo wa *Vehicle Tracking System* umefungwa katika mabasi yote nchini ili kudhibiti mwendokasi kwa lengo la kupunguza ajali za barabarani:-

- (a) Je, mfumo umegharimu fedha kiasi gani?
- (b) Je, mzabuni wa kazi hii kwa nini hakupatikana kwa ushindani kwa kufuata Sheria ya Manunuzi?
- (c) Je, mfumo huu unaendeshwa na kusimamiwa na nani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum kuhusiana na mfumo wa Kuratibu Mwenendo wa Mabasi (*Vehicle Tracking System*), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa *VTS* ni mfumo unaowezesha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za basi likiwa safarini. Taarifa hizo ni pamoja na mwendokasi, mahali basi liliopo, matukio ya ajali, jina la dereva na kadhalika. Taarifa hizi hupatikana baada ya basi kufungwa kifaa maalum cha mawasiliano kinachochukua matukio na kuyarusha kuititia mfumo wa satelaiti na teknolojia ya *Global Positioning System - GPS* pia kuititia mitandao ya simu yenye teknolojia za *Global Pocket Radio System - GPRS* na hivyo kutoa taarifa za basi husika kwa wakati (*real time*). Lengo la kuweka mfumo huo pamoja na mambo mengine ni kudhibiti matukio ya ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba nijibu swalii la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa VTS uligharimu kiasi cha shilingi bilioni 2.4 ambazo zilitokana na mapato ya Serikali kupitia *SUMATRA*.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mzabuni aliyefanya kazi hii ni Kampuni ya *BSMART Technologies* ya Malaysia akishirikiana na Kampuni ya *Computer Centerya* hapa nchini na alipatikana kwa njia ya ushindani kwa mujibu wa kifungu cha 150 cha Kanuni ya Sheria ya Manunuzi, Tangazo la Serikali No.446 la mwaka 2013. Zabuni hiyo ilitangazwa kupitia zabuni ya kimataifa Na.AE/025/2015-2016/HQ/G/22 katika gazeti la *Daily News*la tarehe 14 Januari, 2016 pia kupitia *PPRA Tender Portal, Tanzania Procurement Journal*Toleo No. ISS:1821 VOL IX-No.3 pia zabuni ilitangazwa kwenye tovuti ya *SUMATRA*.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu unasimamiwa na kuendeshwa na *SUMATRA* kupitia kituo maalum kilichoko Mikocheni Jijini Dar es Salaam. Hata hivyo, *SUMATRA* imeingia mkataba na Kampuni ya *TERA Technologies and Engineering Company*kwa ajili ya kufunga vifaa hivyo kwenye magari. Kampuni hiyo ilipatikana kwa ushindani kupitia zabuni (*Invitation for Tenders*Na.AE/025/2016-2017/HQ/G/39 ya tarehe 25 Oktoba, 2017 ambayo pia ilitangazwa kupitia *PPRA Tender Portal, Tanzania Procurement Journal*na kwenye tovuti ya *SUMATRA*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, pamoja na malalamiko makubwa ya wamiliki wa mabasi juu ya upatikanaji wa mkandarasi aliyefunga mfumo huu lakini wenyе mabasi wanalipia kwa kila basi tozo ya Sh.60, 000 kwa mwezi kwa kila basi, tofauti na wenzetu nchi jirani ambao wanalipia Sh.120,000 kwa kampuni nzima. Swali langu, Serikali inanufaika vipi na tozo hii ya kinyonyaj?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, Serikali inasimamia maeneo mengi ambayo fedha za Serikali zinaingia kwa ajili ya kuhakikisha kwamba imedhibiti upatikanaji wa maduhuli ya Serikali. Ni kwa nini Serikali isihamishie mfumo huu *Police Traffic* ili wakauendesha na Serikali ikawa na uhakika wa kupata hayo maduhuli yake yote kuliko kwa njia hizi za panya na malalamiko kama ilivyo sasa hivi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Selasini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo zinazotozwa kwa ajili ya kufanya *service* ya *VTS* kwa mabasi mbalimbali ilikuwa ni kikao kati ya wamiliki pamoja na wakandarasi mbalimbali ambapo wamiliki waliwapendekeza kwa *SUMATRA* kwa ajili ya kufanya *service* hiyo. Kwa hiyo, pale *SUMATRA* haikingilia mapatano kati ya wenye mabasi na wamiliki. Hata hivyo, kama kutakuwa na mapendekezo ya wenye mabasi kutaka aina nytingine ya mfumo wa kufanya *service* ya vifaa hivyo sisi kama Serikali tuko tayari kupokea na tutawashauri *SUMATRA* waweze kutekeleza.

Mheshimiwa naibu Spika, kwenye swalii lake la pili, Serikali inaendelea kudhibiti mapato kupitia vyanzo mbalimbali lakini inaendelea kutengeneza wigo mpana wa kushirikisha hata sekta binafsi nazo kuweza kufanya shughuli kama hizo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa viti Maalum sasa aulize swalii lake.

Na. 429

## **Fidia Kutokana na Wanyama Waharibifu wa Mazao**

**MHE. GIMBI D. MASABA** aliuliza:-

Wananchi wa Wilaya ya Itilima, Mkoani Simiyu huvamiwa na kuharibiwu mazao yao na wanyama aina ya tembo na Serikali hutoa fidia kidogo na wakati mwingine kutowafidia kabisa:-

Je, Serikali inatoa ahadi gani kwa wakulima juu ya fidia kwa waathirika wa uvamizi huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vinavyoathiriwa na uvamizi wa wanyamapori hasa tembo katika Wilaya ya Itilima ni vile vinavyopatikana na Pori la Akiba Maswa. Kutokana na changamoto hiyo, Wizara huchukua hatua kadhaa ili kunusuru maisha na mali za wananchi. Hatua hizo ni pamoja na kushughulikia matukio ya uvamizi wa tembo kwa haraka iwezekanavyo pindi yanapojitokeza. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi kuhusu namna ya kujilinda na kuepuka kulima kwenye shoroba na mapito ya wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekuwa ikitoa kiasi fulani cha fedha kwa wananchi wanaoathirika na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu ikiwa ni kifuta jasho na kifuta machozi na siyo fidia kwa mujibu wa Kanuni za mwaka 2011. Mfano, katika kipindi cha miaka miwili ya 2016/

2017 na 2017/2018 jumla ya Sh.35,614,000 zimelipwa kwa wananchi 336 wa Wilaya ya Itilima.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa sasa Wizara imepokea maombi ya malipo ya kifuta jasho na kifuta machozi ya wananchi 238 kutoka katika vijiji 7 vya Nyantungutu, Ndingho, Ngwalali, Pijulu, Mbogo, Mwamtani B, Lungwa na Longalombogo. Wizara inaendelea kuhakiki maombi hayo na itawalipa wananchi baada ya kujiridhisha na hatua za uharibifu na kiwango cha kifuta machozi wanachostahili kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kiasi kinacholipwa ni kidogo na Serikali inatambua suala hili ambapo kwa sasa Wizara inafanya mapitio ya sheria na kanuni za uhifadhi wa wanyamapori, moja ya masuala yanayozingatiwa katika mapitio hayo ni suala la kifuta jasho na kifuta machozi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, swali la nyongeza.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, ifahamike kuwa gharama za kukodisha mashamba zinapanda kila siku, unakuta kukodisha hekari moja ni Sh.200,000, uandaaji wa shamba ni kama Sh.300,000 bado ushuru wa Serikali. Je, Serikali haioni kwamba sasa inatakiwa kuweka mkakati wa lazima kuhakikisha wananchi hawa wanapata kifuta machozi ambacho kinastahili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa tatizo hili ni kubwa sana na utafiti umeonyesha kuwa miti ya pareto, pilipili, mizinga ya nyuki inasaidia kuwafukuza wanyama hawa. Je, Serikali ina mpango gani kuanzisha kampeni mahsus kuhakikisha kwamba wanapanda hiyo miti kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nikiri kwamba swali hili limeulizwa mara nyingi sana hapa Bungeni na matukio ya wanyama kama tembo kuendelea kuharibu mashamba yanaendelea katika maeneo mengi na hivi karibuni Kalambo, Same yameendelea kusumbua. Kwa hiyo, tunakiri kwamba tunahitaji kuwa na mkakati kama nchi wa kuangalia namna tunavyoweza kuendelea kulinda mali za wananchi pia na maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakubaliana na swali lake la pili kwamba kama Serikali tunahitaji mkakati na tumewaelekeza watu wa *TFS* kuhakikisha kwamba wanatoa elimu na kusaidia kusambaza mizinga ya nyuki katika maeneo yote ambayo yamekuwa yakipata athari za wanyama hawa mara kwa mara. Pia katika mikutano yote ya hadhara tumekuwa tukihamasisha upandaji wa pilipili. Katika maeneo mengi zao za pareto siyo maarufu lakini limeaminika kwamba linapokuwa limepandwa kwenye mipaka ya mashamba linasaidia kuzuia tembo wasisambae. Kwa hiyo, tunachukua ushauri wa Mheshimiwa Mbunge tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu kifuta machozi, ni kweli kwamba hata lugha inayotumika kwenye majibu yetu ni kifuta jasho na kifuta machozi sio fidia na gharama za kuandaa shamba heka moja zinakadiriwa kuwa takribani Sh.300,000 mpaka Sh.350,000 ambapo sisi kwenye taratibu zetu tumekuwa tukilipa pesa isiyozodi Sh.100,000. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge moja ya maeneo ambayo tunayarejea sasa kuyaangalia vizuri ni kuangalia gharama kutokana na hali halisi ya sasa zikiwemo gharama za uandaaji wa mashamba pamoja na mbegu

na mambo mengine. Kwa hiyo, tumemaliza hatua ya wadau wa ndani na tunajielekeza sasa kupata maoni ya wadau wa nje na mara taratibu hizo zitakapokamilika tutakuwa tumefikia kwenye kiwango ambacho kinaweza kikawa angalau ni cha kuridhisha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete, sasa aulize swali lake.

Na. 430

**Ushirikishwaji wa Jamii Katika Usimamizi wa Maliasili**

**MHE. MBAROUK SALIM ALI** aliuliza:-

Je, ni mafanikio gani yameweza kupatikana katika kushirikisha jamii katika jitihada za usimamizi wa maliasili nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya Ushirikishwaji wa Jamii katika Usimamizi wa Misitu nchini (*Participatory Forest Management*) inatekelezwa katika nyanja kuu mbili: Kuwashirikisha wananchi katika usimamizi wa misitu iliyopo kwenye ardhi ya vijiji (*Community Based Forest Management*) na kuwashirikisha wananchi katika kusimamia hifadhi ya misitu kwa ubia na Serikali (*Joint Forest Management*). Madhumuni ya dhana hii ni kuwapa fursa wananchi kushiriki katika usimamizi na uhifadhi endelevu wa rasilimali za misitu iliyopo katika maeneo yao hali wakiboresha maisha yao

kupitia mapato mbalimbali yanayopatikana kutokana na misitu iliyopo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonyesha jumla ya hekari milioni 7.7 zimehifadhiwa kupitia dhana hii ya ushirikishwaji wa jamii. Aidha, dhana hii imesaidia sana katika kupunguza matukio ya uharibifu wa misitu kama ukataji wa misitu hovyo, uchomaji wa mkaa holela na matukio ya moto yaliyokuwa yakifanyika katika misitu husika katika misitu ya hifadhi ya mazingira asilia (*nature reserves*). Ushirikishwaji huu umekuwa ni nyenzo muhimu ya kufanikisha ustawi wa misitu ambayo mingi kati ya hiyo ni misitu ya lindimaji (*catchment forest*).

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo faida mbalimbali ambazo jamii husika imefaidika kupitia dhana hii ikiwepo kupata msamaha wa mirahaba ya Serikali juu ya mazao ya misitu, kubakiza asilimia 100 ya mapato yatokanayo na mauzo ya mazao ya misitu japokuwa kodi zingine kama kodi ya mapato, Kodi ya Ongezeko la Thamani zimeendelea kulipwa, kubakiza tozo ya faini mbalimbali na utaifishaji wa mazao ya misitu na vifaa kutokana na uvunaji haramu katika misitu ya hifadhi ya kijiji. Aidha, sehemu ya fedha zinazopatikana zimetumika katika shughuli za maendeleo ya vijiji kama kujenga vyumba vya madarasa, zahanati, nyumba za watumishi, walimu na waganga, kutengeneza madawati na kuchimba visima. Vilevile sehemu nyingine ya fedha hiyo imeendelea kutumika katika shughuli za usimamizi wa misitu ikiwemo kununua vifaa vya walinzi wa misitu hiyo ikiwemo sare, buti, filimbi, balskeli na kadhalika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, swali la nyongeza.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri, lakini mimi swali langu lilikuwa linajumuisha maliasili zote kwa ujumla ingawaje yeye amekwenda *very specifically* kwenye misitu, lakini hayo tuache.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, zoezi hili la ushirikishwaji wa jamii ni la muda mrefu kwa kweli, inasikitisha kwamba bado kuna malalamiko mengi ya migogoro na mambo mengine mengi. Nilitaka kujua ni kwa nini mpaka leo hii *WMA*'s nydingi hawapati gawio lao kwa wakati na kwa ukamilifu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, pamoja na miradi mingi ambayo inafanywa na Serikali katika jamii hizi ambazo zimezungukwa na maliasili hizi ni sawa lakini jamii hizi ni maskini wa kutupwa na miradi mingi imemelekea zaidi kwenye miradi ya kijamii. Je, Serikali haioni kwamba sasa kuna haja au ulazima wa kubadilisha mwelekeo na kuelekeza nguvu zao zaidi kwenye miradi ya kiuchumi na kuwapatia taaluma wananchi ili waweze kujikimu? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anasema swali lake lilikuwa linauliza maliasili kwa ujumla na ili kumjibu swali hilo labda pengine ningehitaji nusu saa nzima kwa sababu kama unavyofahamu maliasili kwa ujumla *almost* asilimia 50 ya nchi hii iko kwenye maliasili. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge kama ana swali la nyongeza tunaweza tukawasiliana ili kuweka vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kufahamu kwa nini *WMA* nydingi hazipati migao yake ya fedha kwa wakati na kwa kiwango cha thamani halisi. Naomba kwanza nitoe maelezo mazuri kwamba *WMA* ni jumuiya ambazo zinaanzishwa na vijiji kwa kutenga maeneo yao wanaanzisha jumuiya ambayo wanatafuta mwekezaji ambaye wanaingia naye mkataba kwa kutumia vikao mbalimbali wanakuwa na uongozi wao ambao unawajibika

moja kwa moja kwenye kusimamia maslahi ya WMA. Hapa katikati tulirekebisha kanuni baada ya kuona tulikuwa na viongozi wengi ambao walikuwa wanapokwenda kwenye vikao hivi vya WMA wanazidiwa maarifa na wawekezaji tukarekebisha kanuni ili kuruhusu aina fulani ya elimu ili iweze kutumika lakini jumuiya ya WMA yenyewe imerudi na malalamiko kwamba inataka watu wote ili mradi anajua kusoma na kuandika waingie kwenye uongozi wa WMA. Kwa hiyo, hii ilikuwa ni changamoto lakini tumetoa maelekezo maalum kupitia Mkurugenzi wa Wanyamapori kuhakikisha kwamba inatoa msaada wa kitaalamu na kitaaluma katika usimamizi wa WMA ili iweze kupata maslahi yake kwa mujibu wa mkataba walioingia na mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, jamii nyingi ambazo zinazunguka maeneo haya yenyewe maliasili ni maskini na kwa sababu Serikali labda imejielekeza zaidi katika miradi ya kijamii kama shule na kadhalika. Miradi yote inayofanywa na Mapori yetu ya Akiba na Hifadhi za Taifa na WMA ni miradi inayochaguliwa na vijiji vyenye. Viji viinakaa na kutenga miradi ya kipaumbele na vinapeleka muhtasari wa makubaliano haya kwenye mamlaka husika ya hifadhi, ndiyo inakwenda kujenga au kutoa msaada huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumeanza hivi karibuni sasa kuweka *package* ya kutoa elimu ya fursa mbalimbali ambazo zipo katika maeneo yanayopakana na hifadhi ili kuwaruhusu wananchi hawa kushiriki moja kwa moja kwenye mapato na biashara ya hifadhi na utalii yanayopakana na maeneo yao ya vijiji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba tu nikushukuru kwamba maoni yako na ushauri wako tayari tumeanza kuufanya kazi na tunashukuru kwa mtazamo huo na ndiyo mtazamo wa Wizara kuanzia sasa kuwashirikisha wananchi wote katika farsa ambazo zinapatikana katika maeneo yao.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti sasa aulize swali lake.

Na. 431

## **Mahitaji ya Umeme Kwenye Maeneo ya Delta Kibiti**

**MHE. ALLY S. UNGANDO** aliuliza:-

Jimbo la Kibiti lina Kata 5 na Vijiji 17, sawa na Vitongoji 72 ambavyo vipo kwenye maeneo ya Delta lakini havina umeme:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka umeme kwenye Visiwa hivyo?

(b) Je, utapelekwa umeme wa aina gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kuwapatia huduma wananchi wake Serikali kupitia TANESCO ilifanya upembezi yakinifu kwa ajili ya kupeleka umeme katika vijiji vya Pombwe, Kiongoroni, Mbuchi, Mbwera Mashariki, Mbwera Magharibi, Maporoni, Kiechuru, Msala, Kiasi, Kiomboni, Mchinga na Mfisini vilivyo katika Delta ya Mto Rufiji. Aidha, katika hatua hiyo imesaidia kupata mahitaji halisi na kubaini changamoto zilizopo katika kutekeleza mradi wa kufikisha umeme katika vijiji hivyo. Mradi wa kupeleka umeme katika maeneo hayo tajwa unatarajiwa kutekelezwa kuanzia mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwezi Desemba, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya upembuzi yakinifu kufanyika vijiji vya Mbuchi, Mbwera Mashariki na Mbwera

Magharibi vitaunganishiwa na umeme wa Gridi ya Taifa kutoka Muhoro umbali wa kilomita 40. Ujenzi wa njia ya umeme itatumia nguzo za zege kwa kuwa maeneo mengi ni chepechepe na oevu. Vijiji vingine vilivyobaki vitapelekewa umeme wa *solar* kwa kuwa ujenzi wa laini ya umeme wa Gridi kupeleka katika vijiji hivyo umekuwa na changamoto kutokana na jiografia ya maeneo hayo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Seif Ungando swalii la nyongeza.

**MHE. ALLY SEIF UNGANDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, nina maswali mawili ya nyongeza, moja kwa kuwa sasa wananchi hawa wa Delta wamesubiri sana kwa muda mrefu umeme wa *solar*; Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuwapelekea hata taa katika wakati huu mfupi ili waweze kujipatia huduma kwenye vituo vya afya na shule?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii langu la pili, kwa kuwa wananchi wa Lungungu, Nyamatanga, Lwaluke, Kikale, Mtunda, kuna laini kubwa ambayo imepita na tayari kazi imekamilika. Je, lini umeme utakwenda kuwashwa kwenye maeneo hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge Ungando hii ni mara ya tatu anawaulizia wananchi wa Visiwa vya Delta, kwa kuwa ni Mbunge wa Mkoa wa Pwani natambua Visiwa hivyo na nimefanya ziara kimoja hadi kimoja vyote pamoja naye Mheshimiwa Mbunge Ally Seif Ungando.

Mheshimiwa Naibu Spika, atakubaliana na mimi kwamba kwa kuwa Serikali yetu ina nia ya kufikisha umeme vijiji vyote nchini, na kwa kuzingatia yapo maeneo kama 89 hivi ambayo yako Visiwani na wao lakini wana haki ya kupata umeme. Ndiyo maana kuitia Wakala wa Nishati

Vijijiini (*REA*) Serikali iliamua kufanya upembuzi yakinifu kuainisha mahitaji na kumpata mzabuni mkandarasi ambaye atafanya kazi hiyo na mchakato huo unakamilika tarehe 26 Juni, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza ameainisha kwa kuwa huu muda wa mchakato mpaka mkandarasi, inawezekana ikachukua muda mrefu anauliza namna gani Serikali inaweza ikatumia mkakati wa muda mfupi wa kuwezesha hususan taasisi za umma ikiwemo kituo cha afya cha Mbwera. Tunaishukuru sana Serikali kwa mara ya kwanza kutupatia fedha za kujenga kituo cha afya Mbwera, kinapatiwa umeme mara baada ya kuanza shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge hilo tumelipokea na Wakala wa Nishati Vijijiini katika maeneo ya Kiongoroni, Kiechuru, Kiasi na Mbwera itafanya kupeleka mfumo wa taa kwa ajili ya taasisi za umma ili zitoe huduma kabla mradi huu wa kupeleka nishati ya *solar* katika maeneo haya kwa ajili ya matumizi ya wananchi na wa taasisi za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, Mheshimiwa Mbunge ameyaulizia maeneo ya Lungungu, maeneo ya Rwaluke, maeneo ya Nyamatanga, maeneo ya Mtunda. Maeneo haya kulikuwa na mradi wa *REA* Awamu ya Pili na mkandarasi hakufanya vizuri lakini Serikali hii inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli iliamua kuanza tena mchakato na maeneo yale ambayo kazi haikukamilika ilipewa *TANESCO* na baada ya kupewa *TANESCO* wameendelea na kazi. Nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge ajiandae ili twende tukazindue kuwasha umeme kuanzia Jumatano wiki ijayo mara baada ya kuhitimisha bajeti yetu ya Serikali. Tutafanya sherehe kubwa sana katika maeneo haya kwa kuwa wamesubiri muda mrefu. Kwa hiyo, niwataarifu wakati wa Kibiti kwamba maeneo haya ambayo mmesubiri Serikali imefanya kazi na tutawasha umeme kwa kishindo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba. Swali lake linaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Devotha Minja.

Na. 432

**Kupeleka Umeme Katika Baadhi ya Kata – Mlimba**

**MHE. DEVOTHA M. MINJA (K.n.y. MHE. SUSAN L. KIWANGA)** aliuliza:-

Kata za Mchombe, Igima, Mbingu, Namwawala na Idete katika Jimbo la Mlimba zilipelekewa mradi wa umeme kwa gharama nafuu lakini mradi huo umefanywa vibaya na hivyo kusababisha wananchi wengi kukosa umeme:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwa wananchi hao?

(b) REA ilikabidhiwa mkandarasi kupima maeneo yatakayounganishwa umeme katika vijiji vya Msolwa, Miembeni, Iduimdembo, Ipungusa, Matema, Lumumwe, Uchindile, Kitete na Ngwasi katika Awamu ya Pili; Je, kwa nini kazi hiyo inasuasua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa umeme kwa gharama nafuu (*Low Cost Design*) katika Mkoa wa Morogoro ulitekelezwa katika vijiji 14 vya Wilaya ya Kilombero. Kazi za mradi zilihusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa

kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 35.2; njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 82.6; ufungaji wa transfoma 262 za KVA 15 na 25; pamoja na kuunganisha umeme wateja 4,671. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 6.935.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Desemba, 2018 vijiji vyote 14 vya Mkusi, Njage, Ngajengwa, Igima, Mbingu, Kisegese, Namawala, Idete Magereza, Miwangani, Katurukira, Mihelule, Mikoleko, *Msolwa Station* na Nyange vilipatiwa umeme na wateja 4,286 waliunganishwa na huduma ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mradi huo wa *Low Cost Design* katika Wilya ya Kilombero hususan Jimbo la Mlimba, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijiini (*REA*) Awamu ya Tatu Mzunguko wa Kwanza inapeleka umeme katika Jimbo la Mlimba katika vijiji vya Ipugusa, Msolwa, Kalengakelu, Miembeni, Iduindembo, Ipungusa, Matema, Lumumwe, Uchindile, Kitete, Idandu na Ngwasi. Kazi zinazofanywa kwa sasa ni pamoja na kusimika nguzo, kuvuta nyaya na kufunga transfoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia utekelezaji wa mradi huu, Kijiji cha Kalengakelu kimepatiwa umeme na wateja zaidi ya 20 kutoka Vitongoji vya Usalama na Samora vimeunganishiwa umeme. Kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivi itakamilika mwezi Juni, 2020, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Haule umekaa nikadhani labda umeridhika unataka akuulizie Mbunge mwenzio wa Morogoro. Mheshimiwa Devotha Minja swali la nyongeza.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nimesikiliza majibu ya Serikali kwa namna zoezi hili linavyokwenda kwa kusuasua hivi, Serikali itafanya juhudu gani za ziada ili ifikapo Juni, 2020 kama alivyosema Naibu Waziri kwamba umeme huo umefika katika Vijiji vya Ipungusa,

Msolwa, Kalengakule, Miembeni, Iduindembo, Ipungusa, Matema, Lumumwe, Uchindile, Kitete, Idandu na Mgiasi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika Manispaa ya Morogoro zipo kata ambazo hazina umeme licha ya kuwepo mjini, kata hizi ni Kauzeni Juu, Kiegea, maeneo ya Mkundi, Magadu Juu, katika Kata ya Tungi maeneo ya Paranganyiki, Kambi A, na B; Je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwa wananchi hao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Devotha Ninja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza Mheshimiwa Devotha Ninja ameulizia ni namna gani Serikali itafanya kuhakikisha ifikapo Juni, 2020 kwamba umeme maeneo hayo yaliyotajwa katika swali la msingi yanapatiwa umeme. Naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge, ni kweli kulikuwa na kusuasua kwa mkandarasi *State Grid* katika Mkoa wa Morogoro lakini hivi ninavyosimama ndani ya Bunge naomba nimtaarifu kwamba kwa wiki ijayo kwanza kwa sasa alishawasha vijiji 18 katika Mkoa Morogoro; na kwa kuwa kulikuwa na tatizo la nguzo, alikuwa na nguzo zaidi ya 900 ambazo zilivyopimwa zilionekana kama haizifai. Ninapozungumza ndani ya Bunge zaidi ya nguzo 700 zimeonekana zinatafaa sasa zinaweza zikaendelea na mradi na wiki ijayo anapokea nguzo 2,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, wiki ijayo atawasha vijiji 16 vikiwemo 6 vya Wilaya ya Kilombero vikiwemo alivyovitaja ambavyo ni Kilama, Kalengakelu, Matema, Iduendemo, Miembeni na Msolwa. Vijiji hivi vitawashwa wiki ijayo na mimi natarajia kufanya ziara katika Mkoa wa Morogoro, tutamwalika Mheshimiwa Mbunge tuambatane pamoja. Sambamba na hilo, kwa hiyo

nithibitishe tu kwamba kwa kweli kama tulivyojipanga na kwa kuwa tumejitahidi kutatua changamoto zinazojitokeza na zipo bado zinaendelea lakini tunakaa vikao mara kwa mara. Tuna uhakika mpaka ifakapo Juni, 2020 tutakamilisha mzunguko wa kwanza *REA* Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ameulizia kwenye Manispaa ya ya Morogoro, naomba nimtaarifau Mheshimiwa Mbunge mwenyewe nimeshatembelea Manispaa ya Morogoro kama mara mbili nikiwa na Mheshimiwa Aboud. Moja wapo ya maeneo ambayo tuliwasha ni maeneo ya Tungi, ni kweli maeneo ni mengi na kwa kuwa Mkoa wa Morogoro una kua sana katika ujenzi wa makazi. Maeneo haya kwa kuwa tumelitambua hilo, kama nilivyosema hapa Bungeni tuliona kwamba licha tu ya Wakala wa Nishati Vijijini kuendelea na kazi ya kusambaza umeme vijijini lakini pia tuitake *TANESCO* nayo ifanya kazi hiyo hiyo na kwa kuwa tumesema bei ya kuunganisha iwe 27,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kulitambua hilo katika mpango mkakati wa ndani ya *TANESCO* na kwa kuwa tumeona tuna umeme wa ziada unaosalia kama Megawatts 300, *TANESCO* kwa mwaka wa fedha 2019 itajielekeza kwanye miradi ya *distribution* (usambazaji wa umeme). Takribani milioni 400 zimeidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kusambaza umeme katika maeneo ambayo yanakuwa kwa kasi yakiwemo Majiji na Manispaa, ikiwemo Manispaa ya hapa Dodoma, Manispaa ya Morogoro, Jiji la Tanga, Jiji la Mwanza, Jiji la Mbeya na maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimthibitishe tu Mheshimiwa Mbunge jana nilikuwa Kondoa kukagua haya maelekezo yalivyoanza. Kweli *TANESCO* wameanza kazi ya kupeleka vijijini umeme na kwa kuunganisha wateja 27,000. Nimehakikisha kweli jana tu wateja zaidi ya 500 wameunganishwa baada ya maelekezo ya Serikali ya Awamu ya Tano kwamba *TANESCO* sasa kazi kubwa ni kutafuta wateja na ipunguze bei ya kuunganisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilithibitishie Bunge lako tunatambua mahitaji, tumejipanga vizuri na tutaendelea kusimamia na kupambana ili lengo hili lifikie. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Willy Qulwi Qambalo.

Na. 433

### **Hati za Kumiliki Ardhi**

**MHE. QAMBALO W. QULWI (K.n.y. MHE. SUSAN A. LYIMO)** aliuliza:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu ucheleweshaji wa kupata hati za kumiliki ardhi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa hapo awali kulikuwepo na malalamiko ya ucheleweshaji wa upatikanaji wa hatimiliki za ardhi. Sababu kubwa iliyosababisha changamoto hiyo ni kuwepo kwa Kamishna mmoja tu kwa nchi nzima aliyeruhusiwa kutia saini hati kwa nchi nzima, hali hiyo ililazimu rasimu zote za hati kuwasilishwa Makao Makuu ya Wizara. Hata hivyo, tangu mwaka 2018 mpaka sasa Wizara imefanikiwa kuanzisha jumla ya Kanda 8 za usimamizi wa ardhi kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali ikiwemo

hiyo. Utoaji wa hatimiliki za ardhi, upelekaji wa huduma za ardhi katika Ofisi za Ardhi za Kanda pamoja na kutumia mfumo wa kielektroniki katika utoaji wa huduma zimeondoa kwa kasi kubwa changamoto ya kuchelewesha utoaji wa hatimiliki kwa wanachi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kuanzishwa kwa Ofisi za Kanda, Wizara imejenga Mfumo Unganishi wa Kutunza Kumbukumbu za Ardhi (*Integrated Land Management Information System*). Mfumo huu unalenga kurahisisha, kuharakisha na kupunguza gharama za utoaji huduma za ardhi. Kwa sasa tayari mfumo huo umeanza kutoa hatimiliki za kielektroniki katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni na Ubungo. Aidha, Serikali imekamilisha ufungaji wa mfumo huo katika Ofisi za Ardhi za Manispaa ya Ilala, Kigamboni na Temeka na utaanza kutumika kuanzia Julai 01, 2019. Serikali inaendelea na utaratibu wa kusimika mfumo huu katika halmashauri zote nchini kwa awamu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Willy Qulwi Qambalo swalii la nyongeza.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, pamoja na majibu hayo ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza. Changamoto kubwa ya upatikanaji wa hatimiliki za ardhi ni pamoja na gharama kubwa zinazohusu upimaji wa maeneo. Jambo ambalo wananchi wengi wanlishindwa hasa pale ambapo upimaji unatakiwa ufanyike kwa kundi kadhaa kubwa la wananchi ili yapimwe kwa pamoja. Kwa nini Serikali isipunguze gharama hizo ili wananchi waweze kupata fursa ya kumiliki ardhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, Waziri wa Ardhi Mheshimiwa Lukuvi alipokuwa Karatu tarehe 07 Machi, mwaka huu aliagiza kufutwa kwa hatimiliki ya ekari 20 katika Kitongoji cha Ngorongoro, Ayalabe, Kata ya Ganako ambayo ilitolewa kinyemela kwa mtu binafsi. Hadi leo ni takribani miezi minne eneo hilo bado halijarudishwa kwa umma;

Je, nini kauli ya Wizara kwa Kamishna wa Ardhi Kanda ya Kaskazini ili kutekeleza agizo hilo la Waziri ambalo wananchi walilishangilia sana? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza amezungumzia kwamba gharama za upimaji ni kubwa na hivyo wananchi wengi wanashindwa kulipa na wakati mwingine wanakuwa wako kundi kubwa wanaopimiwa. Naomba tu nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge ya kwamba gharama za upimaji zimepunguzwa sana katika kipindi hiki cha miaka mitatu na huu mwaka wa nne tumeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukikumbuka wakati tunaanza mwaka 2015/2016, gharama za upimaji ziliwu juu sana ziliwu wanachaji kwa ekari moja shilingi 300,000. *Premium* ilikuwa asilimia 15, ikapunguzwa ikawa asilimia 7.5 mwaka wa fedha uliofuatia. Kama hiyo haitoshi mwaka wa fedha uliofuatia 2017/2018 ikapunguzwa ikawa asilimia 2.5 na sasa hivi imepunguzwa ikawa asilimia moja. Maana yake ni kwamba zinakwenda zinapungua kutegemeana pia na uhitaji kama walivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tukumbuke hapa katikati tumekuwa na zoezi kubwa la urasimishaji ambalo limechangia katika kupima maeneo mengi sana. Wakati wanaanza gharama ziliwu kubwa, ziliwu kwenye kama 250,000 mpaka 300,000 lakini kwa sasa kuna watu wanapimiwa kiwanja kwa shilingi 60,000; kuna watu wanapimiwa kwa 150,000; kuna watu wanapimiwa kwa 90,000, mifano tunayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Halmashauri ya Chemba nadhani wako kwenye 90,000; ukienda kwenye Halmashauri ya Mkinga wako kwenye 90,000; kwa hiyo zinakwenda zinashuka pia kutegemeana na uhitaji wa watu,

kadri unavyokuwa na *volume* kubwa ya kazi na bei inapungua. Maeneo mengi sasa hivi yamepimwa kwa njia ya urasimishaji lakini katika kaya zinazopimwa kwa taratibu za kawaida gharama bado siyo kubwa kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amelalamikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili amezungumzia kufutwa kwa hatimiliki katika eneo la shamba moja katika Eneo Lake. Naomba niseme Mheshimiwa Waziri kutamka kwamba hati hiyo ifutwe ni jambo moja, lakini jambo la pili ni *process* pia kuhakikisha inafutwa na umiliki wake unaanza tena upya kwa namna itakavyokuwa. Unapofuta zile hatimiliki haina maana kwamba basi hapo hapo wanaanza kugawiwa, kuna utaratibu ambao lazima Mheshimiwa Rais aidhinishe na ikiidhinishwa inarudi kwa Halmashauri husika na kuwekewa mpango maalum kwa ajili ya matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haufutwi tu ukaletwa kwa wananchi moja kwa moja, unakuwa pia na maelekezo ya namna ya kupanga matumizi kutegemeana na mahitaji yalipo. Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie tu kwamba ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri iko pale pale na muda utakapokamilika basi tutawaleta utaratibu wa matumizi mtakayokuwa mmejandalia.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali. Nitaleta matangazo tuliyonayo hapa mezani.

Tunaanza na tangazo la wageni walioko Bungeni siku ya leo. Kwanza ni wageni wangu, mgeni wa kwanza ni Mheshimiwa naona nimempa na uheshimiwa leo, lakini ni Wakili msomi wa kujitegemea aliyewahi kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM (*NEC*) kutoka Mkoa wa Mbeya Kapteni Mstaafu Samboye Shitambala. Karibu sana (*Makofi*)

Pia Waheshimiwa Wabunge, ninao wageni wengine wageni 10 ambao ni Viongozi wa Benki ya *NMB*, wa kwanza ni ndugu Juma Kimori ambaye ni Mkuu wa Kiltengo cha

Ukaguzi wa ndani *NMB*, karibu sana. Tunaye pia ndugu Abraham Augustino ambaye ni Meneja Kanda ya Ziwa, kwa maana ya Mwanza, Kagera, Mara na Shinyanga, karibu sana. Tunaye pia ndugu Badru Iddi ambaye ni Meneja Kanda ya Dar es Salaam kwa maana ya Dar es Salaam, Pemba na Unguja, karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia ndugu Sospeter Magesse ambaye ni Meneja Kanda ya Magharibi yaani Tabora, Kigoma, Geita na Simiyu, karibu sana. Tunaye pia ndugu Dismas Prosper ambaye ni Kaimu Meneja Kanda ya Mashariki yaani Morogoro na Pwani, karibu sana. Tunaye pia ndugu Aikansia Muro ambaye ni Meneja Kanda ya Kaskazini yaani Arusha, Kilimanjaro na Tanga, karibu sana. Tunay vile vile ndugu Janeth Shango, ambaye ni Meneja Kanda ya Kusini yaani Mtwara, Lindi na Ruvuma, karibu sana. (*Makofi*)

Vile vile tunaye ndugu Vincent Mnyanyika ambaye ni Meneja Idara ya Mahusiano na Mawasiliano, karibu sana. Tunaye pia ndugu Richard Mwariba ambaye ni Kapteni ya timu ya mpira *NMB*, karibu sana. Tunaye pia ndugu Nsolo Mlozi ambaye ni Meneja wa Kanda ya Kati yaani Dodoma Singida na Manyara, yeye pia ndiye msimamizi wa Ofisi ya Makao Makuu Dodoma, karibu sana. (*Makofi*)

Tunae pia Mzee Kikumbi Mwanza Mpango maarufu kama King Kiki. Waheshimiwa Wabunge huyu ni mwanamuziki maarufu. Nadhani hayo makofi yanaashiria kwamba... na leo naona amevaa kitambaa cheupe, kwa hiyo, karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge na kundi la kwanza ni wageni 22 wa Mheshimiwa Najma Giga ambaa ni Asasi ya Wazalendo na Maendeleo Tanzania (AWAMATA) iliyo na Makao Makuu yake Moshi kutoka Mikoa yote ya Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wa Asasi hiyo ndugu Daudi Mrindoko. Karibuni sana. Wageni hawa pamoja na kwamba tangazo litakuja baadaye lakini

watashiriki Bonanza la *NMB*siku ya kesho. Kwa hiyo mtapata nafasi ya kuwaona wale wanaotoka kwenye mikoa yenu. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu ambaye ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na hawa ni wanafunzi kutoka Chuo cha St. John Kilichopo Jijini Dodoma na wanaongozwa na ndugu Valence Mhobesya, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 27 wa Mheshimiwa Atashasta Nditiye, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Kibondo, Mkoa wa Kigoma wakiongozwa na ndugu John Sikudhani. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 25 wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na ndugu Rahma Juma. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo ambaye ni Naibu Waziri wa Madini na hawa ni rafiki zake kutoka Tegeta Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na ndugu Alex Milinga. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa ambaye ni Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni ndugu zake kutoka Ushetu Mkoa wa Shinyanga wakiongozwa na ndugu Clement Madinda. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 16 wa Mheshimiwa Fatmah Toufiq ambao ni wasaidizi wa kisheria kutoka Halmashari zote za Shinyanga wakiongozwa na ndugu John Shija. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa Toufiq anao wageni wengine wawili, mmoja ni binti yake ambaye ni mwanafunzi wa Virginia

*Technical University cha Marekani na huyu ni ndugu Asha Habib Shayo, karibu sana na huyu ameambatana na Katibu Mwenezi wa CCM kutoka Wilaya ya Chamwino Dodoma ndugu Sostenes Tumbo, karibu sana. (Makof)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Oliver Semguruka ambaye ni mume wake ndugu Cosam Nyamtera, karibu sana. Pia yupo na mtoto wa Mheshimiwa Oliver Semuguruka ndugu Vanessa Cosam, simameni kwanza Waheshimiwa Wabunge hawajawaona vizuri, karibuni sana. Nadhani Waheshimiwa Wabunge wamefurahi sana kumwona shemeji yao. Kwa hiyo ni jambo jema. Karibuni sana. (Makof)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Khadija Nassir Ali ambaye ni mtoto wake na huyu ni ndugu Abdulrahman Festo Mselia, sijui yuko wapi huyu mtoto wetu jamani. Mtoto wa Mheshimiwa hebu simama kidogo, karibu sana. Mheshimiwa Khadija hajaleta taarifa za ziada hapa kama yeye ni mama mdogo ama vipi, lakini ni mtoto wake. (Makof)

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Joseph Haule ambaye ni mbunifu wa mavazi ya asili kutoka Dar es Salaam na huyu ni ndugu Joktan Maluli maarufu kama Makeke. Karibu sana. (Makof)

Waheshimiwa Wabunge, leo tunashukuru Mheshimiwa Keissy simuoni hivi maana angekumbushia michango ya Waheshimiwa Wabunge, maana nakumbuka lile vazi Waheshimiwa Wabunge lilitanya sherehe ifane sana ya kukusanya fedha. Kwa hiyo karibu sana ndugu Makeke na sasa kwa sababu yuko hapa Waheshimiwa Wabunge wanaohitaji mavazi kama hayo, basi wanaweza kumwona ili aweze kuwatengenezea. (Makof)

Tunao pia wageni 117 wa Mheshimiwa Grace Tendega na Mheshimiwa Anastazia Wambura ambao ni wanachama wa Chama cha Wajane Tanzania (*TAWIA*) Kanda ya Kaskazini kutoka Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro wakiongozwa na

Mratibu wa *TAWIA* Kanda hiyo ndugu Julieth Omary. Karibuni sana akinamama. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 12 wa Mheshimiwa Justin Monko ambaao ni watumishi Ofisi ya Mbunge na Wazee wa CCM Kata ya Kanoda, Mkoa wa Singida wakiongozwa na Diwani Kata ya Iliongero Mheshimiwa Issa Mwiru, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 27 wa Mheshimiwa Neema Mgaya ambaao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na ndugu Rahma Juma, hawa nadhani walishatambulishwa, nadhani wanao wenyeji wengi hapa Bungeni. Karibuni tena.

Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Frank Mwakajoka ambaao ni watumishi wastaa fu wa Reli ya *TAZARA* kutoka Mlimba wakiongozwa na ndugu John Ngaraguza, karibuni sana wazee wetu. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambaao ni ndugu zake kutoka Mkao wa Mbeya wakiongozwa na ndugu Lucia Mwakalinga. Nadhani pengine hawajapata fursa ya kuingia, siwaoni lakini pengine watapata nafasi baadaye. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambaao ni wadogo zake kutoka Kinyerezi Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Diwani wa Kata ya Rungembwa Mheshimiwa Patrick Mwihava, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Anthony Komu ambaye ni mtafiti na huyu ni ndugu Aikande Kwayu, sijui amekaa upande gani lakini karibu sana ndugu Kwayu. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 13 wa Mheshimiwa Amina Mollel ambaao ni wanafunzi waliosoma shule ya Kibosho Girls kuanzia 1985 hadi 1993 wakiongozwa na Sr. Mary Consolatha Shayo,

karibuni sana. Karibuni sana mabinti wa siku nydingi ambao mmesoma Kibosho *Girls. (Makof)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, wa kwanza ni ndugu Benedict Maregesi ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Musoma, karibu sana Mwenyekiti. *(Makof)*

Tunaye pia ndugu Fidelis Manyerere ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Kata ya Nyasho, karibu sana. *(Makof)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge hili linawakumbushia kwa sababu tulishatangaza jana jioni lakini tutalirudia tena leo. Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kwamba siku ya Jumamosi kesho tarehe 22 Juni, 2019 kutakuwa na michezo mbalimbali itakayochezwa katika timu ya Bunge na timu ya Benki ya *NMB*. Ratiba ya michezo ni kama ifuatavyo:-

Saa 12.30 mpaka saa 1.30 asubuhi matembezi kuanzia viwanja vyta Bunge mpaka uwanja wa Jamhuri; Saa 1.30 mpaka saa 2.30 asubuhi, mazoezi ya viungo ambayo yatafanyika uwanja wa Jamhuri, lakini saa 2.30 mpaka saa 3.00 asubuhi kuvuta kamba (*tug of war*) na hili pia litafanyika uwanja wa Jamhuri kuanzia saa 3.30 mpaka saa 4.30 asubuhi mpira wa wavu (*volley ball*) katika uwanja wa mambo poa, lakini pia saa 8.00 mpaka saa 9.00 alasiri mpira wa kikapu (*basketball*) katika uwanja wa Jamhuri. Saa 9.00 mpaka saa 10.00 mpira wa pete (*netball*) nao utafanyika uwanja wa Jamhuri. Saa 10.00 mpaka saa 12.00 jioni mpira wa miguu (*football*) na wenyewe utafanyika Jamhuri. Saa 12.00 mpaka saa 12.30 jioni ugawaji wa makombe, medali na zawadi za washindi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya michezo hiyo, wote mnakaribishwa kwenye mchaparo (*cocktail*) utakaofanyika kwenye ukumbi mpya wa *Mckee Capetown Kisasa Complex*, kwa hiyo Wabunge mnakaribishwa wote kwenye hii *cocktail*ni Wabunge wasiocheza na wanaocheza, wote mnakaribishwa. Kwa kumwona Mzee wa kitambaa

cheupe pale juu nataka kuamini kwamba na yeye atakuwepo hilo eneo la tukio ili aweze kuonesha kwamba umri ni miaka tu tunataja kwa idadi, lakini ubunifu na kazi nzuri bado ipo pale pale. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wakati Naibu Waziri wa Ardhi akijibu swali hapa kuhusiana na masuala ya ardhi, nimekumbuka kitu kimoja. Pamoja na jambo zuri la kuwapimia wananchi ardhi hususan kwa wenzetu wa vijijini wanapewa zile hatimiliki za kimila, lakini kumekuwa na utaratibu wanapofika Benki, Taasisi za Fedha hawazitambui zile hatimiliki na hawapatiwi mikopo hawa wananchi wa vijijini. Je, nini kauli ya Serikali kuhusu jambo hili?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hakuna mwongozo wowote ulioombwa hapo kwa sababu ameuliza swali kana kwamba Naibu Waziri atapewa nafasi ya kujibu. Hakuna Mwongozo hapo, Mheshimiwa Joseph Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba Mwongozo wako kuhusiana na hali iliyomo humu Bungeni. Takriban siku tano hivi zinazoendelea humu ndani kuna hali ambayo kiukweli wengine tunashindwa kuvumilia kukaa humu ndani. Baridi ni kali sana na ninavyoolewa hii baridi ni ya kutengeneza sasa sijui wataalam wetu huko chini utaaliam wao umeishia hapa? Naomba Mwongozo wako vinginevyo utakuwa unaona watu wanakaa dakika mbili wanaenda nje, mfano mzuri unaweza ukamwona Waziri wa Fedha alivyovaa, hii hali ni hatari utusaidie. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jambo hili alilosimama Mheshimiwa Musukuma nilishalitolea Mwongozo jana. Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako nikirejea swal 421 kuhusiana na *payroll* na tunajua *payroll/inatumika* na *EPICA*, Serikali imetoa kwamba tarehe 23 itakuwa ndiyo mwisho wa kutumia *EPICA* kama mfumo wa malipo na tunajua halmashauri zetu 185 zote zinatumia mfumo wa *EPICA* na wiki hizi za mwisho ndiyo wanakimbizana kufanya malipo na malipo yanalenga kwa watumishi, wakandarasi na watoa huduma mbalimbali. Naomba Mwongozo wako Serikali kwa nini isisogeze mpaka tarehe 30 kama ilivyokuwa siku zote miaka ya nyuma ili kutoa nafasi kwa Halmashauri zetu kufanya malipo katika kukamilisha Mwaka huu wa Fedha unaoishia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbogo, sasa hilo linahitaji mimi kulitolea Mwongozo au ni la mchango ili Wizara ije ijibui?

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, vyovoyote ambavyo utaona inafaa kwa ruhusa yako itusaidie wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

### **KAULI ZA MAWAZIRI**

**Kauli ya Serikali Kuhusu Mlipuko wa Ugonjwa wa  
Homa ya Dengue Nchini**

**NAIBU SPIKA:** Kauli za Mawaziri, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 49(1), (2) na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge

la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la Mwaka 2016, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu mlipuko wa homa ya *dengue* nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugonjwa wa *dengue* sio ugonjwa mpya. Ugonjwa huu ulianza kutolewa taarifa hapa nchini tangu mwaka 2010 na kutolewa tena taarifa mwaka 2013, 2014, 2018 na mwaka huu 2019. Kidunia inakadiriwa watu milioni 390 huugua ugonjwa wa homa ya *dengue* kila mwaka huku vifo vitokanavyo na ugonjwa huu kwa mwaka vikiwa 40,000 ikilinganishwa na ugonjwa wa malaria ambapo watu milioni 216 huugua ugonjwa huo kwa mwaka huku vifo vikiwa 450,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo katika nchi nydingi duniani zinazoathirika na mlipuko wa ugonjwa huu, mara nydingi hutokeea nyakati za mvua hasa katika maeneo ya mijini ambayo kuna mazalia mengi ya mbu kutokana na kutuwama kwa maji. Ugonjwa huu huenezwa na mbu aina ya *Aedes* ambaye ni mbu mweusi mwenye madoadoa meupe ya kung'aa na ambaye hupendelea kuuma hasa wakati wa asubuhi, mchana na jioni.

Ugonjwa huu huenezwa na mbu aina ya *Aedes* ambaye ni mbu mweusi mwenye madoadoa meupe ya kung'aa na ambaye hupendelea kuuma hasa wakati wa asubuhi, mchana na jioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, dalili za ugonjwa huu ni pamoja na homa ya ghafla, kuumwa na kichwa hususan sehemu za macho, maumivu ya viungo na uchovu. Dalili hizi huanza kujitokeza kati ya siku ya tatu hadi 14 tangu mtu alipoambukizwa virusi vya homa ya *Dengue*. Wakati mwengine dalili za ugonjwa huu zinaweza kufanana sana na dalili za ugonjwa wa Malaria. Aidha, mara chache hutokeea mgonjwa wa homa ya *Dengue*, anapata vipele vidogo vidogo, anavilia damu kwenye ngozi na wengine kutokwa na damu sehemu za fizi, mdomoni, puan, kwenye macho na pia kwenye njia ya haja kubwa au ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka huu 2019, ugonjwa huu umeanza kutolewa taarifa katika vituo vya kutolea huduma za Afya hapa nchini kuanzia mwezi Januari, ambapo hadi tarehe 19 Juni, 2019 jumla ya wagonjwa 4,320 na vifo vinne viliviyotokana na homa ya *Dengue* vimetolewa taarifa huku Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo unaoongoza kuwa na wagonjwa wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifuatayo ni idadi ya wagonjwa na vifo kwa mikoa: Dar es salaam wagonjwa 4,029 na vifo vitatu, Dodoma wagonjwa watatu na kifo kimoja, Tanga wagonjwa 207 na vifo sifuri, Pwani wagonjwa 57 na vifo sifuri, Morogoro wagonjwa 16 na vifo sifuri, Arusha wagonjwa watatu na vifo sifuri, Singida wagonjwa wawili na vifo sifuri, na Kagera wagonjwa viwili na vifo sifuri. Aidha, vifo viliviyotolewa taarifa ni kutoka katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, kifo kimoja, Hindu-Mandal kifo kimoja na Hospitali ya *Regency* vifo viwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka kuripotiwa kwa mlipuko wa *Dengue*, Wizara imeendelea kuimarisha mikakati ya kudhibiti ugonjwa huu, kwanza kwa kuandaa mpango wa dharura wa miezi sita wa kuanzia mwezi Mei hadi Oktoba, 2019 wa kukabiliana na ugonjwa wa *Dengue*. Katika mpango huu yafuatayo yanatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kuangamiza mazalia ya mbu wapevu (*Adults mosquitoes*) na viluwiluwi nchini ambapo Serikali imeshanunua kiasi cha lita 60,000 za viuavidudu (*biolarvicides*) kutoka kwenye kiwanda cha uzalishaji kilichopopo Kibaha kwa ajili ya kuangamiza viluwiluwi katika mazalia ya mbu. Kati ya hizi, Lita 11,400 zimesambazwa kwenye Halmashauri 5 za Mkoa wa Dar es Salaam. Lita 48,600 zinasambazwa kwenye Halmashauri za Mikoa ya Geita (lita 8,092), Kagera (lita 12,308), Kigoma (lita 7,616), Lindi (9,048) na Mtwara (lita 11,536).

Mheshimiwa Naibu Spika, pia lita nyngine 36,000 zimeagizwa na Serikali kutoka kiwandani ambapo zitasambazwa kwenye Mikoa yenye mlipuko wa ugonjwa huu

ikiwemo Pwani, Morogoro Tanga na Singida. Aidha, Wizara imeagiza mashine kubwa sita kwa ajili ya kupulizia mbu wapevu aina ya *Fogging machine* na mashine hizi zinatarajiwu kufika nchini kabla ya mwisho wa mwezi Julai, 2019. Dawa za kunyunyizia mbu aina ya *Acteric* lita 2,000 kwa ajili ya kuua mbu wapevu pia zimeagizwa ambazo zitasambazwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuunda kikosi kazi cha watalaan cha kushughulikia udhibiti wa mbu wanaoeneza ugonjwa wa *Dengue* na Malaria nchini na inategemewa kuwa kikosi kazi hiki kitaimarisha jitihada za udhibiti mbu ndani ya Mikoa na Halmashauri zote nchini hususan zenyenkiango kikubwa cha maambukizi ya *Dengue* na Malaria, yaani Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Morogoro, Lindi, Mtwara, Kigoma, Geita na Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuimarisha uchunguzi na matibabu ya ugonjwa wa Homa ya *Dengue* ambapo Bohari ya Dawa (*MSD*) imeshanunua vipimo 30,000 vya kupima Homa ya *Dengue* na awali Wizara ilielekeza Vituo vya Umma vya kutolea huduma kutoa huduma ya vipimo vya *Dengue* kwa utaratibu wa kawaida wa uchangiaji wa gharama za matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kutengeneza na kusambaza Mwongozo wa Matibabu ya Ugonjwa huu kwa ajili ya watoa huduma katika vituo vya kutolea huduma; tano, kuimarisha ufuatiliaji wa magonjwa nchi nzima kwa kutumia mfumo uliopo wa ukusanyaji wa taarifa, ambapo tunaendelea kupata taarifa za kila siku juu ya mwenendo wa ugonjwa huu na magonjwa mengine; na sita, kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo vya habari pamoja na ujumbe kwa njia ya mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia hatua hizi, takwimu za hali ya maambukizi ya ugonjwa wa *Dengue* zinaonyesha kuwa maambukizi mapya yameanza kupungua kutoka

wagonjwa 2,494 mwezi Mei, 2019 hadi wagonjwa 813 kufikia tarehe 19 Juni, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kumekuwa na changamoto mbalimbali katika kudhibiti mlipuko wa Homa ya *Dengue* nchini. Changamoto hizi ni pamoja na gharama za kupima ugonjwa wa *Dengue* ingawa Serikali kupitia Bohari ya Dawa imenunua vipimo moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji na hivyo kuviuza kwa bei nafuu ukilinganisha na gharama inayotozwa kutoka kwenye baadhi ya Hospitali binafsi, bado wananchi wengi wanashindwa kumudu gharama za uchangiaji matibabu ya ugonjwa wa Homa *Dengue*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ushirikishwaji wa Jamii. Jamii bado haijaweza kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa kampeni ya usafi wa mazingira ambayo ni njia kuu ya kudhibiti mazalia ya mbu; na tatu, watoa huduma za Afya kutokufuata kikamilifu miongozo ya matibabu ya ugonjwa wa Homa ya *Dengue*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge Iako Tukufu kuwa Serikali kupitia Wizara ya Afya, imepitia Miongozo na Kanuni za Kimataifa, ambayo pia ipo katika Sheria ya Afya ya Jamii Na.1 ya mwaka 2009 kuweza kupata mwongozo wa namna bora ya utoaji wa matibabu kwa mlipuko wa ugonjwa wa *Dengue* ambao upo sasa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia sheria hii, viro vipengele mbalimbali ambavyo vimeainisha jinsi gani matibabu ya magonjwa ya milipuko mikubwa kama ya Homa ya *Dengue* inapaswa kutolewa na hii ikiwemo utoaji wa matibabu bure ili kurahisisha udhibiti wa magonjwa ya milipuko yasisambae kwa haraka katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia sheria hii, Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, inayowajali wananchi wake, sasa imeamua kuwa, vipimo kwa ajili ya Homa ya *Dengue*

vitatolewa bure kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vya Umma wakati huu wa mlipuko huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie tena. Kwa kuzingatia sheria hii, Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufulsi, inayojali wananchi wake, sasa imeamua kuwa vipimo kwa ajili ya Homa ya *Dengue* vitatolewa bure kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya vya Umma wakati huu wa mlipuko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali itaboresha matibabu kwa wagonjwa kwa kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa dawa za kutosha na pia itaendelea kuwajengea uwezo wataalam wa Afya sambamba na kuboresha mifumo ya ukusanyaji takwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa tunadhibiti ugonjwa huu nchini, ninaitaka Mikoa na Halmashauri zote nchini hasa zenyenye kiwango kikubwa cha maambukizi ya *Dengue* na Malaria kusimamia kikamilifu kampani za usafi wa mazingira na kuangamiza mbu kwa kunyunyizia dawa kwa ajili ya kuuwa mbu wapevu na kutokomeza mazalia ya mbu. Aidha, natoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikiana na Serikali katika kudhibiti ugonjwa huu kwa kuchukuwa hatua stahiki za kujikinga na ugonjwa huu na kuimarisha usafi wa mazingira na kuangamiza mazalia ya mbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa niaba yenu nyote nadhani tuishukuru Serikali kwa kufanya kipimo hiki kuwa bure. Kwa sababu maeneo mengi ingekuwa changamoto kwa watu wengi. Kwa hiyo, tunawashukuru sana, maana yake hata wasio na bima wanaweza sasa kwenda hospitali kupima. Kwa hiyo, nitoe wito watu wawahii wanapoziona dalili hizi, wakiwa nazo basi wawahii hospitali. (*Makofi*)

Katibu.

**NDG. RUTH S. MAKUNGU - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea, tutaanza na Mheshimiwa Justin Monko, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mhagama na Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, ajiandae.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuanza kuchangia bajeti kuu ya Serikali katika siku ya leo. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nami fursa ya kuweza kusema leo mbele ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara kwa namna ambavyo wametuletea bajeti ambayo kwa kweli imekidhi mambo mengi ambayo Wabunge tumekuwa tukiyatafuta kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni, kwa namna ambavyo wamesimamia Wizara na kuweza kuleta bajeti ambayo kwa kweli imegusa kwenye maeneo mengi ya muhimu hasa katika Sekta za

Miundombinu ambayo ni chachu kubwa sana ya maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimponeze pia Mheshimiwa Rais, kwa kitendo chake cha kukutana na wafanyabishara na makundi mbalimbali ambayo ni muhimu sana katika ukuzaji wa uchumi wa Taifa letu la Tanzania. Amefanya jambo jema. Ombi langu na wito wangu kwa viongozi wengine, wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri walioko hapa, Wakuu wa Mikoa na baadhi ya viongozi wengine huko, wasisubiri tena Mheshimiwa Rais aendelee kuwaita watu lkulu na kuzungumza nao kusikiliza kero zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo kero nyingi, leo kaongea na wafanyabiashara, kesho na kesho kutwa walimu watakuwa na kero, wakulima wanzo kero zao, hatuwezi kusubiri Mheshimiwa Rais aweze kuita makundi yote haya na viongozi wapo. Kwa hiyo, wachukue hatua ili waende kutatua kero za wananchi kwa kuwasikiliza na siyo kutoa tu maelekezo peke yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii ya mwaka huu imegusa kwenye maeneo mengi. Mimi nitazungumzia kidogo upande wa Sekta ya Kilimo. Waheshimiwa Wabunge, waliotangulia wamesema bajeti kwa upande wa kilimo kwa kweli ni ndogo. Nami niseme, sitaki kuzungumza sana, mwaka 2018 nilisema sana kuhusiana na takwimu za bajeti ya kilimo, lakini naomba sana, kilimo ndugu zangu kinahitaji kuongezewa bajeti kwa sababu kinachukua zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania. Ni muhimu sana tukaona namna ambayo tunaweza tukaboresha kilimo chetu sambamba na viwanda ambavyo tunavifungua sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ambavyo tunavianzisha haviwezi kuwa na tija, kwa sababu mwelekeo wote ni wa viwanda ambavyo vitatumia malighafi za mashambani au malighafi za kilimo. Kwa hiyo, naomba sana, tuboreshe kilimo chetu na hasa kilimo cha umwagiliaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wetu bado wanateseka. Tanzania yetu, wakulima wengi ambao tunawategemea ni wakulima wadogo wadogo, sio wakulima wakubwa. Hawa ndio wanahitaji kuangaliwa namna ya kuweza kuboresha mazingira yao, wanahitaji kusaidiwa ili waweze kupata pembejeo, wasaidiwe waweze kupata mbegu na vitu vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumekuwa hata na uvamizi wa ndege ambao baadaye wanavamia mazao. Serikali inapaswa kuchukua jukumu la kuweza kuwasaidia wananchi hao kwa sababu hawana uwezo wa kupambana na wadudu waliokuwepo pamoja na ndege wanaoshambulia mashamba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie zao la alizeti ambalo kwa kweli ni zao kubwa kwa Mkoa wetu wa Singida na hususan Jimboni kwangu. Zao hili la alizeti bado linazo kero kadhaa ambazo naomba sana Mheshimiwa Waziri mtusaidie kuziondoa. Tunawapongeza sana, mmeondoa kero zaidi ya 54 katika bajeti ya mwaka huu ambazo zinawasaidia sana wananchi. Hata hivyo, katika zao la alizeti, kwa mfano mashudu sasa hivi bado yanakuwa na ushuru wa mazao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mashudu siyo mazao, ni *byproduct* ya alizeti. Kwa hiyo, sasa mtu anapokuwa amenunua alizeti, amelipa ushuru wa mazao, halafu baadaye tena kwenye mashudu, anakuja kuchajiwa ushuru wa mazao, nadhani hizi zinakuwa ni kero. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye mashudu, tunayo pia tozo ya shilingi 20,000/= ambayo inatolewa na Wizara ya Mifugo. Pale ambapo unataka ku-*export* mashudu, wanapotaka ku-*export* mashudu kuna tozo ya shilingi 20,000/= kwenye Wizara ya Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye Tume ya *Atomic*, pia iko tozo kwa ajili ya *radiation*, lakini tozo hii siyo *requirement* ya wanunuzi kule nje. Kinachofanya sasa,

matokeo yake sasa, bidhaa yetu hii ambayo ni *byproduct* ya alizeti inakuwa siyo *competitive* kwenye masoko ya nje. Tumeona hapa tumeongeza sana ushuru kwenye bidhaa zinazotoka nje, lakini tuone kwa sababu watakaokwenda kuzitumia bidhaa hizo ni Watanzania hawa hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tuna nia na lengo zuri sana la kuweza kulinda viwanda vyetu vya ndani, lakini tukumbuke Kenya watafanya hivyo, Uganda watafanya hivyo na nchi nyiningine zitafanya hivyo, nasi pia tunataka tuuze nje. Jambo kubwa ambalo tunatakiwa kufanya ni kuona namna ya kupunguza gharama za uzalishaji wa bidhaa zetu, siyo kuongeza zaidi tozo kwa bidhaa zinazotoka nje, lakini tukiweza kupunguza gharama za uzalishaji, tutaweza kushindana kwenye soko..

Mheshimiwa Naibu Spika, Soko hili ni huru. Kwa hiyo, moja ya vitu ambavyo vinafanya gharama zetu zinakuwa kubwa, ni hizi tozo ambazo sisi tunaona kwa kweli hazisaidii na hazina tija kwa wananchi na pengine hata kwa Serikali. Sidhani kama zina ongezeko kubwa sana zinaweza zikawa zinaongeza mapato, lakini zinawafanya wafanyabishara wanaanza kukwepa na kinakuwa ni chanzo pia hata cha kushawishi kwenye masuala rushwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba sana Wizara kuziangalia tozo hizi ili iweze kuziondoa ili ikishaziondoa wananchi wetu, wakulima, kwa sababu mashudu yakipata bei, alizeti itapata bei. Alizeti ikipata bei, wananchi wetu watanufaika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wameanza kukimbia zao la alizeti sasa. Hata Mheshimiwa Kiula hapa, yeye ni mkulima mzuri, sasa ameanza kulima dengu. Wanaogopa kwa sababu limekuwa ni tatizo. Mbegu ni gharama kubwa, halafu ukishalima pembejeo ni tatizo, ndege wanashambulia, lakini bei yake inakuwa ni ndogo mno. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara ijaribu kuangalia, vyanzo vingine na kufuta tozo hizi ambazo kiukweli hazina tija sana kwa ajili ya wakulima wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu, naunga mkono hoja, bajeti hii ya mwaka huu ambayo iewasilishwa, lakini naomba sana Wizara ifanye marekebisho ambayo nimeyaomba kwa niaba ya Watanzania, ili kusudi kuweza kulinda kweli viwanda vyetu na kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanaweza wakanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Bahati Ali Abeid na Mheshimiwa Bhagwanji Maganlal Meisuria ajandae.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Awali ya yote naomba nitoe salamu za pongezi sana kwa Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri sana ambayo anaifanya kwa ajili ya kukuza uchumi na kuboresha maisha ya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya salamu za shukrani zimfikie Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mbunge, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, pamoja na timu yake yote Wizarani. Salamu hizi zinatoka kwa wananchi wa Hanga Ngadinda katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba. Wananchi hawa kwa muda mrefu wamehangaiaka sana kupata eneo la kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hekima kubwa na kwa uzalendo Mheshimiwa Waziri amekubali kuwapa hekta 1,800 ili kutatua tatizo la wananchi hawa. Tunamshukuru sana, sana, sana. Mheshimiwa Luhaga Mpina amekuwa mmoja katika Mawaziri ambao wapo tayari kuchukua maamuzi magumu yanayotatua matatizo ya wananchi. Tunaombia Serikali pia itambue mchango mkubwa wa Waziri huyu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba nijielekeze kwenye kuishauri Serikali katika mambo muhimu yanayohusu kukuza uchumi, hatutapata Tanzania ya viwanda kama hakuna uratibu wa pamoja wa sekta na Wizara zinazotegemeana. Hizi Wizara zinazotegemeana tunaziita *Line Ministry*. Ili upate Tanzania ya viwanda unahitaji uratibu wa pamoja wa Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Viwanda na Biashara pia kwa karibu sana na Wizara ya Ardhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, malighafi asilimia 65 inayohitajika viwandani au niseme viwanda kwa asilimia 65 vinategemea malighafi kutoka katika sekta hizi nilizozitaja ambazo ni sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi, madini lakini ardhi ndio Mama katika haya yote ambayo nimeyataja. Kama hakuna uratibu wa pamoja wa hizi Wizara hatutaipata Tanzania ya viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na eneo la kilimo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye hotuba yake ameondoa vikwazo vingi sana vya biashara, tunamshukuru na tunampongeza sana, hatua aliyochukua itatatu tatizo la kufanya biashara nchini na ufanyaji biashara utakuwa rahisi zaidi, lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesahau sekta Mama ambayo inaa jiri zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania, sekta ya kilimo. Kwenye mchango wangu wakati nachangia Wizara ya Kilimo nilisema, hatutaweza kupata mapinduzi ya kilimo kama hatutawekeza kwenye usambazaji wa pembejeo na usambazaji wa pembejeo vijiji unakwazwa na gharama kubwa za kufungua maduka ya pembejeo na gharama hizo zinachangiwa na *TFRA*, *TPRI*, *TOSC* na *TFDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo hizi Mheshimiwa Wazri Mkuu alizijibbia humu ndani. Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba urejee kwenye majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu hizi tozo zinazokwaza uendelezaji wa sekta ya kilimo. Huwezi kupata mapinduzi ya kilimo kama hautaki kuwekeza kwenye usambazaji wa pembejeo. Sasa mtu wa kijiji anayetaka kufungua duka la kusambaza pembejeo na ninaposema pembejeo maana yake mbegu bora, mbolea

na viuatilifu, kama hivyo havipo huwezi kupata mapunduzi ya kilimo. Kwa hiyo Mhehsimiwa Waziri wa Fedha naomba rejea kwenye majibu ya Waziri Mkuu kaondoe hizi tozo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha ondoa tozo kwenye *TFRA* shilingi 100,000, ondoa tozo kwenye *TPRI* shilingi 320,000, ondoa tozo kwenye *TOSC* na *TFDA* ili mjasiriamali wa kijiji aweze kufikisha pembejeo kwa wakulima wadogo bila hivyo huwezi kupata mapinduzi ya kilimo na usipopata mapinduzi ya kilimo hakutakuwa na Tanzania ya viwanda. Hili ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na kama kutakuwa na fursa ya kushika shilingi Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wote tunaoamini kwamba wakulima ndiyo mtaji mkubwa wa Watanzania na mtaji mkubwa wa CCM tutasimama na tutashika shilingi yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema sekta hizi Mama zisipofanyakazi pamoja hatutapata mapinduzi ya viwanda. Ninaomba pia Waziri wa Fedha akubali kuziratibu hizi Wizara zote nilizozitaja. Ukitiwa kwenye hotuba ya Waziri wa Kilimo ana vipaumbele vya mazao, atakuambia katika msimu huu kipaumbele changu ni mazao moja, mbili, tatu, nne huyo ni Waziri wa kilimo. Ukienda kwa Waziri wa Viwanda na Biashara ukisoma kwenye hotuba yake Waheshimiwa Wabunge mkasome mtaona baadhi ya mazao ambayo yamepewa kipaumbele na Wizara ya Viwanda na Biashara hayapo kwenye vipaumbele vya Wizara ya Kilimo sasa huyu anayeenda kuzalisha viwanda malighafi anazitoa wapi? Kwa hiyo, uone kwamba hapa ni kama hakuna *coordination*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili upate mapinduzi ya viwanda unahitaji *coordination*. Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Nishati na Madini, Viwanda na Biashara na Wizara ya Ardhi mkubali sasa kukaa pamoja, kutengeneza mpango kazi wa pamoja, utaratibu wa *joint planning*, mfanye *joint evaluation* na *monitoring* ili tuweze kuipata Tanzania tunayoitaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maslahi ya muda, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Sana. Mheshimiwa Bahati Ali Abeid atachangia kwa dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Bhagwanji atachangia kwa dakika tano, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ajiandae.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia ingawa ni kwa dakika tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa sana wanayoifanya ya kumshauri Mheshimiwa Rais kwa kuleta maendeleo ya nchi yetu, pia napenda sana niwapongeze Marais wangu wawili kwa kazi kubwa sana wanazozifanya kwa kutekeleza llani ya CCM kwa viwango kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge wa muda mrefu, nimeona llani mbalimbali zinavyotekeliza lakini miaka hii ambayo Mheshimiwa Rais wangu John Pombe Magufuli amekamata madaraka kwa kweli haijawahi kutokea, ni miradi mikubwa tunaiona inayotekeliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini naona miradi mikubwa ya umeme inayoendelea kwa kweli tumefanikiwa kuanza kuzima mitambo inayoendeshwa kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta. Hii ni habari nzuri sana naamini mitambo yote inayozalisha umeme kwa kutumia mafuta itaendelea kuzimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwenye hiyo Nishati. Kwa kweli nimeona kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mpango na kitabu hiki kimeandalisha vizuri na kwa kweli Waheshimiwa Wabunge niseme uwe mtaalam kweli kweli wa kukipinga kitabu hiki, ni kitabu kizuri

sana, kimejifafanua, kina miradi mingi mikubwa ya maendeleo. Naamini miradi hii ikipitishiwa pesa kama tutakavyozipitisha hapa naamini miradi hii itatekelezwa vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimechangia kwa muda mrefu juu ya umeme wa Zanzibar, Umeme wa Zanzibar kwa kweli *ZECO* tulionba sana wapunguziwe bei ya umeme na hatukupata jibu hadi leo, Serikali ilisema inaenda kukaa na itaangalia hilo ingawa nipongeze na nishukuru sana kwa ile VAT ilioondoshwa ni jambo jema sana, lakini kama miradi mizuri inaendelea kutekelezwa na kwa nini *ZECO* wamejenga mitambo yao wenyewe na mitambo hii *TANESCO* wameunganisha wafanyabiashara mbalimbali na hakuna pato lolote wanallowapa *ZECO*.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Kwa nini haiwi sababu basi ya kuona sasa wawapunguzie...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mattar sijui kama una fursa ya kuchangia, maana kila Mbunge akisimama kuzungumzia *ZECO* wewe una taarifa, sijui kama umeizingatia ile Kanuni yetu inataka useme nini. Mheshimiwa Mattar.

## TAARIFA

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kumpa taarifa Dada yangu Mheshimiwa Bahati, kuna vitu vikikugusa unatakiwa lazima uwe unatoa taarifa ili viende vizuri sana. Nimpongeze Mheshimiwa Bahati lakini suala la...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mattar taarifa ni kwa ajili ya ufanuzi wa jambo ambalo analizungumza Mbunge mwingine sasa naona unaanza kwa kumpongeza sasa pongezi tena Mheshimiwa?

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpe taarifa Dada yangu Mheshimiwa Bahati kuhusu suala la umeme, *ZECO* wanauziwa umeme KV Moja ni shilingi 16,500 lakini *ZECO* wanauza umeme shilingi 13,500, kwa hiyo ukiangalia tunauziwa umeme ghali lakini *ZECO* wanakwenda kuza umeme rahisi na tukiangalia hii ni Tanzania moja kwa hiyo tumuongezee Mheshimiwa Bahati tuweze kupungziwa bei ya umeme ili tuweze kwenda vizuri ili wananchi wetu waweze kupata maslahi mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Mattar, Mheshimiwa Bahati ndicho alichokuwa anazungumza kwa hiyo wewe umekichukua chake kimekuwa Taarifa sasa ye ye anatakiwa azungumze nini sasa? Ndiyo maana nasema taarifa ni kwamba unamsikiliza Mbunge amalize hoja yake Je, wewe unatakiwa kuchangia kwenye hicho, kwa sababu la sivyo unauchukua ule mchango wa Mbunge anayesimama ndiyo maana nilikuambia namna hiyo. Mheshimiwa Bahati na kengele imegonga hivyo ninakupa dakika moja malizia muda wako.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Naibu Spika, utakuwa umenionea huyu amenichukulia muda wangu. Mheshimiwa Mattar hiyo taarifa unatakiwa uwe na subira unisikilize kidogo ingawa naipokea. Kwa kweli amenionea muda wangu ameuchukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Mpango atakapokujahapa hebu atupe ufanuzi juu ya umeme huu wa *ZECO*, miundombinu yao wenyewe na miundombinu hiyo wameunganishwa na wateja wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la kumalizia ni wafanyabiashara wa Zanzibar, wenzangu wamelisema sikutaka kurejea jambo hili. Zanzibar ni Kisiwa na uchumi wake unaeleweka. Kama wafanyabiashara hawa wananyanyasika naamini uchumi wa Zanzibar utaendelea kushuka. Wazanzibar au Tanzania nzima wanategemea

kuvuna pato la biashara yao kipindi cha Mwezi wa Ramadhani, lakini wafanyabiashara hawa wengi wamekosa kuza nguo zao Mwezi wa Ramadhani, nguo ziko huko Mombasa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa muda uliokuwa umeongezewa pia umekwisha. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Bhagwanji lakini kabla hajasimama wapo wageni ambao hawakutangazwa.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Wapo wageni wa Mheshimiwa Aisharose Ndogholi Matembe, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Singida na hawa wageni wake ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Manyoni wakiongozwa na Mheshimiwa Joyce Kalikawe ambao wako hapa na wako saba. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani, karibuni sana. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Bhagwanji Maganlal Meisuria atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha na Mipango nakupongeza sana kwa bajeti yako pamoja na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Watendaji wote, kwa sababu ya hiki kitabu walichoandika basi naunga mkono moja kwa moja kwa sababu kitabu hiki kimeandika uhakika na Serikali itasimamia, Wabunge na Watanzania sote tunaunga mkono. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nampa hongera Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Dkt. John Joseph Magufuli kwa kusimamia llani ya CCM, amesimamia wanyonge wote Tanzania kwa kufanikisha kupunguza mambo mbalimbali kama ushuru pamoja na

matatizo mengine, sekta zote amesimamia. Vilevile Rais wangu wa Zanzibar pamoja na Makamu wake wamefanyakazi nzuri Zanzibar kwa kusimamia Zanzibar nzima, maji, umeme pamoja na nyumba, barabara, nawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu barabara; barabara za Tanzania zinatakiwa kuboreshwa kwa sababu wanapakia *container* kutoka Dar es Salaam mpaka kwenda mipakani, pamoja na mizigo midogo midogo, Serikali tunapata ushuru kutokana na mizigo, hawa watu wanapakia mizigo wanafika mpaka sehemu za Burundi, Kenya pamoja na Malawi, nashukuru sana Serikali kusimamia kutengeneza barabara iboreshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu pamoja na Makamu wa Rais wamesimamia Serikali yetu, Mheshimiwa Waziri Mkuu anasimamia Mawaziri wote, Mheshimiwa Waziri Mkuu anasimamia Wabunge wote kwa kushikamana na kufanyakazi nasi tunaunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia kuhusu bandari ya Zanzibar na bandari ya Dar es Salaam. Mheshimiwa Rais amekwenda kutembea nchi mbalimbali na bahati nzuri tumepata Rais wa Congo amekuja kutembelea Bandari yetu ya Dar es Salaam pamoja na reli ya *standard gauge*. Bandari ya Dar es Salaam inatakiwa kupanuliwa kwa sababu meli moja inapita, inatakiwa kupanuliwa ili zipite meli mbili kwa pamoja, kwa hivyo nampongeza Rais na Rais wetu wa Congo wakae pamoja tupate kuiendeleza bandari yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari ya Zanzibar Mpigaduri, naomba Rais wangu wa Muungano amsaidie Rais wa Zanzibar ili bandari ya Mpigaduri itengenezwe kwa sababu *container* nydingi zinakuja na *container* zetu za Zanzibar zinakwamba Mombasa na mahali mbalimbali, hivyo ninaomba Serikali yetu ya Tanzania, naomba Muungano wetu Zanzibar tupate msukumo kutokana na Tanzania, Rais wetu wa Muungano Mheshimiwa Dkt. Magufuli aisaidie

Zanzibar kutengeneza bandari yetu na kuboresha kwa sababu *container* kutoka Dar es Salaam inakwenda mpaka Burundi, inakwenda Kenya mipaka yote basi Serikali tunaongeza kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ya *standard gauge* namshukuru Rais amefikiri Mheshimiwa Magufuli kufanya kitu cha muhimu sana kwa Tanzania itapakia mali mbalimbali, biashara ndogo, biashara kubwa, *container* na wananchi watafaidika kwa hivyo, peleka salama kwa Mheshimiwa Rais hongera sana kwa kutengeneza reli ya *standard gauge*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda, ninaomba Mheshimiwa Rais asimamie viwanda vyote. Viwanda vinatakiwa kuboreshwa kwa sababu viwanda viwo vya aina nyingi, kuna viwanda vya sukari, viwanda vya pamba, tumbaku, alizeti, pamoja na korosho na vingine. Viwanda hivyo lazima tusimamie vifanyekazi, vikifanyakazi viwanda basi tunaongeza mapato na *TRA* wanapata mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bhagwanji muda wako umekwisha, ahsante sana. Ahsante sana Mheshimiwa Bhagwanji. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Mheshimiwa Injinia Lwenge ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante...

**MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima yako, naunga mkono Serikali na bajeti. (*Makofi*)

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Namshukuru Mungu kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu sana kwa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na bajeti, hii nafikiri ni ya nne na sisi Kambi Rasmi ya Upinzani tumetoa mawazo mbadala kuweza kusaidia Taifa letu kusimamia masuala ya uchumi. Tunashukuru kuna wakati mnakubali kuna wakati mnakataa lakini mwisho wa siku Watanzania watajua kwamba sisi tulikuwa tunatoa mawazo kwa ajili ya kusaidia Watanzania wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti zinapotangazwa nchi za Afrika Mashariki kwa siku moja inasomwa na hii imefanywa kimkakati sawasawa na tulivyosaini kama nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi ya Kenya imeweka bajeti yake kiasi cha dola billioni 30.2. Naizungumzia Kenya kwa sababu mimi binafsi naamini vitu vingi sana tunavyofanya sisi wenzetu wanatuangalia tunafanya nini na sisi pia tunawaangalia wanafanya nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti yetu imefika shilingi triliuni 33, wakati wenzetu bajeti yao ukichukua Burundi, Rwanda, Uganda na nchi zingine za Afrika Mashariki, Kenya peke yake imetuzidi. Kwa nini nazungumzia hilo? Soko lillipo hapa nchini ukienda kwenye *spices* zote kwenye maduka ya jumla vifaa vya Kenya vimejaa hapa nchini na sisi kama nchi ya Tanzania tunajinasibu ni nchi ya viwanda kwa miaka hii minne hizi bajeti tumezizungumzia ni kitu gani ambacho tumezalisha na kimeuzika katika soko la Afrika Mashariki kama wenzetu walivyofanya? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango na timu yake nzima ni lazima tufanye kazi kimkakati ili kuweza kuinua uchumi wa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wenzetu wanatangaza bajeti yao sisi Waziri wetu Mheshimiwa Dkt. Mpango anazungumzia tunaelekea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni mtu gani achaguliwe atoke CCM. Wakati huu siyo wa kuzungumzia mambo ya vyama ni wakati wa kuzungumzia mustakabali wa Taifa hili hasa katika mambo

ya kiuchumi. Kwa hiyo, naomba Msomi Mwalimu Mheshimiwa Dkt. Mpango simamia sehemu uliyopewa na wananchi lakini na Mungu amekupa hiyo nafasi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kipaumbele kama Taifa. Katika kipaumbele cha kwanza ambacho nimekisoma kwenye kitabu cha Mheshimiwa Dkt. Mpango amezungumzia suala la kilimo na viwanda. Kinachonishangaza asilimia 40 ya mapato na mgao umeenda kwenye nishati na ujenzi. Kipaumbele ni kilimo ambacho kina asilimia zaidi ya 70 ya Watanzania hawana pembejeo za kutosha, masoko ya mazao yao hata wakilima na *network* ya hiyo *East Africa* tunayoizungumzia ya kupeleka bidhaa. Matokeo yake Wakenya wamewekeza maparachichi kule kwetu Rungwe na Mbeya wanalima na wanapeleka kwao wanafanya *packing* wanaenda kuuza nchi za nje Sweden na sehemu mbalimbali, wakati wananchi wetu sisi wa Tukuyu wanaendelea kuuza kwa bei rahisi maparachichi hayo. Ukipisema kipaumbele chako ni kilimo au viwanda tunategemea bajeti uliyopanga asilimia hiyo 40 ungeiwekeza huko ili iweze kuwa na tija na manufaa kwenye Taiga letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi bado nashangaa Mafisa Ugani katika kilimo ni wachache. Kwa mwaka wa nne sasa ajira hazijakuwepo kupata Maafisa Ugani wa kutosha katika kilimo. Masoko kama nilivyo sema, tunatumia *SIDO* wakati mwengine wanajitahidi kutangaza masoko madogo lakini haya masoko ni watu gani wanapata taarifa kwa wakati? Tumesaini mikataba mbalimbali, biashara kwenda *AGOA*, watu wetu wanazo hizo taarifa? Tunahitaji kubadili na hasa kuhakikisha wakulima wanatendewa haki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbegu zinazouzwa sasa hivi ziko chini ya kiwango. Je, watafiti tulionao, tuna Chuo cha Uyole, *SUA*, Serikali imepeleka kiasi gani cha pesa ili wawewe kufanya utafiti na kuweza kuwasaidia hawa wakulima kutoa mazao bora na yenye tija katika soko la kidunia? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Chuo cha Uyole hakijapata pesa za maendeleo kwa muda mrefu sana na huwezi kuendelea bila kuwekeza kwa watafiti au kwa hawa wataalam. Tuna mazao ya ng'ombe wale wanaozalisha mitamba, vifaa vyatia kutosha hawana *then unafikiria unaweza ukashindana na nchi kama ya Kenya ambayo leo hii wametuacha kwa mbali sana katika bajeti yao.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweka tozo nyingi sana ambazo naziita tozo za kuudhi. Mheshimiwa Mbunge mmoja alizungumza jana juu ya peremende na *sausage* na vitu kama hivyo, wenzenetu Wakenya wametazama matumizi ya simu, Wakenya wengi wanatumia simu za mkononi wameona ni bora kutoka asilimia 10 ya tozo waliiyokuwa wanadai wamepeleka asilimia 12 angalau zile asilimia 2 pesa inayopatikana iende kwenye afya. Hizo ndiyo akili za kufanya kwa sababu kutokuwa na simu hutakufa, kwa hiyo, kama unataka kuwa na matumizi ya simu basi simu yako utakapotumia pesa inayopatikana ikasaidie afya na hasa mama na mtoto katika Taifa lao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hicho hicho kilimo, pesa za maendeleo bajeti iliyopita shilingi bilioni 98 zilitengwa na Bunge lilipitisha lakini ni kiasi kidogo sana cha shilingi bilioni 41 zilikwenda. Sasa unawezaje kufanya maendeleo wakati pesa ambayo umelitenga haijafika kwa wakati na kuweza kufanya kazi iliyokusudiwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha pili tumesema ni ukuaji wa uchumi wa Mtanzania. Mtanzania huyo atakuwaje kiuchumi wakati wanafunzi hawapati kwa wakati mikopo, tunatengeneza vijana wa aina gani na ni uchumi gani tunauzungumzia? Tumesema vijana wanaosoma masomo ya sayansi na hasa wanawake kwa mfano Udaktari wapate mikopo asilimia 100 lakini kuna wasichana wengi wanarudishwa hawajaweza kupata mikopo na hawana uwezo wa kulipa ada, tunatengeneza uchumi wa aina gani? Unapozungumzia kukua kwa uchumi wa mwananchi mmoja mmoja ni pamoja na kujali na kuwa

na *dialogue* na hao watu kuweza kuijendeleza ni jinsi gani tunaweza kupeleka Taifa mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vitambulisho vya Taifa vilizungumziwa wapi, sisi kama Wabunge haikuletwa humu Bungeni, ni uchumi gani ambao mnauzungumzia? Bado tunahitaji Watanzania waweze kuendelea kiuchumi. Baada ya miaka minne ndiyo mnakumbuka kukaa na wafanyabiashara na hii ni kwa sababu hampendi kusikiliza mawazo mbadala mngechukua hatua mapema haya matatizo yasingetukuta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni la Taifa. Mwaka jana nilichangia hapa nikasema Deni la Taifa limekuwa ni tatizo, naogopa kusema kansa nitaambiwa nifute, limekuwa ni tatizo. Leo hii limefikia shilingi triliioni 51 kutoka shilingi triliioni 49, hii ni hatari. Kibaya zaidi katika kulipa deni hili bado tunaweza kushindwa kulilipa kwa wakati na mwisho wa siku watoto wetu watapata shida sana kulipa haya madeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitoa wazo kuhusiana na Deni la Taifa kabla Serikali haijakopa ilete humu ndani sisi kama Wabunge tuone umuhimu wa hilo deni kama linatakiwa kukopwa tupitishe kwa pamoja maana sisi ni wawakilishi wa wananchi. Nadhani ni vyema tukaliangalia hili deni la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuja kwenye tauzo za kike, wewe na mimi kama mama tunaowatetea wasichana na wanawake, leo hii unasema kwamba tumerudisha kodi kwa sababu wafanyabiashara walishindwa, mimi sioni kama Serikali imesimama katika nafasi yake maana ni Serikali ilitakiwa kuwasimamia hawa watu kusambaza au kushusha bei. Leo hii mazao ya Coca-Cola, Pepsi yanauzwa bei moja kwa sababu kuna bei elekezi, Serikali ilishindwa nini kuweka bei elekezi kwenye tauzo hizi za kike? Mwisho wa siku kwenda hedhi ni suala la kibailojia na mimi sikupanga kwenda hedhi, ni kitu nimezaliwa nimekikuta, kwa hiyo, tuisiwahukumu wanawake na mabinti zetu kwa sababu ya

hali yao ambayo Mungu amewapa. Naomba Serikali itakaporudi ijaribu kufikiria hili suala na waweze kulibadilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nina...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono bajeti yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzani, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa lakini niliwaambia unajua inabidi utafute maneno mengine lakini kikanuni ukiunga mkono hoja huwa ni moja tu na ndiyo inayoungwa mkono. Nawakumbusha tu Kanuni zinavyosema siyo jambo baya kuunga mkono. Hoja ni moja tu kama unakubaliana na maoni sema maneno hayo kwamba unakubaliana na maoni, ukiunga mkono ni hoja ya Serikali ambayo ni jambo jema Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kuunga mkono hoja ya Serikali. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel atafuatiwa na Mheshimiwa Gerson Lwenge, Mheshimiwa Dkt. Tisekwa Bunga ajiandae.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kusema kwamba mpaka 2100 yaani miaka 81 kutoka sasa Tanzania inakadiriwa kuwa ni nchi ya sita kwa idadi ya watu duniani lakini itakuwa ni nchi ya pili kwa Afrika ikiongozwa na Nigeria, tukifatiwa na DRC, Ethiopia na Uganda. Kwa hiyo, mambo yote ambayo tunayafanya leo na mipango ambayo tunaipanga leo ni kujipanga kwa ajili ya kupokea hiyo idadi ya watu na changamoto kwa ajili ya hiyo idadi ya watu.

Kwa muda mrefu tulikuwa tukitamani Serikali inayofikiri miaka 100 mbele siyo inafikiri kwa miaka mitano. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali kubwa linaloendelea hapa ni kwamba Serikali hii imekuwa akipanga bajeti kwa ajili ya vitu na sio kwa ajili ya watu. Nianze kwa Wilaya ya Siha, nikija kwenye eneo la barabara, Serikali hii imepeleka shilingi bilioni 52 na barabara ya lami inaendelea kujengwa ndani ya Wilaya ya Siha. Ukienda kwenye *TARURA*, barabara za kuunganisha vijiji kuna kata moja ya Ivaeni pamoja na Kashashi ilikuwa ili watu waliofautiana mita 200 kukutana wanazunguka kilometra saba. Serikali hii imepeleka shilingi milioni 960 na sasa wananchi wanaungana kwa kupitia daraja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni nini? Leo utakuta Mbunge anasimama hapa anasema kwamba Serikali hii inapeleka fedha kwenye vitu hapo hapo analalamika kwamba bei ya petroli imepanda kijijini kwa sababu barabara imekatika, unashindwa kuelewa huyu kiongozi anataka nini kifanyike. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye Wilaya ya Siha, Serikali hii na bajeti hii, Wilaya ya Siha ina vijiji 100 umeme umefika vijiji vyote, ina vitongoji 168 umeme umefika vijiji 125 bado vitongoji 43, ni Serikali hii hii ya Chama cha Mapinduzi. Hii maana yake ni nini? Ukipeleka umeme vijijini wananchi wataongezeka mazao yao thamani na watapata karibu huduma zinazohitaji umeme na hata mzunguko wa fedha unaongezeka kwenye vijiji vyao. Hiyo ndio maana yake, tunaposema tunawekeza kwenye umeme mfano *Stigler's Gorge* tunapandisha thamani ya maisha kule vijijini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata leo ukiangalia Korea ya Kusini na Korea ya Kaskazini, Korea ya Kusini ni tajiri kuliko Korea ya Kaskazini hata kama unapita usiku utaiona Korea ya Kaskazini kuna giza lakini utaiona Korea ya kusini kuna mwanga wa kutosha. Maana yake umeme ndiyo chanzo kikubwa sana cha kusimua maendeleo ya wananchi. Kwa

maana hiyo, tunaposema tunawekeza kwenye umeme wa uhakika na kwa sababu umeme wa maji ndiyo wa bei rahisi mpaka sasa hakuna mwingine, dunia sasa hivi inafanya utafiti namna ya kuwekeza kwenye umeme huu wa *uranium* na kuweka ndani ya bahari ambapo ni salama zaidi na utatoa umeme rahisi na sisi wangetufikirisha pamoja na sisi kuwekeza kwenye huu umeme wa maji sasa tuanze kufikiria na kujifunza wenzetu wanafanya nini kwenye *uranium*, hilo ndilo tungelitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye afya kwenye Wilaya ya Siha. Bajeti hii na Serikali hii imepeleka shilingi bilioni 9 Hospitali ya Kibong'oto na shilingi bilioni 1.75 tunajenga Hospitali ya Wilaya. Maana yake ukipunguza magonjwa, huduma ya akina mama na watoto na *life span* inaongezeka, hiyo ni michango ya kugusa maendeleo ya watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unakwenda kwenye maji, kwenye kata zingine imepelekwa shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya vijiji 17 na shilingi bilioni 1.75 kwa ajili ya vijiji 13. Maana yake ukipeleka maji vijijini unapunguza magonjwa lakini akina mama muda wa kwenda kuchota maji unapungua. Baada ya muda hata muda wa kufanya kazi za maendeleo unaongezeka lakini magonjwa ambukizi yanapungua na unaongeza maisha ya watu na uzalishaji. Kwa hiyo, hoja ya kusema hii bajeti ni ya vitu siyo ya watu ni uongo uliotukuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye umwagiliaji sisi kwetu tuna shilingi milioni 380 kwenye Kata ya Levishi na shilingi milioni 450 kwenye Kata ya Kashashi. Maana yake ni kwamba wananchi wanaenda kumwagilia mazao yao kwa kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, maana yake ni bajeti ya watu na inayoenda kukugusa maisha ya watu siyo bajeti ya vitu kama ambavyo wenzetu wanataka kutuaminisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo wenzetu walewale leo wanasema kwamba idadi ya watalii kwenye Taifa hili haiongezeki na wanasema pato la utalii haliongezeki. Watu wamefanya utafiti wameona kwamba

wenzetu ambao tunashindana nao kwenye utalii wana ndege na wanasafirisha watalii kwa ndege zao wanaanza kupidisha kwenye nchi zao ndiyo watalii waweze kuja Tanzania. Maana yake sisi Watanzania pesa ya kwanza wanayotoka nayo Ulaya wanapita nazo kwanza kwenye nchi yetu chenchi ndiyo inafika kwenye nchi yetu. Sasa leo tumenunua ndege anaibuka yule yule anayesema kwamba pato na idadi ya watalii haiongezeki anasema kwamba unanunua ndege haigusi maisha ya watu. Haya ndiyo mambo tunayoyasema. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia suala la ajira, tunatakiwa tufikiri sana na tunawekeza kwenye elimu, tunaenda kwenye dunia ya *artificial intelligence*, vitakuja viwanda hapa mtu atakuja na roboti tatu halafu anahitaji watu wenge uwezo wa kufikiri. Ndiyo maana Mheshimiwa Profesa Ndalichako kuna hela nyingi zimewekezwa kwenye elimu na mabweni yanajengwa kwenye maeneo mbalimbali, uwekezaji unafanyika kwenye elimu ili tufike hapo kwa sababu ajira ijayo ndugu zangu siyo hii mnayoipigania hapa ambayo leo inagharimu asilimia 43 ya pato la *TRA*, ni ajira ambayo inahitaji mtu kufikiri siyo kufanya *casual job*. Miaka ijayo *artificial intelligence*, roboti ndiyo zitakuwa zinafanya kazi sasa wanatakiwa watu *creative na innovative*. Twendeni tukatengeneze watu *creative na innovative* kwa sababu ndiyo ajira itakayokuwepo siyo aina hii ya ajira ambayo tunaifikiria sasa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina malalamiko kutoka kwa wenzangu wazuri wa CHADEMA wameniambia jambo niombe kuwasaidia na Watanzania wazuri. Wameniambia kwamba kuna kiongozi wao mmoja mkubwa amekopa ndani ya chama shilingi milioni 600 akaenda kuwekeza Morogoro lakini huo mradi ulivyoshindikana anataka sasa kugeuka hiyo pesa iwe ulikuwa ni mradi wa CHADEMA usiwe tena mradi wa kwake yeye binafsi. Wakaniambia nisaidie hapa kuiokoa hiyo mali ya CHADEMA na tuiombe TAKUKURU iende pale na hata ikiwezekana kwa sababu tunataka maendeleo yanayogusa watu basi hayo matrekta ambayo yanabadilishwa majina na hizo mali kwa sababu hizo pesa

ni ruzuku na ni kodi ambayo Mheshimiwa Dkt. Mpango umekusanya, sasa hiyo kodi ambayo Mheshimiwa Dkt. Mpango umekusanya ikaenda CHADEMA halafu mtu mmoja amechukua anataka kuwapakazia CHADEMA baada ya yeye kukopa tunataka ikachunguzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mashamba ya ushirika kule Siha na Hai tunataka sasa yale matrekta yachukuliwe yaende kwenye hayo mashamba na ichunguzwe tuletewe ukweli hapa. Wakati kule Hai tunaendelea kuchunguza, Sabaya anaendelea kuchunguza kale kataasisi cha kihuni, tuendelee kufanya na hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu anapenda kusema kansa hapa. Kansa maana yake ni nini? *Cell* zote za mwili zinakuwa *controlled* na *central nervous system*. Maana yake *cell* moja iki-jump ikawa haisikiliza ubongo inakuwa inajigawanya bila kusikiliza ubongo unataka nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Serikali ya Tanzania na Chama cha Mapinduzi kuna *control system* kutoka juu mpaka chini na akisema Mheshimiwa Rais basi chini tunafuata lakini CHADEMA sasa hivi wanatafutana wamekuwa kansa wenyewe, kila mmoja yuko kivyake kama *cell* ya kansa. Kwa hiyo, kufafanua vizuri kansa ni CHADEMA wala siyo kama yeye anavyofikiri ni Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namsikia Kiongozi Mkuu, namheshimu sana kaka yangu Mheshimiwa Selasini lakini naunga bajeti mkono, hebu rekebisha kansa kwenye chama chako watu wasikilize kama *central nervous system*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, basi kusema namsikia kiongozi namheshimu sana Mheshimiwa Selasini, lakini naunga bajeti mkono hebu rekebisha kansa kwenye chama chako watu wasikilize kama sisi tulivyoosikiliza. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamuita

Mheshimiwa Eng. Gerson Lwenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare ajiandae.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara ya Fedha kwa kutuletea hotuba nzuri ya bajeti na ameanza kwa kutoa *quotation* nzuri kwenye Biblia, kawabariki watu ambao wanamuombea. Basi naomba niongeze tu kwa sisi Waheshimiwa Wabunge, tunatakiwa tuwe wamoja, umoja huu ndiyo unatufanya tuweze kusonga mbele na Mwalimu wetu Julius Nyerere aliwahi kusema kwamba umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna mambo mengi makubwa ambayo Serikali ya Awamu ya Tano imeyafanya. Ninukuu mambo saba, yapo mambo mengi, tukitaka kuyataja yote katika miaka mitatu tutakesha hapa kuonesha kwamba kwa kweli wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kutoa elimu bure, kila mwezi bilioni 23 zinapelekwa kwenye shule zetu kwa ajili ya elimu bure, ni kitu kikubwa sana. Kununua ndege nane kwa mara moja na kufufua Shirika la ATCL, kupeleka umeme katika vijiji 7,000 katika mpango wa REA, kuanza ujenzi wa SGR Dar es Salaam – Morogoro, kilomita 722 ni Jambo kubwa. Kuhamia Dodoma na kujenga mji wa Serikali, Wizara zote zimejengwa katika muda mfupi zimejengwa ofisi za Serikali na kujenga vituo 352 vya afya na hospitali 67 katika muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndugu zangu kama mtu huwezi kuzungumzia haya na kupongeza Serikali ya Awamu ya Tano, ukajisita katika vitu vidogovidogo ambavyo ni kweli vinahitajika lakini haya makubwa ambayo yameanza ni lazima tuunge mkono. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiri pamoja na haya ambayo nimeyasema na Serikali hii imeonesha

kuthubutu, ninaomba sana ithubutu katika miradi mitatu; kwanza mradi wa Liganga na Mchuchuma, hapa panahitaji maamuzi magumu ya kuthubutu, hatuwezi kuwa na uchumi wa viwanda bila kuwa na chuma, chuma ndiyo nguzo muhimu katika viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni lazima Serikali ithubutu kuanzisha mradi huu wa Liganga na Mchuchuma, kama kuna majadiliano basi yasiwe yanachukua miaka kumi bado mnajadiliana. Kama kitu hakiwezekani basi tunajua hakiwezekani tunatafuta mbadala mtu mwengine tukaweza kujadiliana nae ili huu mradi wa Liganga na Mchuchuma uweze kuanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi mwengine ambao nilliona ni muhimu na upo kwenye mpango wa miaka mitano ni ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Ndugu zangu Bwawa la Kidunda lisipojengwa, Dar es salaam muda si mrefu itakuwa haina maji. Kwa hiyo, tunahitaji sana tujenge Bwawa la Kidunda ili tuwe na maji endelevu katika Mji wa Dar es salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, nilikuwa naomba Bwawa la Farkwa kwa ajili ya Mji wa Dodoma, ni mradi muhimu sana ambao tunahitaji Serikali hii ithubutu tuweze kujenga Bwawa la Farkwa. Sasa ili tuweze kufanya mambo haya tunahitaji kupanua wigo wa makusanyo yetu ya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nashauri kwenye kodi ya majengo, miundombinu ambayo ilitengenezwa na halmashauri zetu, wanaweza wakakusanya kirahisi zaidi kuliko *TRA*. Hii kodi ya shilingi 10,000 kila nyumba ni rahisi sana zikakusanywa na halmashauri zetu. Kuwe na mfumo tu kwamba zile fedha akikusanya ziingie kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, naona jambo hili kidogo Mheshimiwa Mpango mnasita kulifanya lakini litatusaidia, tutapata fedha nyingi katika kodi ya majengo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *service levy* kwa mfano kwenye hoteli na *guest house*, kutoza asilimia 10 kwenye mauzo, naflkiri hii siyo sawasawa. Na nadhani hata kama mtu unafanya biashara 10% kupata faida ni ngumu sana lakini fedha ile yote inachukuliwa na manispaa yetu na halmashauri. Kwa hiyo, naomba hili jambo mliangalie ili kusudi kwa kweli watu waweze kuwekeza kwenye eneo hili la huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni hivi vitambulisho vya wajasihamali ambavyo vinatozwa kwa elfu 20 lakini utekelezaji wake unatofautiana kati ya mkoa na mkoa, naomba jambo lihuishwe na pia iainishwe ni aina gani ya biashara za hao watu watakaokuwa na vitambulisho. Mama ntilie anapika supu naye anatakiwa aliye elfu 20 kwa mwaka, ni fedha kubwa sana. Mama amepanga nyanya anauza kwa siku hata 1,000 hapati, na yeye aweze kuwa na kitambulisho cha elfu 20, nafikiri siyo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tungetengeneza *category* kama tatu kama mtu anafanya mauzo kwa mwaka yasiyozidi 500,000 hii asihitajike kuwa na kitambulisho. Yule mtu ambaye ana 500,000 – 1,000,000 angalau tumpe kitambulisho cha 10,000, tutapata mapato mengi sana. Halafu wale wanaozidi sasa 1,000,000 – 4,000,000 ndiyo tuweke 20,000. Nina hakika kabisa tukiweka mageuzi haya tutapata mapato ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Wanging'ombe pia ina nafasi ya kuweza kuchangia kuweza kupata mapato. Tunalo eneo ambalo ukifika pale Wanging'ombe kuna jiwe ambalo kuna ramani ya Afrika, yaani Mwenyezi Mungu aliweka ramani pale, ukienda pale unapata ramani ya Afrika. Sasa hili tunaweza tukapata, tukiboresha barabara inayotoka Njombe mpaka Iyai tukaweka lami, watalii watakwendwa kuangalia hii ramani ya Afrika ambayo Mwenyezi Mungu alikwenda kuiweka kwenye Wilaya yetu katika Kijiji cha Igodiba, tutapata mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Msitu wa Asili wa Nyumbanitu ambao unapita barabara hiyo hiyo, kuna kuku weusi ambao pengine huwezi kuwapata maeneo mengine duniani utawapata Wanging'ombe. Sasa tutaongeza mapato kwa sababu watalii watakwenda wataangalia wale kuku wa ajabu wapo kwenye Msitu wa Wanging'ombe, karibuni sana muweze kufika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mwekezaji ambaye anataka kuwekeza kuchakata matunda ya parachichi katika Wilaya ya Wanging'ombe toka mwaka jana mwezi wa 8 anazungushwa kuweza kupata leseni na makontena na kila kitu kipo bandarini. Ilikuwa mpaka mwezi wa nne kile kiwanda kiwe kimeshaanza kufanya kazi. Kwa hiyo, naomba sana urasimu upunguzwe katika hizi taasisi mbalimbali zinazohusiana na *process* ya wawekezaji kuweza kuanza kupata vibali vya kujenga viwanda ambavyo vitatusaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia sana suala la kukuza kilimo na kuomba bajeti iongezwe lakini ni vizuri tukaangalia tunaongeza bajeti kwenye eneo gani. Kuna wengi wamesema vizuri sana kwamba lazima tuweke nguvu sana katika mbegu na mbolea pamoja na viuatilifu, hapa ndio tungeongeza bajeti na tuondoe vikwazo vile vya kuanzisha hizo biashara za kusambaza mambo ya mbegu bora na viuatilifu pamoja na mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiondoa vikwazo nina hakika sana kilimo kitapanda juu na pia tuangalie mazao yale ambayo yanaendana pamoja na viwanda vile tunavyovianzisha. Kwa hiyo, hili jambo ni muhimu sana tuweze kuunganisha ili kusudi ndugu zangu kilimo kikue lakini pia na viwanda viweze kuanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo pia tulifanyie nguvu sana ni katika suala la kutafuta masoko ya wakulima. Wakulima wetu wamekuwa wanahangaika sana kwa kuweza kupata masoko ya mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nichangie machache, naunga mkono hoja hii, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Shukrani sana. Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga atafuatiwa na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Pauline Gekul ajiandae.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika bajeti yetu hii. Kwanza kabisa niungane na Waheshimiwa Wabunge wote walotangulia kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wake na timu nzima ya Wizara hii ya Fedha kwa kazi nzuri wanayoifanya hasa katika kutatua changamoto zinazohusu makundi mbalimbali, wafanyabiashara wakubwa na wadogo lakini na makundi ya wakulima kwa kutoa tozo mbalimbali ambazo zilikuwa ni kero kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutowana na suala la muda, napenda nijielekeze hasa katika mambo mawili; kwanza nijikite katika idara yangu ya vyuo vikuu lakini baadaye nitajikita kwenye bajeti kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa wetu Rais mpPENDWA Dkt. John Pombe Magufuli katika kushughulikia masuala ya chuo kikuu hasa katika utoaji wa mikopo ambao mwaka hadi mwaka bajeti yake inazidi kupanda. Kwa mfano, mwaka jana takribani wanafunzi 123,000 walipata mikopo na bajeti hii ya 2019/2020 takribani wanafunzi 128,000 wataendelea kupata mikopo takribani bilioni 450, tunapongeza sana Serikali yetu kwa juhudhi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, kwa nia njema kabisa mikopo hii inalenga katika kuhakikisha makundi yote ya watoto wa Tanzania wakiwemo wakulima, wafanyakazi lakini hasa wale wa kipato cha chini wanaweza kushiriki katika kutengeneza wataalam mbalimbali katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ombi langu moja kwa Mheshimiwa Waziri, mikopo hii pamoja na uzuri wake lakini kuna changamoto ambazo zimejitokeza hasa ukiangalia sasa jinsi ilivyoboreshwa kweli mwanzo watu walisucasua lakini baadaye wakatafuta namna ya ulipaji wa mkopo. Mkopo huu unatakiwa mwanafunzi anapomaliza chuo alipe baada ya miezi 24 lakini alipe kwa asilimia 15 lakini pamoja na hiyo kuna hiki kipengele cha *Value Retention Fund*. Sasa kwa kufuata vigezo hivi, inafanya huu mkopo sasa badala ya kumsaidia huyu mtoto wa maskini imekuwa sasa ni mzigo mkubwa sana hasa kwa sababu ya hii *Value Retention Fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kijana ambaye amemaliza chuo kikuu mwaka 2015, kama utatoa hii miezi 24 maana yake unahesabu 2016 na 2017, yupo kwenye *grace period*, ina maana unahesabu 2018 na hii 2019 kidogo. Kijana huyu juzi wakati anakwenda kuangalia anadaiwa shilingi ngapi, kwa sababu ya hii *Value Retention Fund*; huyu kijana alikopeshwa milioni 10 lakini alivyokwenda kucheki juzi amekuta anadaiwa milioni 16.5. Sasa je huu mkopo kweli nia yake ile njema imetolewa sasa imekuwa kama ni *business* ambayo kwa kweli itaathiri kwa kiasi kikubwa sekta hii ya chuo kikuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri aliangularie hili suala kuweza kurekebisha kama vile tulivyofanya ile *quick appraisal* kwenye tozo ya kodi ya pedi. Kwa hiyo, hivi nayo sasa wafanye *evaluation* kwamba huu ulipaji kwa kweli utamsaidia mtoto wa mtanzania au viperi. Kwa hiyo, hilo ni ombi langu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na asilimia 15 naomba tena nirudie bado ni kubwa mno. Hii sasa *implication* yake itakuwa kwamba wanafunzi sasa wameshaanza kuambizana *burden* ya huu mkopo, matokeo yake itafika mahali wakati ule Pride, Finca walitoza kodi kubwa sasa hivi zimepotea baada ya watu kutafuta vyanzo vingine. Kwa hiyo, tunaweza tukakosa hata wanafunzi wa kuchukua mikopo au kozi zile ambazo zinahitaji kusomewa muda mrefu hasa za sayansi, zitaathirika

vibaya wanafunzi hawataenda kusoma kule kwa sababu ya huu mzigo ambao umeongezwa na hii *Value Retention Fund*. Kwa hiyo, naomba sana tuangalie hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja hayo, ninaomba niseme kwamba hawa vijana alipe asilimia 15, mkopo ambao haumaliziki mpaka anazeeka, inaweza pia hata kichocheo kwa upande wa ujisadi na rushwa ambayo Mheshimiwa Rais wetu kila siku anapambana na ujisadi na rushwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, ninaomba kwamba Serikali itoe zile fedha ambazo zimeahidi katika kujenga hosteli. Juzi tumpoteza binti yetu wa kike ambaye alivamiwa na majambari wakati anakwenda. Kwa hiyo, hosteli zikijengwa ndani ya chuo, zikawa na ulinzi mkuu, itasaidia sana kupusha madhara kama haya tullyoyapata hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niingie sasa kwenye suala la sera mbalimbali katika nchi yetu katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Wengi tumeangalia suala la sera ya huduma bure, sasa huduma bure katika jamii kwa mfano naipongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kuwa sikiu kwa kuweza kuwasaida wanyonge katika kupata huduma mbalimbali. Kwa mfano, tayari tuna Sera ya Huduma Bure kwenye elimu bure, watoto, wajawazito na wazee wanatibiwa bure lakini hata kwa magonjwa ya kansa bure. Kwa hiyo, Serikali imajaribu kupunguza mzigo mkubwa kwa wazazi ili waweze kupeleka watoto wao shule. Pia kuna mpango mzuri wa *TASAF* ambao unasaidia watu maskini waweze kuwasaidia hasa kwa upande wa mtoto wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, sasa hivi kuna hii *debate* inayoendelea kuhusu taulo za kike. Ni wazo zuri sana lakini tuangalie je uwezo wa uchumi wetu, hivi tutaweza kweli kila kitu bure, tayari Serikali jamani imeshatoa mpango wa *TASAF*. Sasa *TASAF package* mojawapo ni kumsaidia hata huyu mtoto wa kike kupata taulo. Hata hivyo, tuangalie je,

kigezo cha kwamba mtoto anapokuwa kwenye mzunguko wake ule wa mwezi, je, tukitoa hii taulo bure tayari inaweza ika-solve problem?

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, nafikiri kipaumbele tungewekeza kwenye vyoo na maji. Huyu mtoto anaweza akapata taulo lakini kama shule haina choo, hawesi kwenda shule lakini shule kama hakuna maji hawesi pamoja na kwamba ana taulo atabaki nyumbani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndugu zangu, tukiangalia ukisoma kweli kuna nchi zimeweza ku-*implement* haya masuala ya taulo lakini wameangalia *the needy people* siyo *the whole population* watoto wa kike wote kama ilivyokuwa elimu bure hata mtu mwenye uwezo basi umlipie. Tuangalie ni familia zipe kweli hazijiwezi lakini tayari kuna mpango wa *TASAF* ambao umeshasaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri tujielekeze sasa kwenye masuala yale ya msingi, tuelekeze suala letu la vyoo, maji na afya kwa sababu huyu mtoto anaweza akawa kwenye mzunguko wa mwezi lakini anaumwa tumbo, atahitaji apate panadol na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tujielekeze kwenye masuala ya kimaendeleo, tuache hivi vitu bure bure kwa sababu ukiangalia sana, dunia ya leo kuna watu watapitia kwenye mgongo wa demokrasia, usawa wa jinsia na harakati za binadamu kutengeneza maslahi yao binafsi. Uchumi wa nchi yetu bado ni wa chini hatujafikia hata uchumi wa katii, hatuwezi kila siku tunatoa kitu burebure, je, nafasi ya mzazi naye katika kuchangia familia yake ni nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sababu zinazofanya Afrika ziwe maskini mojawapo ni uvivu pamoja na *poor policies*. *Poor policies* maana yake siyo kwamba ni *policy* mbaya lakini una-*implement* sera ambayo siyo wakati muafaka kwa wakati huo. *It's not a bad policy* lakini *it's a poor policy*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano sasa hivi unasema kila kitu bure, Waheshimiwa Wabunge ninyi ni mashahidi kila siku mnasema bajeti haitimii, hakuna bajeti hata siku moja ikafika asilimia 100, leo unataka uongezee tena Serikali eti ikatoe tena pedi bure kwa watoto wa kike, fedha zitatoka wapi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri kwa Serikali katika kusaidia mpango wa TASAF, katika kusaidia elimu bure, mzazi naye aendelee kuchangia katika kumlea huyu mtoto ili sasa tujielekeze kwenye mipango hii ya maendeleo. Mwanamke anahitaji maji na afya ili tuweze kutekeleza mipango hii ya maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme ukweli pamoja na nia nje, lakini hatujafikia bado wakati muafaka wa kufanya kila kitu burebure, hii sasa ni kuingizana mkenge ili kesho na keshokutwa waje tena watugeuzie kibao ooh mlipanga hivi; nasema hizi zote ni *political pressures*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Uganda waliibeba hii ajenda ya pedi bure, ukiangalia Kenya, *South Africa* kwa nini zote zitokee kwa wakati mmoja; tunajua *strategies* hizi za watu. Wanajua sasa hivi tuna wataalam, tutawekeza, tutafanya maendeleo wanaturudisha nyuma, wewe kila kitu utoe bure ile hela haizalishi maana yake nini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo niliamua nijikite hapo, nashukuru sana kunipa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe ajiandae.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Kwanza nipongeze hotuba ya Kambi ya Upinzani iliyotolewa hapa na nishauri Serikali chini ya Mawaziri wake wote wawili na washauri wao ni vyema wakachukua

ushauri ambao umetolewa na Kambi ya Upinzani kwa manufaa ya bajeti nzuri kwa ajili ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili; Waheshimiwa nizungumze kauli ambayo nimewahi kuitoa hata tangu nikiwa kiongozi wa Kambi ya Upinzani huko nyuma na sasa nairudia kwamba vipindi mfululizo ambavyo tumekuwa ndani ya Bunge hili na mpaka leo hii sijawahi kuona upande wa pili ukisema hii bajeti ni mbaya na kwamba siyo bajeti ya wanyonge, bajeti zote tunaambiwa ni bajeti za wanyonge pamoja na kwamba zinakua kwa kiasi mwaka baada ya mwaka lakini matatizo yanabaki vilevile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu mimi nakwenda mbele zaidi ya kuhoji *capacity* ya wataalam wetu na watu wanaotutengenezea bajeti hizi, kwamba nashauri *Researchers* wetu, wataalam wetu, taasisi zinazojenga *capacity* na hata taasisi zinazosaidia *capacity building* ya sisi Wabunge, wajaribu kuangalia tatizo letu la msingi liko wapi; kwa nini tunatengeneza bajeti ambazo miaka nenda, miaka rudi hazioneshi *effectiveness* kwa kuondoa umaskini ule unaolengwa wa kipato kwa watu wetu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna masikio, tuna macho, tuna mikono, tunasafiri na leo nilikuwa naangalia kwenye *ma-group*, naangalia watu waliokwenda *Egypt* wanatuonesha mahali walipo, wanakopita. Kwangu mimi kinachokuja ni kwamba mambo yote tunayoyaona kwenye runinga au ukienda kwenda *geographical* ile *TV* ukaona mambo watu wanayofanya, ile ni *brain*, *brain* ndiyo inayofanya mambo yote hayo. Sasa na mimi najiuliza, *brain* ya sisi Watanzania na wataalam wetu ikoje? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli Mheshimiwa Dkt. Mpango, Naibu Waziri, Mawaziri wetu, Wabunge; huko tunakotoka vijijini tunapozungumzia suala la umaskini wa watu wetu, kweli tunahitaji Wazungu ndio waje watuneshe umaskini wa watu wetu? Hivi mtu atoke hapa aende kilometra 20 tu kutoka ndani ya Dodoma, aone kama hajui

umaskini unafananaje, aende aone; hivi tunaridhika na hizi bajeti tunazotengeza kwamba kweli zinajielekeza kubadili hali ya watu wetu? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kabisa, kuna nchi ambazo *early 50s* kuja mpaka *90s*, Nchi kama Indonesia, Malaysia, *Philippines*, Thailand, Vietnam na sasa Botswana, hata Rwanda hapa jirani ambaa tulikuwa tunalingana na wengine wako nyuma ya uchumi wetu wakati tunapata uhuru, wamefanya maajabu gani mbona wana vichwa kama vyetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mbona akina Mheshimiwa Dkt. Mpango ndio wanakwenda katika nchi kule, tena Watanzania wanasifika sana wakienda kwenye mitihani au kuandika *thesis* wanapata A nyingi, lakini inapokuja kwenye kutafsiri elimu wanayoipata kuja kwenye matendo tunapotelea wapi, mbona mambo hayabadilki? Naomba hilo tujielekeze tuangalie matatizo yetu kimsingi yako wapi. Tulete *Researchers* wajaribu kutafiti vichwa vyetu vinaharibikiwa wapi, kutuhamisha akili tulizonazo kwenda kwenye vitendo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili, naomba Mheshimiwa Dkt. Mpango wakati tukieleka Jumanne kupiga kura, nataka aniridhishe na kitu kimoja ambacho hapa katikati kinaweza kunipa ushauri wa kupiga kura; aniridhishe kwamba bajeti hii inakwenda kufanya maajabu gani, anakwenda kufanya maajabu gani tofauti na *experience* ambayo tumeipata katika bajeti hii inayokwenda kumalizika mwisho wa mwezi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa na maana gani; kwamba bajeti iliyopita kwa mapato ya kodi kwamba tuliambiwa kwamba kila mwezi wanapata *average* ya 1.2 pamoja ni nje ya trilioni 17 ambazo Mheshimiwa Rais alikuwa anazzungumzia. Sasa ukija kwenye *average* tumekuwa tunaelezwa wanajaribu kupata 1.2 *trillion* kila mwezi. Kwa bajeti hii inaonekana lazima tutakwenda katika *average* ya

kutaka kukusanya *at least 1.4 – 5 trillion* kwa kila mwezi kama tutakuwa tumekwenda vizuri, ili tupate ile 19 ya mapato ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa *experience* ilioonekana hapa kupata hata hiyo 1.2 ni kwamba Mheshimiwa Dkt. Mpango na wasaidizi wake na *TRA* na taasisi nyingine wametumia mitulinga isiyo ya kawaida. Maana yake wame-*pull forces* zote kadri walivyoweza; maana yake pale polisi wameshiriki, mgambo wameshiriki, *TISS* imeshiriki, wajasiriamali nao na vitambulisho wameshiriki, yaani kuna watu wengine hata mpaka wakawekwa ndani na wengine wakawekewa hata kesi za *money laundering*, yaani hata kwa *forces* zote hizo lakini amepata *average* ya 1.2 *trillion*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakati tukielekea tena kwenye hii bajeti naiita bajeti ya uchaguzi, yaani kupata 1.5 *trillion*, kama kule alikuwa anatumia viboko nafikiri safari hii atatumia rungu au inabidi atumie *SMG* kabisa mtaani na vinginevyo mimi naitafsiri kwamba inaweza ikawa bajeti ya mateso na maumivu kwa wananchi wetu na wafanyabiashara. Maana yake tusidanganyane; wananchi watarajie hilo. Vinginevyo kama ni tofauti napo anieleze anakwenda kufanya maajabu gani ili kuwaepusha watu na mambo ambayo mimi nayaota kwamba yatatokea. Kama wafanyabiashara walikuwa wanakimbizana na *TRA* sasa watahama hata nchi kabisa kwa sababu hali kusema kweli haivutii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ambalo nataka kumaliza nalo; mimi natoka *Bukoba Town* na kwa *Bukoba Town* na wananchi wa Kagera sisi meli, unapomwambia mwananchi wa Kagera meli wameijua tangu wakati wa Mkoloni, kumekuwepo na Mei *MV Victoria* ile ililetwa tangu wakati wa Mwingereza. Kwa hiyo kwa mwananchi wa Kagera meli ni maisha, meli ni uchumi. Kwa sababu leo mwananchi wa Kagera njia pekee ambayo anapata huduma na kuwa *supplied* na vitu mbalimbali ni

kutumia barabara. Ukitumia barabara tunajua *expenses* za ku-*transport* mizigo kwenda mpaka Kagera kwa njia ya barabara, kwamba ni *very expensive*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi naomba, tuliona bajeti iliyopita, kwenye upande wa huduma za meli ni kwamba zilikuwa zimetengwa *20 billion*, lakini zilizotoka mpaka mwezi wa Nne ni *only three billion*. Na mwaka huu nimeona zimetengwa *70 billion*. Sasa ile 20 ilishindikana na zikatolewa tatu kwa bajeti ya kutafuta kwa mitulinga, sasa hii ya sasa *70 billion* sijui zitapatikana wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nalizungumza kabisa. Bahati nzuri Mheshimiwa Dkt. Mpango ni Muha na Waha ni wajukuu zetu maana yake ile ya Wahaya babu zao, sisi tunaitwa Wahaya tulipoona mjukuu asilingane na babu tukaondoa ya ikabaki Waha. Hata Mheshimiwa *Engineer Nditiye* nafikiri anatoka kule na shemeji yangu, Naibu Waziri, sisi Bukoba tunataka meli. Kama meli mpya imeshindikana watupe Victoria yetu alioacha Mwingereza, hebu wajaribu kuikarabati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu meli sisi wakati inafanya kazi mfuko wa simenti ulikuwa 17,000, 16,000, lakini sasa hivi kwa barabara simenti 20,000. Sisi Kagera wamekuwa wepesi kutuambia sisi ni mkoa maskini sasa hivi. Ni lazima tutafute tuliharibikia wapi Kagera, Kagera ulikuwa ni mkoa ambao unasifika dunia nzima. Ule mkoa hata wakati tunapata uhuru Mwalimu Nyerere aliwekewa *guarantee* gari la kwanza kutoka kiwandani na *BCU* (*Chama cha Ushirika cha Kagera*). Kwa hiyo huu umaskini wa Kagera mimi nafikiri umetengenezwa tunahitaji *Marshall Plan* ya Kagera ili mkoa urudi katika nafasi yake, wasianze kutuambia ninyi ni watu wa matatizo, sijui mafuriko huko, matetemeko huko. Sasa turudi katika kuutengeneza huo mkoa ili urudi mahali pake. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa taarifa hapa kwamba wageni wa Mheshimiwa Bahati Ali Abeid wameingia, na hawa ni watoto wake wawili, Salama Mabruk na Jafari Abubakar na wanafunzi wenzao 25 wa Chuo cha Mipango. (*Makofî*)

Sijui wamekaa upande gani? Haya, naona pengine wameshatoka ama hawakupata fursa ya kuingia.

Mheshimiwa Pauline Gekul nilikuwa nimekuita, utafuatiwa na Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe, Mheshimiwa Timotheo Mnzava ajiandae.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa fursa nami nichangie katika Bajeti hii Kuu ya Serikali. Nimshukuru pia Mwenyezi Mungu, huyu Mungu ambaye anatupa pumzi ya uhai bila kuilipa VAT au chochote, ni kwa neema yake tu, namshukuru sana, anatufanya tutimize wajibu wetu tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze viongozi wetu kuanzia Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha, Mawaziri na watendaji wa Serikali kwa kuendelea kutumikia Taifa letu kwa upendo na moyo wa uzalendo. Hongereni sana, na sisi tunawaombea pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi hii bajeti, mimi binafsi nilivyoipokea nikawa najiuliza ni nani huyu anakwenda kuthubutu kuipinga bajeti hii? Nitatoa sababu za kutosha tu; kwa sababu naamini Wabunge tunawakilisha wananchi ambaeo wametutuma, tunaishauri Serikali lakini bajeti hii imekwenda kuonesha vitu vikubwa ambavyo havijawahi kufanyika. Nafikiri siku ya kura kama vile haifiki, tuone ni nani anasema hapana kwenye bajeti hii, na sababu ntazitoa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wachache wanasema hii bajeti ni ya vitu siyo ya watu, lakini vitu hivi wanavyovisema naomba nivitaje, ambavyo wao wanaona ni vibaya sana kwa Watanzania, vimeorodhesha ukurasa wa 19 kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri; ni ujenzi wa barabara ya njia nane kutoka Kimara, Dar es Salaam hadi Kibaha, kilometa 19. Wananchi wa Dar es Salaam walikuwa wanahangaika na foleni huko, wanapoteza muda, lakini hiki kwa wengine ni kitu kibaya, haigusi watu, sasa sijui ni watu wapi wanataka waguswe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vitu wanavyovisema vingine mfano ni ujenzi wa Daraja la Mto Kilombero. Natoa tu mfano, michele, mipunga ilikuwa inakwama inazamia kwenye ule mto lakini leo daraja limejengwa watu wanasema ni bajeti ya vitu. Bajeti hii ya vitu inayotajwa ni bajeti ambayo inakwenda kutatua tatizo la upungufu wa umeme katika nchi yetu lakini watu wanaona kwamba tunapeleka pesa nyingi huko, ni tatizo, ili viwanda vianze na huku chini wananchi wanufaikie na *energy* ambayo imekuwa ikiwa na upungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hao watu wanathubutu kubeza hata jithada za ununuzi wa ndege na vitu vingine. Ukioma watu wamekosa vitu vya kuongea utashangaa wanabaki sasa kuzungumzia mambo madogo madogo, mara wigii, wigii, wigii. Hata hivyo wananchi wetu waliotutuma, naamini wengi tunaowawakilisha huko vijiji hawavai haya mawigi ambayo tunayatetea, wengi wanahitaji maji, umeme na barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili, wanasema milioni 50 hazijatolewa. Nitoe mfano tu, mimi ni wa Babati hapo, ujenzi wa barabara hii kutoka Dodoma mpaka Babati, kilometa zaidi ya 260 ni milioni 50 ngapi kwa vijiji vingapi zimepelekwa kuititia barabara hii tu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa mradi wa maji tu, mfano kijiji change, juzi nimetoka kuzindua huo mradi tukiwa na mwenge pale...

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Taarifa.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** ...ujenzi wa mradi wa maji wa Imbilili wa milioni 600...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul, kuna taarifa; Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Napenda nimpe taarifa mzungumzaji kwamba wakati wa kampeni, wakati Chama cha Mapinduzi kinaomba ridhaa ya kuongoza, pamoja na milioni 50 walizoziahidi, waliahidi wataleta barabara, maji na kujenga reli. Kwa hiyo wasipotoshe kwa *ku-substitute* vitu wanavyojengea wananchi na milioni 50, wapeleke milioni 50 za wananchi. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikumbusha jana, nimekumbusha na leo; matumizi ya Kanuni ya 68(8), tuisome tunazo nakala, ni taarifa ya namna gani unayoweza kuitoa.

Nasisitiza tena; tuisome Kanuni ya 68(8) matakwa yake. Mheshimiwa Gekul, endelea na mchango wako.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, natolea mfano Kijiji kimoja tu cha Imbilili cha jimboni kwangu, milioni zaidi ya 600 wamepeleka pale mradi wa maji ambao walikuwa hawategemei katika maisha yao. Hata hivyo, kuna watu wanajificha milioni 50, labda sasa kuna tatizo la kihesabu, Walimu wa hesabu watusaidie, kati ya milioni 600 ambazo wamepelekewa wanakijiji wanakunywa maji na milioni 50 kipi kikubwa? Huo ni mfano tu, ndiyo maana nasema watu hapa tunachanganyana kwa sababu wamekosa vitu vya kuongea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine mtu anasimama kabisa Mbunge anasema bajeti imekuwa hajiaongezeka, ya Kenya imeongezeka; *so what?* Wakati huo huo mtu anasimama tusipotekeleza bajeti ile ya triliuni 32 anakwambia hii bajeti hewa. Hawa watu watatupotezea sana muda, Watanzania wanasubiri tupeleke maendeleo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niseme ni kwa nini yejote humu ndani hatakiwi kusema hapana kwenye bajeti hii. Baada ya kutoa utangulizi huo niende kwenye *details* za wananchi wetu vitu gani wameguswa, mfano wale wa majimbo ya mijini lakini kwa wananchi wa nchi hii wafanyakazi ni takribani kama milioni moja tu. Wananchi wa Tanzania wengi wao ni wafanyabiashara na wajasiriamali wadogo wadogo, kila mmoja anawakilisha hawa watu kwenye Bunge hilli. Unakataaje bajeti hii, la kwanza, Serikali kuondoa Ushuru wa Forodha wa *EFD machines* kutoka asilimia kumi mpaka sifuri, wafanyabiashara wadogo wadogo walikuwa hizi mashine wananunua kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Serikali imepunguza hili ili wafanyabiashara wapate hizi mashine kwa bei rahisi, kodi ikusanyike, mtu anasema hapana kwenye hii bajeti, nitamshangaa, labda kama hawakilishi wananchi. Kwa sababu hizi mashine zilikuwa zinasumbua, leo Serikali imepunguza hizi gharama ili wapate kwa bei rahisi kodi ikusanyike unakataaje hii bajeti?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili anijibu ambaye anategemea kuikataa hi bajeti; kima cha chini cha kodi kimepunguzwa kwa shilingi 50,000 mpaka 100,000, mtu ambaye mauzo yake si zaidi ya milioni 14 zaidi ya 100,000 imepunguzwa, wananchi wetu wamepunguziwa mzigo wa kodi; mtu anakataaje hii bajeti, hawa wafanyabiashara wadogo wadogo tunaowakilisha? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo natamani nijibiwe kwa nini huyu mtu akatae hii bajeti; hawa

wafanyabiashara wadogo wadogo walikuwa wanaandaa mahesabu yao mtaji wa kuanzia milioni 20 alikuwa anatakiwa ampage mtu wa *CPA* amuandalie bajeti yake, lakini sasa hivi ni mpaka mtu mwenye mtaji wa milioni 100, hao wa chini wameachwa ili mitaji yao ikue; unakataaje hii bajeti? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne; Mheshimiwa Waziri ameongeza tena muda wa miezi sita kwa wale ambao walikuwa wanadaiwa riba za kodi mpaka mwezi wa 12 ili walipe zile kodi wanazodaiwa, amewapunguzia mzigo huo. Huyo anayekataa hii bajeti wananchi wake wamepunguziwa huo mzigo ni nani? Labda kama hawawakilishi wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tano, kuanzisha Kitengo cha *Ombudsman*, cha kupokea malalamiko ya wafanyabiashara ambao walikuwa wanaombwa rushwa, ambao walikuwa wanafungiwa maduka yao, kodi zinadaiwa kwa nguvu. Leo Serikali imeona iandae kitengo maalum kabisa cha kusikiliza malalamiko ya wafanyabiashara pale wanapoonewa. Mtu anasema hataki, maana yake wafanyabiashara wetu waendelee kutozwa kodi kubwa ambayo hawastahili, wafanyabiashara wetu waendelee kuchukuliwa rushwa. Mimi kama Mbunge ninayeongoza Jimbo la Babati Mjini ambalo hawa wafanyabishara wamekuwa wakiteseka nasema bajeti hii hajjawahi kutokea. Sasa nasubiri huyo anayekataa kwenye bajeti hii lake kuna wafanyabiashara au hakuna wafanyabiashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa kuliko yote, wafanyabiashara walikuwa wanalia hapakuwa na *grace period* ya kodi. Unakwenda tu unapewa *TIN* na kodi unakadiriwa hapohapo, leo Serikali imewapa miezi sita kafanye biashara yako halafu tuje tukukadirie kodi. Halafu mtu unasimama unasema hapana kwenye bajeti hii, labda kama unaongoza fisi, ngedere, siyo binadamu hawa tunaowaongoza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni bajeti ambayo mimi binafsi sijawahi kuiona. Pia kuna watu walikuwa wamechimba visima vyao, kila mwezi wanalipa Sh.100,000, Serikali imeondoa hiyo, mtu anasema hapana kwenye bajeti hii ili wananchi waendelee kutozwa wapate tatizo la maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho katika haya mazuri kwa siku ya leo; tozo zaidi ya 54 zile za *TFDA*, *TBS*, zimeondoshwa. Kulikuwa na halmashauri inakwenda kukagua biashara ya mama lishe, *TFDA* wanakwenda kukagua inatozwa mara mbili, wananchi walikuwa wanalalamika. Leo hii Serikali imeondoa tozo zaidi ya 54 halafu eti siku ya kupitisha bajeti mtu anasema hapana. Mimi nafikiri siku hiyo *TV* zionyeshe kabisa Watanzania watu gani ambao hawataki wananchi wapate maisha nafuu, wawaone kwa haya mazuri atakayesema hapana kwenye bajeti hii, huyo ni adui wa Watanzania na wajasiriamali wadogo wadogo na Watanzania zaidi ya milioni 45.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri siku hiyo *TV* zionyeshe kabisa Watanzania watu gani ambao hawataki wananchi wapate maisha nafuu wawaone kwa haya mazuri, atakayesema hapana kwenye bajeti hii, huyo ni adui wa Watanzania na wajasiriamali wadogo wadogo na Watanzania zaidi ya milioni 45. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu tu kwa Serikali yangu, nawaomba, suala la watumishi siyo la kwoo. Mmelipa madeni, mmeendelea ku-review madeni yao na kuyalipa, kamilisheni hilo la upande wa wafanyakazi. Wasifanye wao ndio wanabeba, mnafanya mambo mazuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zitto Kabwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Mnzava na Mheshimiwa Vedasto Ngombale, ajiandae

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2018 Serikali ilikuja na pendekezo kwenye Bunge lako Tukufu la kuweza kutoa unaifuu kwa wanawake milioni 13 wa nchi hii katika matumizi yao ya taulo za kike kila mwezi. Mwaka huu Serikali imeona kwamba pendekezo lile halijaleta yale matokeo ambayo ilikuwa inayataka. Ukurasa wa 38 Waziri wa Fedha anasema, kwa kuwa pendekezo lile halijawezesha kupatikana kwa bidhaa hiyo, muhimu kwa bei nafuu kwa walengwa na badala yake pendekezo lile limefaidisha wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kabisa kwamba Serikali ikawa *concerned* kwamba bei ya taulo za kike haikushuka kutokana na mapendekezo ambayo Serikali iliyaleta, lakini Serikali inapaswa kujitafakari; je, mwaka mmoja ambao utekelezaji umefanyika unatosha kuweza kupima matokeo ya sera ile ambayo iliyefanya mwaka 2018? Katika hilo naomba niikumbushe Serikali kwamba mwaka 2018 Serikali ilikuja na pendekezo la kuongeza kodi kwenye mafuta ghafi yanayotoka nje ili kulinda wazalishaji wa mbegu za mafuta hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika na Bunge lako Tukufu kwa pamoja, nataka tutazame nini matokeo ya pendekezo lile ambalo Serikali ililileta? Mwaka 2017 kabla ya kodi zile kupandishwa katika uzalishaji wa mazao ya mafuta tulikuwa tunazalisha tani 6,600,000 mwaka 2017 kabla ya kupandisha kodi ili kudhibiti uagizaji wa mafuta kutoka nje. Mwaka 2018 tumezalisha tani 1,600,000 ni ukurasa 135 wa taarifa ya hali ya uchumi; pungufu la *negative seventy six per cent* (-76%) kwamba pendekezo ambalo Serikali ililileta mwaka 2018, matokeo yake ukurasa wa 135 wa Taarifa ya Hali ya Uchumi. Matokeo ya kuweka kodi hayakuzalisha tegemeo la uzalishaji wa mbegu kuongezeka, lakini Serikali mwaka huu haijaja na pendekezo la kufuta lile pendekezo la mwaka 2018. Matokeo yake imeendeleza pendekezo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kuna *transition period*. Huwezi ukaweka pendekazo la kikodi sasa ukategemea matokeo ya haraka hapo hapo. Kodi imeanza tarehe 1 mwezi Julai, kuna watu walikuwa wana *stock* ambazo walizinunua hazikuwa na hiyo *exemption*. Lazima wataendelea kuziwa kwa fedha zile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Mheshimiwa Waziri wa Fedha anafahamu, tumepata mtikisiko hapa katikati wa fedha yetu kuporomoka thamani dhidi ya dola za Kimarekani. Taulo za kike zote tunazoagiza nchi hii zinatoka nje. *Factor* ya *exchange rate* tumeitazama?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi natoa rai kwa Serikali kwamba siyo sahihi kuja kufuta ile *exemption* tuliyoiweka mwaka 2018. Serikali inapaswa kutazama vizuri, kutoa muda wa kutosha, kama namna ambavyo imetoe muda kwenye mafuta licha ya kwamba uzalishaji umeshuka, tutazame pia tutoe muda kwenye eneo hili la taulo za kike. Uamuzi wa mwaka 2018 uliipa sifa nchi yetu, tulikuwa ni *a pioneer country* katika kulinda wanawake wa nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, India wametuwa, wametuiga sisi, Australia wametuwa, wametuiga sisi na nchi nyingine mbalimbali. Mwaka huu *South Africa* wametuiga sisi. Sisi tunarudi nyuma kwa sababu tu ndani ya mwaka mmoja, bei haikushuka, hapana, siyo sahihi. Naisihi Serikali itazame upya pendekazo hili na itazame upya pendekazo hili kwa kuwa tayari ndani ya bajeti ya mwaka huu Serikali imependekaze kuondoa ushuru kwenye malighafi zinazozalisha taulo za watoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, malighafi za taulo za watoto ndiyo malighafi za taulo za kike. Meza ambayo inapaswa kufanya kwenye taulo za watoto, ndiyo meza hiyo hiyo inatakiwa kufanya kwenye taulo za kike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naisihi Serikali, moja, pendekazo...

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

## **TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa msemaji kwamba tozo anayosema imepunguzwa kwenye malighafi za *diapers*, tozo hiyo pia kwa miaka minne mfululizo imeondolewa kwenye malighafi za kutengeneza taulo za kike. Kwa hiyo, hili jambo lipo, siyo kwamba ni jambo geni ambalo linatakiwa kupendekezwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto Kabwe unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa hiyo, *VAT exemption* kwenye taulo za kike mwaka huu, labda kuwe na sababu nyingine, lakini kwa sababu ya bei kutokushuka, naomba Serikali itazame upya kwa sababu ni jambo ambalo linaweza kutatuliwa *administratively*. Tuna tatizo kwamba *retailers*, wauzaji wa mwisho *margin* yao kwenye taulo za kike ni kubwa sana na jambo hili linaweza likatekelezwa *administratively* kwa kuhakikisha kwamba wanakaa na kuweza kupata suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala zima la uwekezaji katika nchi yetu. Serikali inazungumza kwamba pato letu la Taifa linakua kwa 7%. Sitaki kuingia kwenye ubishani kati ya Serikali ya takwimu zao na takwimu za taasisi nyingine. Hata hivyo tumeona kuwa ndani ya mwaka mmoja, kwa mujibu wa taarifa ya hali ya uchumi, uwekezaji nchini umeporomoka kwa asilimia 44.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2017 thamani ya uwekezaji ndani ya nchi yetu ilikuwa ni dola za Kimarekani

bilioni 5.2. Sasa hivi imeshuka mpaka dola za Kimarekani bilioni 2.8. Mauzo yetu nje yameporomoka sana na urari umekuwa hasi na tumewahi kuwa na urari wa bidhaa katika ya biashara ya ndani na nje ukiwa chanya miaka ya nyuma iliyopita. Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango anafahamu na ni wote wawili; Waziri na Naibu Waziri anafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pato la Taifa, unachukua *consumption*, unachukua *investment*, unachukua *government expenditure*, unachukua *export minus imports*. *Investment negative forty four (-44) growth* ya matumizi ya Serikali kwa maana ya bajeti ya Serikali inaongezeka kwa 2% tu sasa hivi. *Export minus imports negative*, kwa sababu tuna-import zaidi kuliko ku-export, pato la Taifa litakuwaje katika mazingira kama hayo? Ni lazima Serikali ifanye kazi ya bidii kuhakikisha ya kwamba tunaongeza zaidi *exports* nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia, licha ya miradi ambayo inazungumzwa, hali ya uchumi wa wananchi, uzalishaji wa wananchi unashuka sana. Angalieni mazao yetu ya kilimo, ukiangalia Taarifa ya Hali ya Uchumi unaona na baadhi ya maeneo tunaona uzalishaji unashuka kwa sababu tu ya sera za Serikali ambazo siyo sahihi. Naomba Serikali iweze kutazama kwa umakini. Haiwezekani ukawa na *growth* kubwa kama *foreign direct investment* na *export* zetu zinazidi kushuka mwaka hadi mwaka kwa sababu unakosa *inflows* kwenye nchi ambalo ni jambo la muhimu sana kwa ajili ya kuweza kuhakikisha kwamba uchumi unaweza kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna *continental free trade area*, Waafrika tunatakiwa tuwe katika uchumi wa pamoja.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Ni ya pili? Samahani, nashukuru sana, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Timotheo Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedasto Ngombale na Mheshimiwa Innocent Bilakwate, ajiandae

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, aliyetujaalia uzima. Pia nitumie nafasi hii kwa dhati kabisa kuipongeza Serikali, kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa kazi kubwa wanayoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni mara yangu ya kwanza kuchangia bajeti ya Serikali. Tangu nimekuwa Mbunge hii ni mara yangu ya kwanza kuchangia bajeti. Nafarijika sana kuona kwamba nakwenda kuchangia bajeti ambayo ukilisoma unaiona bajeti inayogusa maisha ya watu wa Tanzania. Yanaweza yakasemwa maneno mengi, kunaweza kuwa na hadithi nyingi, lakini ukweli ni kwamba bajeti iliyowasilishwa inakwenda kugusa maisha ya wananchi wetu kwenye maeneo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali. Hii miradi mikubwa tunayofanya, inawezekana matokeo yake yasionekane kwa haraka leo, lakini ni miradi ambayo inakwenda kutuvusha kama Taifa kutoka hapa tulipo tuweze kwenda kwenye hatua nyingine. Unapoona mtu analalamika anasema hali ya uchumi ya watu wetu siyo nzuri, mtu analalamika anasema tume-*import* sana kuliko ku-*export*, lakini wakati huo huo miundombinu ya kusaidia tuwe na viwanda vya kutosha kwenye nchi yetu watu wanaipiga vita. Ni vitu vya ajabu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapotaka kuwa na umeme wa uhakika ni kwa ajili ya kusaidia viwanda, unapotaka kuwa na miundombinu ya barabara ya uhakika, kuwa na bandari ya uhakika ni kwa ajili ya kusaidia viwanda, ukipata viwanda vingi ukazalisha vizuri, tutafika huko tunakotaka kufika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nimeona tangu mjadala huu umeanza tumekuwa tukipigana kelele, mtu anasema, Serikali hii hakuna kitu illichokifanya. Pia tumefika mahali tunahukumiana kwa kutumia llani za Vyama tulizotumia kwenye uchaguzi wetu wa mwaka 2015. Sisi wote tunajua, Vyama vinapokwenda kwenye uchaguzi, llani tunazozinadi tunazinadi kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania kwa miaka mitano, ndiyo muda tuliojiwekea kwa uongozi kama Taifa kwa mujibu wa Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, muda wa kutekeleza llani ni miaka mitano. Miaka mitano haijaisha, *pressure* hizi zinatoka wapi?mtu anaongea kana kwamba leo ndiyo tunamaliza, Serikali inakwisha, muda wa uongozi umekwisha, tunakwenda kwenye uchaguzi. Hii siyo sawa sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wamezungumza kuhusu shilingi milioni 50, mtu anapiga kelele anasema mliwaahidi Watanzania shilingi milioni 50, ziko wapi? Kwanza nikubaliane kabisa na dada yangu Mheshimiwa Gekul. Tunapoahidi vitu, Serikali iliyopo madarakani iliahidi vitu vingi, kila kitu kinafanyika kulingana na nafasi na wakati ambao tunao. Hizo shilingi millioni 50 za kwenye vijiji, yako mambo yamefanyika makubwa kwenye maeneo ya watu wetu na yanayogusa maisha ya Watanzania, tofauti hata na hiyo shilingi milioni 50 ingekwenda moja kwa moja kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Serikali, tumefanya vizuri kwenye maboma ya shule za sekondari na za msingi, tupeleke na huo moyo kwenye zahanati kwenye vijiji ambavyo watu wetu wapo. Wananchi wetu wanajitoa sana kwenye ujenzi wa zahanati, tumefanya vizuri kwenye maboma shule za sekondari na za msingi, hebu twende tukasaidie na kwenye zahanati. Huyo anayesema kwamba bajeti haigusi maisha ya watu, akaangalie maji, zahanati na barabara, atasema kama bajeti inagusa maisha ya watu au haigusi maisha ya watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri mambo machache kwa ajili ya kusaidia kuongeza mapato kwenye nchi yetu. Mheshimiwa Waziri wa Fedha unafahamu, inawezekana kabisa wakati mwingine kuongeza kodi kukakupunguzia idadi ya watu wanaoweza kuwa walipa kodi. Inawezekana kabisa kuongeza kodi kukakupunguzia idadi ya watumiaji wa huduma ambayo ingesaidia kupata kodi. Sasa naomba sana Mheshimiwa Waziri hili jambo tuliangalie vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mimi nilikuwa naangalia tu barabarani mle, miaka michache iliopita watu waliokuwa wanatumia magari ambayo yamesajiliwa kwa majina yao, ninavyoona kama idadi ile inapungua. Ukiangalia vizuri, inawezekana imesababishwa na kuongezeka kwa kodi ile, lakini kodi ile ingekuwa angalau kwenye kiwango kizuri, ni rahisi kupata watu wengi zaidi na kupata kodi nyangi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili lipo pia kwenye *Sports betting*. Tunachukua kodi kule, wale waendeshaji wanalipa asilimia 25 ya mapato ghafi wanayopata, lakini na yule mtu ambaye anashinda kwenye ile zawadi anayopata analipa asilimia 20. Wako watu ambaao kwa kuona kwamba wanalipa kodi, wengine wameamua kuacha hizo, wameamua kufanya za *online*, inasababisha kwenda kukosa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Mheshimiwa Waziri, tuangalie namna ya kupunguza kodi hasa kwa wale ambaao wanashinda ili ku-*encourage* watu wengi zaidi waweze kushiriki ili kutengeneza kodi zaidi kwa wale wanaoendesha lakini pia wanalipa kodi kwenye huduma nyininge kama wakifanya matangazo wanatoa ajira kwa watu wetu na vitu vingine vya namna hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye upande wa utalii. Juzi hapa tumefanya mnada wa vitalu. Katika vitalu 26 naambiya tumefanikiwa kuuza vitatu saba. Hii imechangiwa sana na ongezeko la gharama za kununua

vile vitalu. Naiomba Serikali, vitalu hivi vikikaa kwa muda mrefu bila kuwa na watu waliovichukua tunapata hasara sisi kama Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati yako ya Bunge, Ardhi Maliasili na Utalii. Tuliishauri sana Serikali, tunaweza tukaweka makadirio yetu lakini tusiyatangaze, lakini pia tusiwe *rigid* kwenye hayo makadirio ambayo tumeyaweka, lakini pia tusiongeze sana ili kuweza kusaidia watu wengi waweze kujitokeza na kuja kuomba kununua vitalu ili tufanye biashara na Serikali iweze kupata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye upande wa utalii ni kwenye hoteli. Miaka ya nyuma Serikali yetu iliamua kubinafsisha baadhi ya hoteli. Ziko baadhi ya hoteli nyingine ambazo ziko chini ya Serikali pia ziliuzwa. Watu waliobinafsishiwa hoteli hizi, ukienda vizuri, hoteli nyingi zilizobinafsishwa hazifanyi kazi vizuri na kwa kutokufanya kazi vizuri hazitengenezi vizuri ajira, hazitengenezi vizuri mapato kwa maana ya kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahangaika sana kukuza utalii na utalii ni eneo ambalo tunaweza kutusaidia kama Taifa kupata fedha nyingi, lakini tunakuza utalii, lakini ili tuwaalike watalii wengi zaidi waweze kuja kwenye nchi yetu, wakati huo huo miundombinu tuliyokuwa nayo haiendani na hii kasi ya uingizaji wa watalii kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye nchi yetu ukilinganisha vitanda ambavyo tunavyo vinavyoweza kulipiwa kodi, ukilinganisha na nchi jirani za wenzetu, sisi bado tuko nyuma sana. Tungeweza kutatua tatizo hili kwa kwenda kuziboresha hoteli ambazo ziko ndani ya nchi yetu. Cha kusikitisha zaidi, ziko hoteli ambazo tulizibinafsisha, watu wakachukua zile hoteli, wakachukua mikopo, wakafungua biashara nyingine za namna ile kama hoteli na wakafanya kazi na wanafanya kazi vizuri. Zao zinakwenda vizuri, walizobinafsishiwa na Serikalihaziendi vizuri. Naishauri sana Serikali, tuna jambo la kuangalia hapa. Tuangalie namna ya

kuboresha hizi huduma za hoteli ili tuweze kuwasaidia watu wetu, tuweze kusaidia nchi yetu kuweza kupata mapato zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubaliana kwamba kilimo ni mionganoni mwa maeneo muhimu katika kutafuta malighali kwa ajili ya viwanda vyetu. Naiomba sana Serikali, tuendelee kuweka mkazo kwenye kilimo, hasa kilimo cha umwagiliaji ili kuhakikisha kwamba watu wetu wanazalisha zaidi na wapate soko la kuweza kulisha viwanda vyetu na waweze kupata fedha, lakini pia viwanda viweze kwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kule Korogwe tunalo bonde ambalo likitengenezwa mradi wa umwagiliaji, tunaweza kulima hekta 5,000. Kwa karne tuliyonayo hekta 5,000 ni eneo kubwa sana. Ukiwa na wananchi 5,000 wamejiingiza kwenye kilimo cha uhakika wanaweza kulima kwa zaidi ya mara mbili kwa mwaka mmoja. Ni kuwa na misimu ya kilimo zaidi ya miwili kwa mwaka mmoja. Ni jambo kubwa sana. Tunatengeneza uchumi mzuri kwa ajili ya maisha ya watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema nichangie hayo machache kuishauri Serikali namna ya kuongeza mpato, kubwa nasema bajeti hii ni nzuri, bajeti hii inafaa, bajeti hii inagusa maisha ya wananchi wetu moja kwa moja, watu wamepiga kelele tulikuwa tunaomba sana tozo zipunguzwe tusiwe na mtiririko wa kodi na ndiyo *spirit* ya Mheshimiwa Rais, bajeti hii iliyowasilishwa inajibu hoja hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono bajeti hii. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Vedasto Ngombale atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwatwe tutamalizia na Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani kwa kunipa nafasi. Nianze na hali ya uchumi hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaonyesha kwamba pato letu la Taifa linapanda lakini uhalsia wa mambo hali mtaani ni ngumu, vyuma vimekaza mambo hayaendi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, viashiria vinaonyesha kwamba hali ni ngumu kwa sababu kwanza kwa sasa hata bidhaa tunazosafirisha kwenda nje zimepungua, mazao kama korosho, kahawa kiasi tunachosafirisha kwenda nje kimepungua. Kutokana na hiyo pia kuna hoja ya mikopo katika sekta binafsi imeshuka. Sambamba na hilo mfumuko wa bei umepungua upo chini ya asilimia tano. Sasa wachumi wanatuelekeza kwamba kama hali ndiyo hiyo ya mfumko wa bei, unaweza ukaathiri kwanza ukasabaisha kutovutia wawekezaji, pili mikopo kutolipika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama hivyo ndivyo ilivyo, mimi siyo mchumi lakini nilikuwa na wazo katika suala moja. Kama mfumko wa bei umeshuka, Wabunge wengi waliposimama wakati wa Bajeti ya Maji walipendekeza Serikali iongeze tozo ya shilingi hamsini katika lita ya mfuta ili basi kupata fedha nyngi pesa nyngi za kutosha kwa ajili ya kuondokana na tatizo la maji. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama mfumuko wa bei umeshuka kwa nini usikubaliane na pendekezo hilo la Waheshimiwa wa Bunge ili basi tukaondokana na tatizo la maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo ambalo Serikali ya CCM bado haijashughulikia vizuri ni tatizo la maji, kuna tatizo kubwa sana la maji. Kama tumefanikiwa kwenye umeme kuititia *REA* kwa utaratibu wa kuweka tozo katika mafuta *why not* tusifanya katika maji kuna tatizo kubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliangalie suala hili kuna tatizo kubwa miradi ya maji haiendi kwa sababu pesa hakuna. Kwangu kule Kilwa tumefanya *contract* na watu wa *DDCA* sasa tuna mwaka wa nne kila siku tunagomba hapa visima havichimbwi kwa sababu *DDCA* hawana pesa, sasa kama

tutakuwa tuna pesa ambazo tumezi- *ring fence*, nafikiri tunaweza tukafanikiwa kutatua tatizo la maji kama ambavyo tumefanikiwa kwenye umeme. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine ni suala zima la mikopo ambayo Benki Kuu imepunza riba kwa benki lakini benki bado hazipunguza riba kwa wateja. Mheshimiwa Waziri wa Fedha ukapokuja hebu tuambie kama Benki Kuu imepunguza riba tena imepunguza sana, kwa nini wateja nao wasipunguziwe riba? Kwa sababu sasa uwezo wa watu kukopa, watu wengi wanaogopa kukopa lakini pia watu wengi wanashindwa kulipa mikopo ambayo wamekwisha kopa. Nalo hilo naomba ulingalie ili basi Watanzania waweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine niende kwenye suala zima la mifugo na uvuvi. Mheshimiwa Waziri wa Fedha katoa mapendelekezo ya kuondoa karibu tozo 15 kwenye sekta ya uvuvi na sekta hii inasimamiwa na Wizara ya Uvuvi na Mifungo, lakini hajaondoa tozo hata moja kwenye sekta ya uvuvi. Mifugo tozo 15 zimeondoka, kwenye uvuvi hata moja hujaondoa tozo. Napata shida kwamba pengine Mheshimiwa Mpina yale mapendelekezo yetu ya shida wanazopata wavuvi haukupelekewa labla, nataka niamini hivyo.

## TAARIFA

**NAIBU SPIKA:** Nani aliyesema taarifa?

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipo hapa.

**NAIBU SPIKA:** Aaaah! Mheshimiwa Julius Kalanga.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kumpa tu taarifa mzungumzaji kwamba siyo busara sana kuendelea kutoa *reference* ya mapunguzo ya tozo katika mifugo kwa sababu kulikuwa kuna umuhimu wake wa kupunguza. Kama kuna hoja ya kudai punguzo kwenye

samaki tudai bila kuona kwamba kupunguza kwenye mifugo maana yake imeathiri haki ya wavuvi, nimeona mijadala hii ikiendelea hivi kanakwamba wafugaji wao hawastahili kupunguziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nafikiri tujenge hoja kulingana na mazingira tuliyonayo kuliko ku-*justify* kwamba tusipunguze kwenye mifugo tupunguze kwenye samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kalanga sidhani hiyo ndiyo hoja ya kwamba mifugo iliyopunguziwa tozo 15 zipungue ili zipelekwe kwenye uvuvi, ni kwamba mifugo tozo zimepungua 15, kwenye uvuvi hakuna nadhani ndiyo hoja ambayo Mheshimiwa Mbunge anajaribu kuiweka hapo. (*Makofi*)

**MHE. VEDASTO E.NGOMBALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa ufanuzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vedasto. (*Makofi*)

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sikusudii kutaka kubagua hizi sekta hapana, hizi sekta zote zinasimamiwa na Waziri mmoja. Waziri na Waheshimiwa Wabunge mnaweza mkawa mashahidi kwa kadhiya ambayo imewapata wavuvi kwenye suala zima la kuchomewa nyavu zao, kwenye suala zima la tofauti ya tozo kati ya dagaa wanaovunwa baharini na dagaa wanavunwa ziwani. Kwa mfano, baharini tozo ya kilo moja ya dagaa ni Dola ya Kimarekani 1.5. Ukienda Ziwa Tanganyika tozo ni Dola za Kimarekani ni 1.5, ukienda Ziwa Victoria Dola za Kimarekani 0.16. sasa ni matarajio yetu sasa hii tofauti Mheshimiwa Waziri wa Fedha wewe ndiyo Baba ungekuja kurekebisha kwa sababu kama nchi moja halafu kunakuwa na tofauti ya tozo inatusumbua sana. Sasa tukiona kwamba sekta hii imeshughulikiwa na nyiningine haijashugulikiwa ndiyo maana tunataka Mheshimiwa Waziri wa Fedha utusaidie katika hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni suala zima la korosho, ni dhahili shahili kutohana na maamuzi yaliyofanyika kwenye korosho uchumi umetetereka na hasa wa Mikoa ile ambayo inazalisha korosho. Kwanza mpaka sasa kuna baadhi ya wakulima wengi hawajalipwa na hasa wale wakulima wa chini, hata katika zile pesa ambazo zimelipwa sasa kuna tofauti ya malipo kati ya Wilaya moja na nyingine, kuna Wilaya ambazo zimelipwa mpaka asilimia 90 lakini kuna Wilaya nyingine hata asilimia 50 haijafika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekeso langu na ushauri, korosho zile zipo maghalani na zinazidi kuoza, wapo wafanyabiashara ambao wanataka kununua ninaishauri Serikali na hasa Waziri wa Wiwanda na Biashara Mheshimiwa Rais amekuchangua ili uweze kufanya maamuzi, fanya maamuzi ya kuza korosho zile hata kwa bei ya chini kwa sababu kadri zinavyozidi kukaa korosho, zinaaharibika ziuzwe sasa angalau tupate nusu hasara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba zile korosho huwezi kuziiza katika bei ile kwa sababu sasa zimeshaanza kuharibia. Sasa nishauri Serikali uzeni angalau tupate chochote kitu ili mambo yawewe kwenda sawa pia wale ambao hawajilipwa walipwe kwa sababu msimu mwingine una karibia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie suala zima la bandari. Katika ukurasa namba 28 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika kipengele cha tatu anasema ana kusudio la kuwekeza kwenye maeneo ambayo Serikali inaweza kupata mapato zaidi hususan katika uvuvi wa Bahari Kuu kwa kujenga bandari ya uvuvi na ununuzi wa meli za uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Serikali ni kama ina kigugumizi kwamba ni bandari gani sasa iwe bandari ya uvuvi. Katika nchi hii kuna bandari nne, kuna Bandari ya Tanga, Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Kilwa na kuna Bandari ya Mtwara. Bandari hizi tatu tayari Serikali

imeshafanya mkakati wa kuziendeleza, lakini Bandari ya Kilwa hakuna chochote ambacho kimefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza Serikali sasa iifikirie bandari ya Kilwa kuwa kama bandari ya uvuvi. Bandari ya Kilwa ina historia kubwa, ukisoma historia ya toka enzi ya Ibn Battuta wanaitaja Bandari ya Kilwa, Mvumbuzi Ibn Battuta alipotembea alipofika katika Bandari ya Kilwa alikutana na Mji mkubwa unaovutia. Sasa kama tuna bandari ya kale toka enzi ya Dola ya Kilwa, lakini mpaka sasa Serikali hajakumbuka kuindelezea. Nafikiri sasa Serikali ione umuhimu wa kuingalia Bandari ya Kilwa na iipe kipaumbele ndiyo iwe bandari ya uvuvi hiyo itakuwa hata mizimu itatuona maana hiyo ndiyo bandari ya kale, kwa kufanya hivi tunaweza kupata mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Bilakwate atafuatiwa na Mheeshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu na bajeti ambayo kwa kweli kila mmoja ambaye ameisoma bajeti hii kwa kweli inagusa maisha ya Watanzania na imekuwa bajeti ya mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kunipa afya na nguvu lakini pia nimpongeze Waziri Dkt. Mpango kwa kazi nzuri unayoifanya na tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kukupa afya nikutie moyo kelele hizi unazozisikia kutoka kwa wenzetu usitegemee zitaisha, wewe unaposikia kelele ujue mambo yanakuwa mazuri songa mbele uendelee kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii kwa jinsi ambavyo imeletwa kama tutaisimamia vizuri ninaamini uchumi wa Taifa letu unaenda kuinuka na tunaenda kuona mambo makubwa ambayo hatujawahi kuyaona katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kwa upande wa kilimo, pamoja na jitihada za Serikali bado hatuja wekeza nguvu kubwa ya kutosha kwenye kilimo. Nasema hivi kwa sababu tunataka kuingia kwenye uchumi wa viwanda ili viwanda vyetu viweze kupata nguvu kubwa lazima tuwe na malighafi ambazo zinapatikana katika nchi yetu, tusitegemee kupata malighafi ambazo zitatoka nje kuendeleza viwanda vyetu. Kwa hiyo, tujikite kwenye kilimo ambacho kitainua kwanza kipato cha Mtanzania na asilimia kubwa zaidi ya 80 ni wakulima, tukiwekeza kwenye kilimo kwa mfano wakapata mbegu bora wakawa na masoko ya uhakika, dawa na pembejeo ninaamini tunaweza uchumi wa Taifa letu ukainuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Serikali imejikita kwenye mazao ya kimkakati ambayo ni korosho, pamba, chai, kahawa mazao haya tukiyasimamia ninaamini yanaweza yakainua kipato cha nchi yetu pia kipato cha mkulima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la zao la kahawa ambalo tukilisimamia vizuri linaweza kuingiiza pesa nzuri na nyangi kwenye Taifa letu, lakini pamoja na kuondoa zile tozo ambazo zilikuwepo bado kahawa haijaweza kumnufaisha mkulima. Zao la kahawa siyo linalimwa Kagera tu zao la kahawa linalimwa maeneo mengi katika nchi yetu, niombi sana Serikali ilisimamie.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki ni kitu cha kushangaza pale kwangu Kyerwa ukivuka tu mpaka hata ukiita wanasi, ukivuka tu mpaka ukienda Uganda kahawa ni shilingi 2000 lakini ukija kwetu ni shilingi 1100. Ukienda kwenye nchi ya Rwanda kahawa ni shilingi 3000. Ninaiomba sana Serikali hawa wenzetu hii kahawa wanaiuzwa wapi tuangalie huko wanakouza kahawa na njia wanazotumia ili tuweze kuinua kipato cha mkulima lakini kipato cha Serikali yetu ninaamini hili litasimamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la kahawa kuna watu ambao mimi ninaamini bila kuingilia kat, Serikali

ikaingilia na Waziri wa Kilimo angekuwepo hili akalisikia, kuna Bodi ya Kahawa, unasema unaunda Bodi ya Kahawa hii angelisikia kuna Bodi ya Kahawa, wewe unasema unaunda Bodi ya kahawa hii bodi inawakilisha wafanyabiashara hakuna mkulima hata mmoja ambaye anawakilishwa mnategemea hawa wakulima ni nani atakayewasemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na vikwanzo vingi kwa mfano mwaka jana tulipata *KDCU* ambao ni Chama cha Ushirika walipata mteja kwa kununua kahawa lakini ilichukua siku 28 kutoa kibali, hii ndiyo bodi ya kahawa na ofisi ya Mrajisi. Mwaka huu tunatangaza msimu wa kahawa mwezi wa Tano mpaka sasa hivi bado kibali hakijatolewa na Benki ya Kilimo ipo tayari kutoa pesa imetenga zaidi ya bilioni 40, lakini bado ofisi ya Mrajisi haitoi kibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni vikwazo ambavyo haviwezi vikainua kilimo kwa sababu huyu mkulima anakata tamaa, lakini kama tukiondoa hivi vikwazo ambavyo viro kwenye Tume ya Ushirika viro kwenye Bodi ya Kahawa na viro kwenye ofisi ya Mrajisi, nanaamini mkulima ataongeza kilimo na pato la Taifa litaongezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nnaipongeza sana Serikali kwa kuwekeza katika mradi mkubwa huu wa umeme, tunasema tunaingia kwenye uchumi wa viwanda hatuwezi tukaingia kwenye uchumi wa viwanda kama hatuna umeme wa uhakika. Hatuwezi tukawakaribisha wawekezaji kuja kuwekeza kwenye nchi yetu kama hatuna umeme wa uhakika. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa maamuzi makubwa na mazito ambayo imeendelea kuyachukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi Wabunge tulikuwa tunalalamika tunasema Serikali inashika huku, inashika huku haileti miradi ambayo inaweza ikasimamia sasa Serikali imekuja na miradi hii mikubwa nilitegemea kama Wabunge wote tuungane kwa pamoja tuiunge mkono

Serikali kuona hii miradi inakamilika, sasa hivi tunashauri, sasa Serikali ikifaya wenyewe tunageuka! Kwa kweli huu niseme ni kama uwendawazimu au ni kama uigizaji, tufanye mambo ambayo tunashauri Serikali, Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali sikivu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine watu walikuwa wanalamika wanasema tumewekeza kwenye mradi wa *Stigler's Gorge*. Huu mradi ninaamini tumekuwa tukilalamika Wabunge tunasema barabara zetu zinaharibika kwa sababu ya mizigo, huu mradi utakapokuwa umekamilika tunaamini barabara zetu zitakuwa salama na usafirishaji utakuwa mzuri kuongeza kipato cha Taifa. Tunaboresha bandari, bandari tunapoiboresha tunategemea mzigo tena ije ipite barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niendelee kuipongeza sana Serikali kwa kazi hii inayofanyika, tusitegemee wenzetu kuwa wasifia kwa sababu yale ambayo walikuwa wanashauri ndiyo leo tunayoyafanya, kwa hiyo wamekosa hoja hawana jambo jingine ambalo wanaweza kuja nalo jipya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Serikali na niiombe sana Serikali Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango bajeti hii kama ulivyoiletu Mungu akuwezeshe uweze kuvisimamia vizuri na ninaamini tunakoenda tunaenda kuzuri, Tanzania tunavyopiga hatua siyo kama Tanzania ya miaka 20 iliyopita na mtakujaa kujionea wenyewe kwenye Uchaguzi Mkuu unaokuja uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mtaona mambo makubwa ambayo Watanzania wanayaona wakati mwingine mnawezza mkafikiri Watanzania hawasikii, Watanzania wanasikia na wanaona mambo makubwa yanayofanyika katika Taifa hili na ndio maana kila kona tunakoenda Mheshimiwa Rais anaungwa mkono na Serikali yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya ninakushuru, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya idadi ambayo Wabunge ambao wanapaswa kuchangia leo nalazimika kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) kuongeza nusu saa ili Mheshimiwa Goodluck Mlinga aweze kumalizia katika kipindi chetu hiki cha kwanza. (*Makofi*)

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapa mkononi nina kitabu kimeandikwa hivi: Ilani ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, ni wakati wa mabadiliko wa kuondoa umaskini chagua CHADEMA tarehe 25 Oktoba, 2015. Kitabu hiki ukurasa wake wa 13 kimeandikwa hivi: "CHADEMA inaamini maendeleo ya kweli yataletwa na Serikali itakayokuwa na nia na mkakati wa kweli wa kupambana, kuondoa rushwa na ujisadi na siyo kwa maneno kama ilivyozoleka".

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba waende wakatembelee Keko na Segerea watapata majibu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitabu hicho hicho ukurasa wa 23 kinasema hivi: "Ujenzi wa miundombinu ya afya lazima uendane na huduma husika. Baada ya miaka 50 ya Uhuru ujenzi wa miundombinu ya afya umeelekeea maeneo fulani na machache". Naomba kuwapa taarifa kuwa sasa hivi vituo vya afya 400 vimeshajengwa vimeelsha na hospitali 67 za wilaya zinaendelea kukamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitabu hicho hicho, ukurasa wa 53 unasema hivi: "Vipaumbele havijawekwa kwenye uendelezaji wa vyanzo vya uzalishaji wa umeme wa bei nafuu vilivyopo nchini, mfano Stigler's kwenye banio la Mto Rufiji". Ilani ya CHADEMA hiyo Rais anafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 40 CHADEMA itafanya nini? Kujenga reli mpya na kukarabati zilizopo kwa viwango vya kisasa na kuzingatia maslahi ya nchi ni pamoja na kujenga uwezo wa kuzalisha mataruma na reli nchini vinafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa huo huo wa 40, CHADEMA itafanya nini? Kuboresha bandari zilizopo na kujenga mpya kuwa vitega uchumi vya Taifa ili kuboresha biashara zilizopotea katika bandari za nchi jirani. Serikali ya CCM inafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa huo huo wa 40, unasema hivi: "Kujenga barabara nchini kwa kuzingatia ubora na hasa zile za vijijiini." Tumeanzisha hadi *TARURA* tunajenga barabara hadi vijijiini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa huo huo wa 40, unasema: "Kujenga Shirika la Ndege la Taifa litakalojidesha kwa misingi ya faida". Mpaka sasa hivi tumeshanunua ndege saba (7), shirika linaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa huo huo wa 40, unasema: "Kujenga miundombinu ya kisasa ili kuondoa msongamano wa magari hasa katika Jiji la Dar es Salaam na Mwanza". *Fly overza kufa mtu zinajengwa Dar es Salaam.* (*Makofi/Vigelegele*)

## **TAARIFA**

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mlinga, kuna taarifa, Mheshimiwa Eng. Ngonyani.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kumpa taarifa msemaji wa sasa kwamba kwa kawaida hizi llani za vyama mbalimbali tunavyoandaa huwa tunadesa. Kwa hiyo, asishangae kuona llani ya CHADEMA anayoisoma ndiyo llani hiyo hiyo ya Chama cha Mapinduzi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata  
utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga, endelea na mchango wako.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Taarifa aliyonipa naipokea nilikuwa naelekeea huko. Hii llani iliandikwa na mtu mmoja anaitwa Mheshimiwa Edward Lowassa na iliandikwa kwa muda wa wiki mbili kabla ya uchaguzi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata  
utaratibu)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, yale ambayo alitoka nayo CCM ndiyo alienda nayo CHADEMA kwa kuamini atatumia kuwashawishi watu. Kwa hiyo, usije ukaona leo hii watu sasa hivi wanakomaa na pedi za kike na mawigi kwa sababu hawana cha kuongea.

## **TAARIFA**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga kuna taarifa, Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpa taarifa kwamba llani ya CHADEMA huwa inatengenezwa mwaka mmoja kabla ya uchaguzi. Hata hivyo, nataka nikubaliane na yote aliyosema na ndiyo maana kila mara tunasema kwamba *brainya* kuongoza nchi hii itatoka CHADEMA. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga, endelea na mchango wako.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ukitaka uthibitishe kuwa anachoongea siyo cha kweli, waulize kama llani inatengenezwa mwaka mmoja kabla Mgombea wa Urais anapatikana kwa muda gani kwa sababu uchaguzi 2015 mgombea alipatikana kwa wiki mbili. Kwa hiyo, sitopokea taarifa yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yote ambayo wao walikuwa wanayapigia kelele Serikali ya CCM inayafanya. Ndiyo maana leo hii hawana hoja na uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaokuja tunaenda kuwapiga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la kuongeza mapato kwa Serikali. Mimi niliwahi kupeleka kampuni moja kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango ambayo ilikuwa inalalamika imeshindwa kusajiliwa nchini, kampuni ya *betting*, kwa sababu illanza biashara kabla ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna makampuni mengi sana ya *betting* ambayo watu wengi wa Tanzania wanacheza na hayalipi kodi, hiyo inaitwa *online betting*. Kampuni ile ilipoenda kufanyiwa upembuzi *TRA* ililipishwa kodi za shilingi milioni 400. Sasa hiyo ni kampuni moja, je, ni kampuni ngapi ambazo zinafanya *betting* Tanzania *online* zikiwa nje ya nchi hazilipiwi kodi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchunguzi tukagundua kwa nini watu wanacheza *online betting* kwa kampuni za nje na siyo Tanzania matokeo yake inaikosesha Tanzania kodi. Sababu kubwa ni *game winning tax* kwa sababu watu wanaamini wanapocheza kamari kwenye makampuni ya nje wanapata zawadi kubwa ambayo haikatwi kodi lakini makampuni yetu ya Tanzania kuna kodi ya *GGR* asilimia 25 na *winning tax* asilimia 20. Kwa hiyo, tunaikosesha Serikali yetu mapato makubwa sana kutokana na *game winning tax* matokeo yake watu wengi wanacheza kamari za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ameliongea mwenzangu, niliongea mwaka jana, nalo ni suala la *plate*

number. Plate number za magari haiongezi gharama katika uzalishaji wake utakapoandika jina la mtu, yaani utakapoweka namba ya kawaida na ukaandika jina la mmliki wa gari gharama ya uzalishaji ni ile ile haiongezeki. Nashangaa Serikali kwa tamaa mmeenda kuweka shilingi milioni 10, haya nikiwauliza leo hii watu wangapi wamesajili kwa majina yao baada ya kuongeza hiyo kodi, hakuna hata mtu mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini mngeweka kwenye magari kuandika *plate number* Sh.2,000,000 na pipipiki Sh.500,000, kuna makabila kama Wahaya wangeandika pipipiki zao zote kwa sababu wanapenda kuonekana. Aidha, Wachaga wangesajili magari yao yote kwa majina. Kwa hiyo, hii ni hela ya bure, Serikali mngefanya hivyo mngepata fedha za bure. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu nalotaka kuliongelea ni utalii. Tujiulize kwa nini Morocco wana *National Parks* kumi lakini wanaingiza watalii zaidi ya milioni kumi kwa mwaka? Tanzania tuna *National Parks* 16 lakini tunaingiza watalii milioni 1 kwa mwaka. Hii yote ni kwa sababu hatufanyi *promotion* za kutosha kwenye utalii wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana ya *National Parks* Tanzania tuna wanyama wengi. Ngedere wako hadi lkulu wanamsumbua Rais lakini kwa nini watalii hawaji Tanzania? Ni kwa sababu ya mipango yetu mibovu ya ku-promote utalii inasababisha tusipate watalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Balozi wetu wa China, shemeji yetu Mheshimiwa Kairuki anafanya kazi kubwa kwa ajili ya kuleta watalii katika nchi yetu. Watumieni Mabalozi wetu kutangaza utalii siyo Mabalozi wanakaa wanakunywa *wine* tu huko nje, watangaze utalii wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nilijaribu kuliongelea jana ni balaa la UKIMWI katika nchi yetu. Serikali yetu wameshindwa kubuni mikakati inayoendana na wakati

kwa ajili ya kupambana na vita dhidi ya UKIMWI. Matokeo yake kila siku iendayo kwa Mungu vijana 80 wanapata maambukizi ya UKIMWI wenyewe umri kuanzia 14 - 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari yake nini? Kwanza vijana hawa wako katika *foolish age*, wanaamini hawana cha kupoteza na hawana majukumu mazito. Kwa hiyo, sisi tunaposema Hapa Kazi Tu wao wanasema Hapa Zinaa Tu. Matokeo yake baada miaka 10 hatutakuwa na kina Tulia Ackson, Jenista Mhagama na Angella Kairuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali isipofanya mikakati ya dhati kwa ajili ya kutokomeza janga la UKIMWI tutakwisha. Jamii imesahau kabisa kama janga hili bado lipo na ugonjwa huu hauna dawa. Zamani Serikali ilikuwa na mikakati, katika vituo vyetu vya radio ilikuwa kila baada ya matangazo fulani kunakuwa na tangazo la UKIMWI lakini sasa hivi hamna hata *TBC* yenyewe ukisikiliza unaweza ukakaa siku nzima usione tangazo la UKIMWI. Matokeo yake redio na televisheni zimekuwa ndiyo kwanza vyanzo vya *ku-promote* ngono na mapenzi. Sasa hivi kila redio kubwa na ndogo ukisikiliza usiku wana-*promote* mambo ya ngono.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitandao ya kijamii, sasa hivi kuna ma-*groupya* *WhatsApp* ya ngono, *Instagram* wana-*promote* ngono, watu tunajiuza hadharani lakini Serikali imekaa kimya wanasema wanapambana na vita dhidi ya UKIMWI, mnchapambanaje?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha kwanza. Nitaje majina ya

Wabunge wachache tutakaoanza nao mchana. Mheshimiwa Dua William Nkurua, Mheshimiwa Fakharia Shomar, Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa Jesca Kishoa, Mheshimiwa Fatma Taofiq, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni ambao hawakupata fursa asubuhi. Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Leah Komanya ambao ni watoto wake pamoja na kaka yake ambaye ni Ndugu Emmanuel Komanya kutoka Kahama Mjini. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni walioko Bungeni kwa ajili ya mafunzo; kundi la kwanza ni wanafunzi 90 kutoka Chuo Kikuu cha Iringa kilichopo Iringa Mjini wanaosoma Kozi ya Biashara na Ualimu wakiongozwa na Ndugu Yohana Tweve. Karibuni sana vijana wetu, tunaamini kuwepo kwenu chuoni kunawaongezea maarifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunao wanafunzi 60 na walimu 4 kutoka Shule ya Sekondari Samaga iliyopo Tunduma mkoani Songwe. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha kwanza. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni leo.

(*Saa 7.10 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 Jioni*)

(*Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae!

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano tutaanza na Mheshimiwa Dua William Nkurua atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar, Mheshimiwa Leah J. Komanya ajiandae.

**MHE. WILLIAM D. NKURUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuweza kutoa mchango

wangu wa mawazo katika bajeti hii. Awali ya yote nitoe shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kuweza kutekeleza ahadi kubwa na muhimu kwa wananchi wangu wa Nanyumbu hasa Kata ya Mikangaula na Kijiji cha Mikangaula kwa sababu Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Kikwete alitoa ahadi ya kituo cha afya pale Mikangaula. Nami kama mwakilishi wao wananchi nilikuwa naendelea kuwasiliana na Serikali kuhakikisha kwamba ahadi inatimia. Hatimaye kwenye bajeti hii tumeshatengewa fedha kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuanza ujenzi huo wa kituo cha afya. Kwa niaba ya wananchi wale natoa shukrani za dhati kwa Serikali yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge nami nimeona niweze kuchangia eneo moja tu la kusisitiza namna ya kukusanya mapato ili Serikali yetu iweze kuwa na uwezo wa kuweza kutoa huduma kwa jamii. Eneo lenyewe ni namna ya kulinda vyanzo vyetu vya mapato. Hapa nakwenda kukiangalia chanzo cha ajira kwa sababu watumishi wanaaoajiriwa na Serikali na kampuni za watu binafsi pia wanachangia katika kulipa kodi ya Serikali. Sasa ni vizuri Serikali ikawa makini kuhakikisha kwamba hao watu ambao wanaajiriwa wanalindwa ili wasipotee kwa sababu wakipotea Serikali inakuwa imepoteza mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutoa mfano mdogo tu ambao naomba Mheshimiwa Waziri auzingatie. Wakati natunga Sheria ya *TASAC* hapa, Sheria ile ilikwenda kuwaondoa watu wanaitwa watu wa *tallying*. Watu wa *tallying* ni kama mashuhuda wa mwenye mzigo, mwenye mzigo akiwa nje akileta mzigo wake hapa anataka watu anaowaamini yeye wauthibitishe kama mzigo kabla haujapokelewa na bandari kama umekuja kama alivyoagiza yeye. Pia kama kuna mzigo unaondoka Tanzania kwenda nje labda majani ya chai, anataka mtu anayemwamini yeye akaungalie mzigo kama ni kweli ndiyo unaopakiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumekwenda kuwaondoa mashuhuda hawa ambao watu wa nje wanapenda kuwaamini. Sasa hii kitu ina athari nydingi, kwanza tunaondoa ajira lakini pili tunakwenda kupoteza kodi ambayo Serikali ingeweza kupata, tatu llani yetu ya Chama cha Mapinduzi ilikuwa imeahidi kuhakikisha kwamba tunaongeza ajira. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nishauri Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba suala hili la *TASAC*, kitendo cha kuwaondoa watu wa *tallying* tunakwenda kufanya makosa makubwa ambayo yataathiri maeneo mengi na makubwa. Kwa hiyo naomba atakapokuja hapa aangalie uwezekano wa kuleta mapendekezo ya kubadilisha sheria ili itakapofika mwezi Julai kama ambavyo wamewaaahidi wasije wakawaondoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakwenda kuangalia kule jimboni kwangu na kutoa ushauri mchache, naanza kwenye suala la umeme, umeme Nanyumbu ni shida; Nanyumbu ina umeme usiozidi asilimia 30 ya vijiji vyote ambavyo vina umeme. Nanyumbu tulipata umeme kwa mpango maalum wa Serikali laini *REA* / Nanyumbu haikupatikana, *REA* // haikupatikana, *REA* /// tukapata vijiji 13. Kwa hiyo, nashauri Serikali inapoona kuna wilaya au eneo ambalo limekosa umeme kwa kiasi kikubwa basi tunapokwenda kugawa huu umeme watu kama hawa wanatakiwa wapate zaidi kuliko wale wengine. Kwa sababu kuna watu wana asilimia 90 ya vijiji vyao, kuna watu wana asilimia 80 lakini Nanyumbu ina chini ya asilimia 30. Kwa hiyo, nilitegemea bajeti iliyopita tungepata vijiji vingi, kwa hiyo, leo nakwenda kuunga mkono hii bajeti lakini nataka nione kwamba vijiji vyangu vingi vinapata umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano ukija Makao Makuu ya Wilaya ya Nanyumbu pale Mangaka ukitembea mita 20 nje ya barabara hakuna umeme. Kuna Kitongoji kimoja kinaitwa Mchangani, kama Mbunge naona aibu kupita kule kwa sababu ni mjini pale pale hakuna umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba hawa watu wanapoanza kushuhulikia haya mambo wahakikishe kwamba maeneo makubwa kama Makao Makuu ya Wilaya tuhakikishe umeme unapatikana. Kuna wilaya zina umeme wa kutosha kwa nini Nanyumbu iwe hivyo. Kwa hiyo, napendekeza *TANESCO* wapewe uwezo wa kuweza kukabiliana na hili eneo langu la Nanyumbu ili wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu wapate umeme, wasiwe watu wa kulalamika kwa sababu sasa wanajisikia vibaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maji yanayotumika pale Mangaka yanatoka kwenye Kijiji kimoja kinaitwa Mara, ni kilomita kama nane kutoka Makao Makuu ya Wilaya. Yale maji tunatumia jenereta laini umeme upo kilomita nane, sasa jenereta zinaharibika wananchi wanakosa maji lakini hata hivyo gharama za uendeshaji ni kubwa, maji yanauzwa kwa bei kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kwenye bajeti hii umeme upelekwe haraka pale kwenye chanzo cha maji ili wananchi waweze kupata maji kwa bei nafuu lakini pia kwa uhakika. Umeme uliotoka Mangaka kuelekea Tunduru hapo katikati pana vijiji vingi sana lakini umeme umeteremka Kijiji cha Mnazi Mmoja pale Michiga peke yake, lakini vijiji vyote vya njiani vimekosa umeme laini kubwa zipo lakini umeme umekosekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri na kuomba Serikali kabla hatujaanza kutoa vijiji vingine tuhakikishe vijiji hivi ambavyo vinapitiwa na laini kubwa vinapata umeme. Kwa mfano Likokola ni Makao Makuu ya Kata hakuna umeme, pana zahanati; Lumesule Makao Makuu ya Kata hakuna umeme lakini pana zahanati. Kwa hiyo, naomba tuvipatie umeme vijiji hivi ili wananchi hawa nao wapate umeme kwa sababu umeme ndiyo maendeleo bila umeme kimsingi huwezi kuwa na maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka nilichangie ni *TARURA*, *TARURA* hao ukiwachunguza matatizo yao wana fedha ndogo sana. Wilaya yangu haipati zaidi ya

milioni 800 ukilinganisha na ukubwa wa barabara ambazo zipo Nanyumbu hii kitu hawawezi kukabiliana nayo. Kwa hiyo, wananchi wanakuja kuliaamu Serikali, wananchi wanakuja kukilaamu hiki chombo cha *TARURA* hata *sometimes* Madiwani kwa sababu bado wananchi hawajaelewa vizuri huu mtenganiko. Kwa hiyo, Madiwani wanapata lawama ambayo siyo yao, sasa naomba sana tuongeze fedha kwa hizi barabara za vijiji lakini pia hata hiyo fedha ndogo ambayo tunawapa kuna tabia ambayo ipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watendaji hawa wa *TARURA* wa Ofisi Kuu Mkao Makuu *TARURA* wanatenga labda milioni 800 Nanyumbu, lakini baadaye wakati Nanyumbu imeshingia mikataba ya kutengeneza ile barabara *TARURA* wanawaandikia barua kwamba sasa mtatumia milioni 600. Sasa hawa wameshaingia mikataba, kwa hiyo tunasababisha mgogoro kati ya *TARURA* na wakandarasi, tunasababisha mgogoro kati ya *TARURA* na Madiwani na wananchi hatimaye Serikali yote inakuwa imepata lawama ambazo siyo za msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba sana Serikali tunapotenga hata hicho kidogo ambacho tumekisema kiende, kwa sababu unaposema kisiende wakati wameingia mikataba ni hatara sana. Tunaweza kusababisha hata kushtakiwa na hao wakandarasi, nashukuru sana wakandara wanakuwa wastaarabu lakini kimsingi wanaweza wakatuchoko. Hilo suala naomba sana Serikali iliangalie kwa makini ili tusije tukasababisha migogoro ambayo kimsingi tunaweza tukaiepuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo sikutaka niongee mengi ila nirudi tena kwenye swali langu la mwisho kabisa la umeme. Nanyumbu kama nilivyo sema tupo chini sana, ninaunga mkono bajeti hii nihakikishe kwamba Nanyumbu kwenye umeme tutakuwa tume pata vijiji vingi kwa sababu ya *nature* ya tulikotoka Tulisahauliwa, kwa hiyo tukipendelewa ni sahihi siyo Nanyumbu peke yake, wale wote walioachwa nyuma waki piwa mwingi awamu hii ni halali yao kwa sababu kuna watu wana vijiji vingi sana. Hilo suala naomba sana

Serikali katika awamu hii, na naunga mkono hoja hapa ya bajeti kwa matumaini hayo Mheshimiwa Dkt. Mpango. Nahakikisha kwamba tunaunga mkono bajeti lakini ikatimize haya ambayo wananchi wanategemea wayaone. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana muda wangu nimeutumia vizuri naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Fakharia Shomar atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa Fatma Toufiq ajiandae. Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa Fatma Toufiq, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Kishoa, Mheshimiwa Emmanuel Papian John ajiandae.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hii hoja iliyopo mbele yetu lakini pia sambamba na hilo naomba nichukue fursa kuungana na wenzangu wote kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango, Naibu Waziri Dkt. Ashatu, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Ndugu zangu pamoja na maneno yote naomba muendelee kuchapa kazi kwa sababu kazi mnayoifanya inaonekana. Naomba niwatie shime kwa hilo kwa hiyo msikate tamaa maisha ni mapambano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia ukurasa wa 31 hadi ukurasa wa 33 wa hotuba hii mmezungumzia kuhusu vipaumbele ambavyo vimewekwa. Naomba nipongeze sana Serikali na Wizara kwa ujumla kwa kuweka vipaumbele hivi na hasa kwenye suala zima la vipaumbele vya kilimo na viwanda. Juhudi zinaonekana pamoja na ufinyu wa bajeti lakini Serikali inajitahidi sana. Niipongeze tena Serikali kwa kuwa na hii *programya* kuendeleza kilimo ya ASDP II. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo nina ushauri, kwamba Serikali imejipanga kujaribu kuona jinsi gani pembejeo zinaweza zikapatikana na kadhalika, lakini bado naomba nisitisize suala la wataalam. Kwa kweli suala

la wataalam bado wataalam hawatoshelezi, huku katika maeneo ya kata na vijiji ambako ndiyo wako wakulima zaidi kwa kweli wataalam hawako wa kutosha. Kwa hiyo utakuta kwamba wanalima mazao bila kufuata zile taratibu za kitaalam, kwa hiyo, nilikuwa nijombe Serikali yangu tukufu waone umuhimu sasa wa kuona jinsi gani wataalam zaidi wanaweza kupatikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo wataalam hawa inabidi waandaliwe kuanzia katika shule za msingi ili watoto waone kwamba kilimo ni sehemu ya ajira na wasione kwamba kilimo ni adhabu. Kwa hiyo, kama wakitengenezwa kuanzia katika ngazi ya chini, naamini kabisa tutaweza kupata watalaam wengi zaidi. Ni ukweli usiopingika kwamba, kwa kuwa Tanzania yetu inakwenda kwenye uchumi wa viwanda suala la malighafi lazima lipatikane, na hizi malighafi lazima zipatikane humuhumu nchini ili kusudi wananchi wetu na wakulima wetu wawzeze kupata tija. Kwa hiyo, bado niendelee kushauri kwamba upo umuhimu kabisa wa kuhakikisha kwamba bajeti ya kutosha inapangwa hasa kuhakikisha kwamba wataalam wanapatikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuhimiza mapinduzi ya viwanda lakini bado tunategemea kilimo cha mvua, na wenzangu wengi wamelizungumza hili kwamba hakika itabidi lazima tufanye mkakati wa uhakika wa kuhakikisha kwamba kilimo kinakuwa ni kilimo cha umwagiliaji badala ya kilimo cha mvua. Tumeona hivi karibuni jinsi gani mvua ambavyo zimechelewa na jinsi gani mazao yalivyoathirika, kwa hiyo, nitoe shime kwamba tuone kwamba suala la kilimo cha umwagiliaji kipewe kipaumbele ili kusudi sasa tuweze kupata zile malighafi kwa ajili ya kulisha hivyo viwanda vyetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala la uendelezaji wa suala la zao la zabibu. Niendelee kuipongeza Serikali suala zima la kupunguza ile bei ya mchuzi wa zabibu lakini bado ilikuwa ili kuliongezea hili zao la zabibu thamani isiwe ni mvinyo tu, lakini zipatikana bidhaa nyingine

zinazotokana na zabibu mfano *juice*, pengine *jam* na mazao mengine ambayo yatatokana kutokana na hii zabibu. Kwa hiyo, tuhamasishe uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo na hasa kwa wanawake ili kusudi waweze kutengeneza hizi bidhaa mbalimbali ambazo zinatokana na zabibu na ikiwezekana wapewe fursa ya kutengeneza mchuzi wa zabibu hatimaye waweze kuuza katika hivi viwanda vikubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, zabibu hizi zinaweza zikakaushwa. Zikakaushwa zabibu naamini kabisa zitaleta sana tija kwa nchi yetu hasa Mkoa wa Dodoma kwa wakazi na wakulima wa Mkoa wa Dodoma. Kwa sababu zabibu kavu nazo zina soko zuri sana na zabibu hizi zinaweza zikailetea pato Taifa letu. Kwa sababu inaonekana kabisa kwamba zabibu hizi nyingi hazitengenezwi hapa *Instead* zinaagizwa kutoka nje. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, zabibu za kukausha basi Serikali ione tunawezaje kupata mitambo ya kutosha ili kusudi sasa wananchi wetu waweze kukausha hizi zabibu na hatimaye Serikali yetu iweze kupata pato la kutosha. Sambamba na hilo, suala zima la zabibu za mezani. Zabibu ambazo zilizopo kwa mfano katika Mkoa wa Dodoma bado zabibu za mezani hazijawenza kupatiwa pembejeo za kutosha. Kwa hiyo, basi nione kwamba Serikali nayo ione kwamba kwenye hili suala la zabibu za mezani nazo ziweze kupatikana ili kusudi tuepuke kuagiza kutoka nje tuweze kuongeza pato letu la ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusiana na Benki ya Kilimo, naipongeza sana Serikali kwa kuanzisha benki hii. Hata hivyo, bado nitoe shime kwamba benki hii iongezewe mtaji na Serikali ili kusudi wananchi wengi zaidi waweze kufaidika na hii Benki ya Kilimo mwisho wa siku wananchi waweze kupata tija. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilikuwa nataka nizungumzie Serikali ione utaratibu wa kuweza kuweka *reserve*

ya maji ili maji haya yaweze kutumika kipindi cha kiangazi hasa katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie kuhusu vifungashio au mifuko ambayo inatumika kwa ajili ya kuweka mazao. Kuna ile mifuko ya kawaida lakini kuna ile mifuko ambayo mazao yakiwekwa mazao yale yanaweza yakakaa kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba niitie shime Serikali kwa sababu wakulima wengi sana kwanza hawana taarifa kuhusu hii mifuko ambayo ni bora zaidi lakini sambamba na hilo mifuko hii ni bei ghali sana kwamba mfuko mmoja unafika mpaka shilingi 5,000. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ione umuhimu sasa au wa kupunguza VAT, au wa kuona jinsi gani mifuko hii inapunguziwa bei ili mwisho wa siku wakulima wote waweze kupata tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie kuhusuana na suala la taulo za kike, taulo za kike kwa sababu wenzangu wengi sana wamelizungumzia na hii iko katika ukurasa wa 38. Pamoja na Serikali kutoa ule msamaha wa kodi ile ya VAT, nilikuwa naomba niishauri Serikali hebu kuona ni jinsi gani kama ikiwezekana tuweze kuweka bei elekezi, bei ambayo itakuwa ni *affordable*. Kwamba kila mtu au kila mtoto wa kike anaweza akai-*afford* hiyo taulo ya kike, lakini sambamba na hilo kwa kuwa kuna vifaa ambavyo vinatumika kwa ajili ya kutengeneza hizi *pad*, basi ufanyike utaratibu wa kutengeneza *reusable pads*. Nakumbuka wakati ule sisi tunasoma tulikuwa tunafundishwa jinsi ya kutengeneza *reusable pads* ili kusudi watoto hawa waweze kuzitumia. Kwa hili suala la *reusable pads* pia linawezekana ili kusudi watoto waweze kuwa na taulo kwa wakati wote bila matatizo yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba naomba nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa kutoa ile miezi sita ya uanzishaji biashara, kwamba ile *grace period*. Kwa kweli hii Serikali imefanya jambo zuri sana kwani hii itasaidia sana wafanyabiashara na itasaidia baadhi ya wafanyabiashara kuanzisha biashara zao na hivyo kufanya

suala la kukwepa kodi likapungua. Kwa hiyo, lakini naomba nitoe rai kwa wakadiriaji hili Mheshimiwa Mpango pamoja na kuandika kwenye hotuba yako basi hawa wakadiriaji pia wawe *fair* sana wasiwe wanafanya kwa ajili ya kukomoa wafanyabiashara. Kwa sababu mfanyabiashara pamoja na Serikali ni marafiki na huo urafiki inabidi lazima uendelee kwa sababu tunategemeana wote, mfanyabiashara pamoja na Serikali. Serikali inategemea kodi ya mfanyabiashara na mfanyabiashara nae anategemea Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nipongeze pia suala la dawati la malalamiko la ukadiriaji wa kodi. Niipongeze sana Serikali kwa jambo hili kwa sababu hii itasaidia sasa wafanyabiashara wengi kwenda kutoa malalamiko yako na hatimaye kuweza kupatiwa ufumbuzi. Nishukuru sana kwa kunipa fursa, naomba niendelee kuiunga mkono hoja. Ahsante sana, ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Roman Selasini atachangia kwa dakika tisa na atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Papian John, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ajiandae.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie kwenye bajeti hii ya Serikali. Ningetaka niseme tu tangu mwanzo kwamba hii siyo bajeti ya Mheshimiwa Dkt. Mpango na mtani wangu Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Ashatu, hii ni bajeti ya Serikali. Bahati mbaya sana Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa sababu ni Waziri anapokea hayo madongo na namjua ni mtu mnyenyeketu anayapokea pia kwa shukrani, kwa hiyo, mzee pokea tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niseme ninaunga mkono sera ya Serikali ya viwanda na kama Mheshimiwa Mlinga angekuwepo aoneshe llani ya CHADEMA angeona kwamba vilevile hiyo sera ipo. Kwa sababu ni mapinduzi ya viwanda yatakayotusaidia kusonga mbele katika nchi hii. Ningependa nitoe ushauri kuhusiana na jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningesema kwamba basi Serikali ijitahidi kabla haijahamasisha au sambamba na uhamasishaji wa viwanda vipyta, ifufue vile viwanda vya zamani vilivyojengwa na Serikali ya Awamu ya Kwanza chini ya Mwalimu Nyerere na kama mtakumbuka, Mwalimu alijenga viwanda karibu katika kila mkoa, kanda na alijenga viwanda kwa ajili ya kuyapa mazao yetu thamani. Tanga alijenga viwanda vya nyuzi, nguo, katani na viwanda vya magunia na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda hivi vilikuwa vimesambaa maeneo mengi katika nchi yetu, kwa mfano, pale Moshi kulikuwa na Kiwanda cha *Machine Tools*, Kiwanda cha Magunia, Kiwanda cha *Plywood*, *Kibo Match*, *Coffee Curing*, *Moshi Textile*, Kiwanda cha Pipi, Kiwanda cha Dawa za Mimea, *Pharmaceutical Industry*, *Plastic Court*, *ICC Meal Café*, Kiwanda cha Bidhaa za Misitu na *Kibo Paper*, vyote hivi vimekufa. Sasa tunahangaika kufungua viwanda vingine lakini viwanda hivi ambavyo vilianzishwa vingine kwa kodi za wananchi na utaalim na wataalam wenyewe wapo tunaviacha tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nashauri hivi kwamba Serikali iamue kwa makusudi mazima kama ilivyoamua kuchukua mashamba pori vile viwanda ambavyo vilibinafsishwa na wale wawekezaji hawakuviendeleta kadri ya mkataba, Serikali ichukue vile viwanda, itafutie Vyama vya Ushirika au labda wananchi amba wana uwezo wa kuendesha hivi viwanda waendeshe hivi viwanda kwa sababu hivi viwanda ni mali yetu na vilianzishwa kwa kodi zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu vilevile napendekeza sambamba na hili tuhakikishe kwamba tunarejesha imani ya wawekezaji kwa sababu ni kujidanganya kusema kwamba sisi wenyewe tuna uwezo wa kuanzisha viwanda wenyewe tu hapa ndani. Sisi tuko katika dunia ambayo imegeuka kuwa kijiji. Sasa katika hilo ningependekeza sasa Waziri Mheshimiwa Dkt. Mpango hapa pamoja na timu yake waangalie kodi zetu katika mambo mbalimbali. Wizara ya

Ardhi iangalie namna ambavyo wawekezaji wanakuja hapa kupata maeneo ya kuanzisha viwanda kwa urahisi. Halafu na hawa viongozi wetu watu wazima, waangalie namna ya kuongea, kuwapa semina hawa viongozi vijana ili waangalie lugha ya kuongea na wawekezaji, vinginevyo mwekezaji mmoja akisumbuliwa hapa, akienda nje matokeo yake anaenda kuharibu *image* ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, ningesema haiwezekani suala la uanzishaji wa viwanda likabaki kwenye Wizara ya Viwanda peke yake, vinginevyo mtawatumbua Mawaziri wa Viwanda kila uchao. Ningeshauri iundwe timu, Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda, Wizara ya Uwekezaji, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Ardhi na Wizara ya Mambo ya Nje kuangalia namna bora ya kuhamasisha wawekezaji kuja kuwekeza. Wizara ya Mambo ya Nje ina mchangano mkubwa sana kwa sababu yenye ndiyo inayoliiza Taifa nje. Sasa kama Wizara ya Mambo ya Nje haitachukua *lead*, tukasema tunaachia Wizara ya Viwanda, kuna mahali tutashindwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo sitazungumza mengi. Naomba ushauri unaotolewa na Wabunge kuhusu Kilimo ufuatwe kwa sababu wananchi katika maeneo yote wanahangaika. Kilimanjaro ilikuwa mzalishaji mzuri sana wa kahawa aina ya *arabica* lakini sasa hivi imekwenda na maji. Wakulima wanang'oa kahawa, wanapanda vitu vingine. Sasa tujiulize tumekosea wapi, tuwasaidie, kama ni pembejeo, kama ni masoko, kama ni utafiti tuwasaidie kwa sababu asilimia 75 ya Watanzania ni wazi wamejajiri katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza ni hili la *pads*. Nashangaa akisimama Mbunge mwanamke katika Bunge hili kuunga mkono hili pendekezo la Serikali halafu hatoi *solution*, nashangaa sana kwa sababu ni *TWPG* pamoja na wanawake wote humu ndani walileta hilo pendekezo katika Bunge liliopita. Sasa ni kweli hilo pendekezo halikuweza kuzaa matunda, lakini tuache hivi na kama kuna mtu ana

mtoto wa kike na yuko karibu naye anaafuatilia, atagundua mtoto wa kike akipewa mtihani wakati wa zile siku lazima atayumba. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nasema hivi; sisi katika Kamati yetu ya Utawala tulishatoa agizo kwa Halmashauri zote kwamba hatuwezi tukaongea nao katika bajeti ijayo kama Mkurugenzi hatatuambia kwamba amenunua hizo pedi na kugawa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuliwapa utaratibu, tulisema kwamba ni lazima kila shule iwe na choo kizuri, iwe na chumba ambacho kitakuwa na sehemu ya kuhifadhi hizo pedi, iwe na *dustbin* ya kutupia na kadhalika. Sasa Wabunge wanawake nendeni kwa mtindo huo, kwa sababu sisi hatuwezi, wale watoto wanateseka. Watoto katika karne hii wa Kitanzania wanatembea na makanga machafu, wanajihifadhi kwa majani na kadhalika, halafu mtu anasimama hapa anasema hakuna cha bure! Sisi hatusemi mtoto wa Selasini apewe, sisi tunasema watoto wa maskini wapewe na kwa sababu wote wapo kwenye shule moja, basi watoto wanazipata pale shulenii na wala sio nyumbani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshangaa mtu anasema kwamba anaweza akapewa akampelekea mama yake, kwanza akimpelekea mama yake *so what?* Si amesaidia, lakini vinginevyo, hili sio suala la kuzungumza. Naomba Mheshimiwa Waziri akae na Mwenyekiti wa Kamati ya TAMISEMI, sisi hili agizo tulishalitoa na katika Kamati yetu walipokuja katika Bunge hili kuna Halmashauri zilikuwa zinatupa ripoti kwamba sisi tumeshatekeleza *by half*, sisi tumeshatekeleza asilimia 100. Kwa hiyo kama hili la kodi linawashinda, tuchukue hili lingine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningetaka niliseme kwa haraka haraka ni kuhusu *TARURA*, uamuzi tuliofanya wa *TARURA* ulikuwa uamuzi mzuri, lakini *TARURA* haina pesa na kwa sababu hiyo haiwezi kutekelezea miradi yake vizuri. Mwaka 2018/2019 katika Jimbo langu bajeti

ilikuwa shilingi milioni 850, zimeenda shilingi milioni 550, wameweza kufanya miradi minne tu. Safari hii wamewaambia *ceiling* ni shilingi milioni 700. Wameniambia hawawezi kumaliza miradi viporo na wakafanya hata mradi mmoja.

Kwa hiyo, pamoja na kwamba najua kuna mikoa ambayo haijaunganishwa bado na lami kwa mfano Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Katavi, hilo jambo linaweza likafanyika, lakini kwenye bajeti ijayo waangalie namna ile *Road Fund* kuigawa labda *TARURA half* na *TANROADS half* baada ya kumaliza kuunganisha ile mikoa mingine ambayo bado haijaunganishwa, kwa sababu kwa mfano jimbo langu, ukanda wa juu wote ambao una *volcanic soil*, una mawe makubwa sana, *TARURA* hawawezi kufanya hiyo kazi. Kwa hiyo naomba hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi barabara ni muhimu sana, tunaweza tukajenga reli, tukajenga barabara za lami, sasa hizi *feeder roads* kama hazitajengwa ni shida na tulishawaaminisha wananchi wetu kwamba halmashauri inajenga. Kwa hiyo Madiwani na Wabunge wanalamikiwa kumbe kuna chombo kinaitwa *TARURA* ambacho kinajenga...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana, umeonesha mfano mzuri sana, lakini umeshamaliza dakika kumi sasa hata niliyokuongeza umemaliza. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nadhani mtakubaliana na mimi *Chief Whip* leo ameonesha mwongozo mzuri sana wa namna ya kuchangia bajeti ya Serikali. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamuita Mheshimiwa Emmanuel Papian John, atafuatiwa na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwanza kwa kunipa nafasi na napongeza Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa maana ya namna ambavyo imekuja na inavyokidhi mahitaji yetu na kwa namna ambavyo mapunguzo mengi ya kodi na uititiri wa kodi nyingi kwa Watanzania ambavyo zimeondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema juu ya viwanda, lakini niongezee pale kwa Mheshimiwa Selasini kwamba wakati tunafikiria kuchukua hivi viwanda kuvitaifisha, zipo benki zetu zilikopesha hivi viwanda kwa miaka kadhaa na zile pesa ziko huko na ni za Watanzania ambaao wali-*inject* pesa zao kwenye zile benki zikatunzwa. Tutakapokwenda kutaifisha hivyo viwanda kwa ule utaratibu mzima wa kuondoka na watu wa Biashara na Viwanda watu wa Wizara ya Fedha, watu wa TAMISEMI na ule mnyororo mzima wa kwenda kuhakikisha kwamba vile viwanda vinarudi Serikalini, basi mimi nataka tuongezee kwamba tuondoke na wale watu wa benki zetu wanaokopesha wakae chini na *document* zao, wahakikishe wanaona chao kiko wapi na mwisho wa siku Serikali itakapochukua mamlaka ya kuvitaifisha basi na zile benki zetu ziweze kuokolewa kwa sababu tukivitaifisha na pesa za benki zilizokopesha pale ziko kule tayari ni kwamba tumesababisha benki zetu kuanguka. (*Makofii*)

Sasa naomba nifikirie wakati mnakwenda muongozane na hizo benki zilizokopesha ili kuweza kuokoa chao kwa sababu tayari kama mtu ameshakufa ni lazima tujue nani anadaiwa na nani alikuwa anadai ili marehemu aondoke salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema juu ya hivyo viwanda, leo tunajenga viwanda Tanzania lakini kuna jambo moja nimeanza kuligundua kwamba inawezekana ikatufikisha pagumu. Naomba Serikali ifanye jambo moja la utafiti wa kina na ijiridhishe kwamba kuna nchi ndani ya *East Africa* sasa baada ya kuona Tanzania inajenga viwanda ikifika saa 5 usiku inashusha *half price* ya umeme ili viwanda viweze

ku-produce na ile *raw material* na zile *product* zote ziweze ku-compete na bidhaa za viwanda vyetu hapa Tanzania. Serikali ilichunguze, ilifanyie kazi kwa haraka, ipunguze michakato, isijadili mara nyingi ili kuokoa viwanda vyetu tunavyovijenga sasa ili viweze kubaki salama. Vinginevyo zile *products* za hivyo viwanda zikiingia hapa ye ye atakachofanya ataondolewa kodi, atapunguza kodi, atacompete na viwanda vya hapa, *under that competition management* ya ku-manage hilo soko itakuwa kwenye competitive na hizo nchi hatutakuwa tuna-benefit kitu na mwisho wa siku viwanda vyetu vinaweza ku-collapse. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze juu ya ardhi; kodi ya ardhi mimi naona kama inakuwa kubwa. Kodi ya ardhi kwenye *Investment* za mashamba makubwa, *ranches, industrial areas*, mambo mengi, naona kama kodi ya ardhi inakuwa kubwa. Naomba Serikali mliangalie hili na kwa *accumulation* ya madeni makubwa yaliyopo hebu ondoeni *penalty* na *interest* muone ni namna gani watu wanaweza ku-afford kulipa hizi *accumulated* madeni mengi ili watu waweze kukusanya na hiyo pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais amekuwa anaonesha mara nyingi, *waive interest, waive penalty* kwenye benki, *waive* kwenye kodi za Serikali, punguza haya mambo ili watu waweze kufanya kazi *otherwise* utakuwa unahesabu mabilioni ya pesa makubwa yaliyowekwa kwa wananchi ambayo ni *unaffordable* watu kulipa na badala yake mnaishia kuhesabu mabilioni ambayo hayawesi kulipika na mwisho wa siku mnaishia migogorio. *Waive* hii ku-simplify maisha ya watu, punguzeni hii ili watu waone namna gani ya kuweza kusonga mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi ya kimkakati kwenye Halmashauri zetu ambazo watu wamekuwa wana-apply wanatengeneza miradi ya kimkakati ambayo ni ya kuona ni namna gani hizo Halmashauri zetu zinaweza kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema tena, Waziri wa Fedha, hebu tufanye kazi kwa kufanya *analysis* kama una Halmashauri 50 au 100 zina *application* ofisini kwako, zimekuja zinaonesha miradi ya kimkakati, *turnover* ya mradi katika Halmashauri fulani inaonesha miaka mitano au kumi, lakini kuna Halmashauri uki-*implement* huo mradi *turnover* yake ku-*manage* huo mradi na kuleta *income* na kupunguza mzigo mkubwa kwa Serikali ndani ya mwaka mmoja, upi wa kuanza? Tengeneza kufata *track* hivi vitu kwa kuona namna gani *quick return of investment* uitumie hiyo itusaidie ku-*support* miradi hii. Leo Kiteto tuna mradi wa gulio, soko la mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri akitupa sisi zile pesa ambazo tumeomba kwenye soko letu la mradi ni kwamba sisi baada ya misimu mitatu tuna uwezo wa kuwa tunajitegemea kwenye Halmashauri yetu ambayo tunaweza kujitegemea hata kwa asilimia 80. Tukikupunguzia kukudai pesa za kutusaidia kama ruzuku kwa asilimia 80 ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto tumeokoa kitu kikubwa sana. Tusaidie tujenge, tutumie huo mud amfupi kurudisha hiyo pesa ambayo sisi tunajitegemea wenyewe ile pesa uliyokuwa unatuletea upeleke kwenye Halmashauri nyingine ambazo hazina miradi ya ku-*survive* na ku-*sustain* zenyewe, tutakuwa tumepunguza *burden* kwa Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo majengo kwenye Halmashauri zetu tunajenga. Mimi nimeona tunajenga majengo makubwa sana kwenye Halmashauri zetu. Hivi kwenye hizi Halmashauri zetu tuna haja gani ya kujenga Ofisi ya Mbunge kama haya majengo makubwa ya Halmashauri yapo! Mbunge mpe vyumba vivili aweke bendera yake pale, asonge mbele na wananchi wake, tupunguze kujenga, hizi pesa tuzipeleke kwenye shughuli nyingine ambazo zinaweza kusaidia kujenga madarasa yetu. Huo ni ushauri wangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye mikopo ya kilimo, mifugo na uvuvi; nataka kuiomba Serikali iangalie hivi sisi tunaona kwenye nchi nyingine wanakuwa na *grants*

kubwa zinazo-*support* miradi mingi kwa wananchi na mwisho wa siku hii miradi inapofanyika kwa mfano miradi ya maziwa, kuboresha wakulima, kufanya mambo ya kahawa, kuwapa mbegu za miche, korosho na kadhalika kuna *a lot of grants*, kwa nini Tanzania haziji? Hawa *donor friends/countries* wanao-*inject* hizi pesa na hii miradi mikubwa na kampuni kubwa zinazo-*support* hii kwa nini Tanzania hatuwaoni? Hebu jitahidini muwaone. Kama mnaona kwamba wachunguzeni muwaone, hizi *grants* zinapokuja zinasaidia wale wakulima wetu, wavuvi wetu, wafugaji wetu kufanya namna ambavyo inawezekana waweze ku-*survive then* wanapokuwa wana-*grow* ndipo unapoweza ku-*introduce* kiwanda kikapata *raw materials*, ndipo utakapokwenda ku-*introduce* kiwanda kikapata wanafanyakazi wengi, ndipo vijana wetu wasomi walioko mtaani watakapokimbilia. Ndiko Serikali itakapokwenda kukusanya kodi kesho kutwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *we are joking!* Hapa tunafanya utani Tanzania kwenye kilimo, mifugo na uvuvi, mfugaji ukimpa ng'ombe wawili wa maziwa au ng'ombe mmoja mwisho wa mwaka ukamwambia wewe nenda *TRA* kalipe kodi ya shilingi 100,000 hawezi ku-*feel* kama alikuwa analipa kodi, *it's just a peanuts*, lakini kwa nchi tunakuwa tumekusanya kitu kikubwa ambacho mwisho wa siku Serikali inapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nishauri, hebu angalieni hizi *grants* ziende kwa wananchi, zi-*supprt* ku-*uproot poverty* iliyopo, lakini pia iwe kama chachu na ku-*boost* vijana wetu wasomi wanaokimbria *SUA* wanaenda mtaani, mwisho wa siku wanaanza kusoma kompyuta, amesoma *animal science*, anaanza kusoma kompyuta, sijui *accountshuku* amesoma kilimo (*agri-business*), hiyo biashara ya nini? Hebu jaribu kuona namna gani tunaweza ku-*trigger* vijana wetu wakaenda kwenye *grassroots* kwenye sekta ya kilimo na mwisho wa siku tunapo-*push* hii inafanya benki zetu zianze kupunguza *risk* ya kukopesha hawa watu kwa sababu tayari mazingira yameshaandaliwa. Kwa hiyo unapomkopesha na anaona *end product* ya kiwanda ipo,

benki haiwezi kusita kujadili mkopo aliyeomba kwa mwananchi mkulima au mfugaji ili aweze kutoa hizo pesa na akaweza kufanya biashara wakati huo tukiendelea kukusanya kodi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niombe mwisho tunayo mazao makubw ya biashara kama kahawa, korosho, chai, pamba na kadhalika, leo tunahangaika kila ukifanya hivi inagoma, ukifanya hivi tunasumbuka wakati tuanfikiria kucheza na haya mazao dunia nzima inatuangalia sio sisi tunaolima haya mazao peke yake. Niombe kuwe kuna uwezo wa kufikiri na kuamua haraka. Uwezo wa kufikiri na kuamua kwa muda ili tuweze kwenda na wakati kwenye haya mazao. *The more you delay one month*, kahawa imeshuka bei, korosho imepigwa chini, pamba hainunuliki, soko limeanguka, nchi ina-shake, naomba Serikali *delayment* ya vikao vya michakato ya kutomaliza kwa wakati na kuamua jambo, Serikali iliangularie sana. Wakulima wetu watakufa, watateseka, watapoteza na hatutapata *income*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe inapotokea of anything katika business trend yoyote ile umeona kwamba soko la korosho katika mfumo wa kulinunua ime-shake hivi twist immediately, hamisha mzigo wa watu, lipa wakulima pumzika. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Lolesia Bukwimba atafuatiwa na Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, Mheshimiwa Juma Kombo Hamad ajiandae.

**MHE. LOLEIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa waliyoifanya. Bajeti hii ambayo umetuletea kwenye Bunge hili kwa kweli ni bajeti nzuri, ni bajeti ambayo imeweza kuangalia zile changamoto za wananchi na kuweza kuzifanyia kazi kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, ndiyo maana nitumie fursa hii kupongeza sana Wizara kwa kazi kubwa ambayo imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia vile vipaumbele vyat Serikali nilikuwa nikiangalia vipaumbele hivi katika ukurasa wa 31 na 32. Vipaumbele ambapo vumezungumziwa, kusema ukweli ni vipaumbele ambavyo ni muhimu kabisa, ambavyo vikitekelezwa nina imani kubwa kwamba nchi yetu ya Tanzania itaweza kupiga hatua kubwa katika suala la uchumi. Mimi binafsi nilikuwa nikiangalia katika kipaumbele namba tatu ambacho kimekusudia kuboresha mazingira wezeshi kwa ajili ya kuwezesha uchumi wetu kuweza kukua zaidi katika kuimarisha biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba maendeleo katika sekta hii ni muhimu sana kuweza kuboresha miundombinu muhimu. Pia Serikali imekusudia kupeleka fedha hizi katika kuendeleza maeneo mbalimbali ya kiuchumi, kwa mfano, reli na barabara. Kwa kweli ni maeneo muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nilikuwa naangalia sekta muhimu ya nishati. Nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuchukua uamuzi wa dhati kuwekeza fedha nyingi katika sekta hii ya nishati. Mwaka huu imeweza kutenga bajeti ya shilingi trilioni 2.1 ambayo imeongezeka kutoka bajeti iliyopita ya shilingi trioni 1.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, najua kabisa kwamba tukiwekeza kwenye nishati, mwisho wa siku tutaweza kufikia azma ya Tanzania ya viwanda. Hatuwezi kuwa na viwanda bila ya kuwa na umeme wa uhakika. Vilevile katika sekta hii ya nishati nilikuwa najaribu kuangalia,

Serikali imekusudia kuangalia vijiji vya Tanzania 1,990 kwa ajili ya kupelekewa umeme na bajeti imeongezeka kidogo kwa asilimia 26 kutoka kwenye bajeti ya mwaka 2018 ambayo ilikuwa ni shilingi bilioni 412, mwaka huu tumeweza kupangiwa bajeti kwenye nishati kwa upande wa *REA*, shilingi bilioni 423. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kwamba bajeti hii bado iko chini sana. Kwa sababu gani? Wote ni mashahidi, umeme ni muhimu sana katika kuchochaea maendeleo. Vijiji vingi vya Tanzania vinahitaji kupatiwa umeme wa *REA*. Ninasema hivyo kutokana na nini? Nimeona uzoefu, vijiji vingi vilivyopatiwa umeme kwenye Jimbo langu mwaka 2014, ni tofauti sana, yaani kiuchumi. Vimepanuka zaidi kiuchumi. Ni tofauti na vijiji ambavyo havina umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo sasa, pamoja na kwamba Serikali imekusudia kupeleka umeme kwenye vijiji 1,990, lakini bado ninaona vijiji hivi ni vichache sana, kwamba mpaka mwaka 2,020 mwezi Juni, vitakuwa vimefikiwa vijiji vya Tanzania nzima vijiji zaidi ya 10,000. Hata hivyo vijiji 10,000, ndani ya vijiji 12,000, tunaona bado kabisa Serikali inahitajika kuongeza fedha zaidi kwenye *REA* ili vijiji vingi vya Tanzania viweze kubahatika kupatiwa umeme. Vikipata umeme vijiji hivi, nina uhakika kwamba vitawezza kupanuka zaidi kiuchumi, kwa sababu watakuwa na uwezo wa kuanzisha hata viwanda vidogo, vikubwa na vya katii. (*Makafii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshuhudia wananchi wakianzisha viwanda vidogo na vya katii kwenye maeneo ambayo yana umeme. Kwa mfano, kwenye Sekta ya Madini ambako mimi natokea, ambako wananchi wanajishughulisha na shughuli za uchimbaji wa madini. Kwa hiyo, vijiji ambavyo vimepatiwa umeme vimeduwa na uwezo wa kuanzisha viwanda vidogo vya uchenjuaji dhahabu; vidogo, vya katii na vikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Wizara ya Fedha, hebu iangalie kuongeza umeme kwenye *REA* ili

vijiji vingi vya Tanzania viweze kupatiwa umeme huu ambao utawawezesha zaidi kuinua kipato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimejaribu kuangalia bajeti hii pia kwa upande wa barabara hasa kwenye upande wa *TARURA*, wote tunafahamu kwamba kuna mtandao mkubwa sana wa barabara, hasa za vijiji na mijini zenyetakribani urefu wa kilomita zaidi ya 100,000, lakini kwenye bajeti tumetengewa kwa ajili ya utengenezaji wa kilomita zaidi ya 21,000. Naona kwamba kwenye kilomita 100,000 tunatengeneza 21,000 tu, bado hizo kilomita ziko chini sana na wote tunafahamu kwamba barabara ndiyo injini ya uchumi. Kama hakuna barabara, maana yake ni kwamba kunakuwa hakuna maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa hasa ni vijiji ambako ndiko kuna changamoto kubwa. Barabara nyngi za *TARURA* ambazo zina changamoto kubwa hazipitiki. Kwa hiyo, naomba, pamoja na kwamba nimeangalia bajeti iliyotengwa, tena mwaka huu wamepunguza kuliko ile ya mwaka 2018. Nimeona wamepunguza, ya mwaka 2018 ilikuwa shilingi bilioni 243, lakini mwaka huu bajeti ya ni shilingi bilioni 224. Ninaona kwa kweli bajeti ni kidogo sana kwa upande wa *TARURA*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii sasa kuishauri Serikali inapofanya marekebisho kwenye bajeti sasa, iangalie hata kuwezesha, kuongeza kidogo bajeti kwenye *TARURA*. Hii itawezesha barabara za vijiji ziweze kuitika vizuri, ambako ndiko Watanzania wengi waliko. Wote tunafahamu zaidi ya asilimia 70 au tuseme kuanzia asilimia 60, 65, Watanzania wanaishi vijiji na ndiko ambako sasa shughuli nyngi za kiuchumi zinafanyika, ukisema ufugaji unafanyika kijiji mara nyngi; ukisema kilimo, kinafanyika vijiji, ukiangalia hata shughuli za uchimbaji wa madini ni vijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali hebu iangalie *TARURA*, iongeze bajeti ili hatimaye wananchi walio wengi waweze kufanya kazi zao vizuri, wasafirishe

mazao yao kutoka hatua moja kwenda sehemu nyingine, ili hatimaye sasa uchumi wetu wa Taifa uendelee kukua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nilikuwa naangalia pia katika kipaumbele namba mbili cha Serikali, ambapo kimekusudia kwa maeleo kwamba ni ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Naipongeza sana Serikali kwa sababu imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba uchumi unakua lakini pia na maendeleo ya watu yanakuwepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekusudia kufanya mambo makubwa sana. Kwa mfano, kwenye Sekta ya Afya, Serikali imekusudia kujenga hospitali nyingine 27, ambapo za mwaka 2018 zilikuwa Hospitali za Wilaya 67. Kwa hiyo, zimeongezeka zaidi. Napongeza kwa kweli kwa kazi kubwa ambayo Serikali imekusudia kuifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hivyo, Serikali inakusudia kujenga vituo vingine vya afya kama 52, jambo ambalo mimi binafsi nalipongeza kuona kwamba Serikali imekusudia kuleta mabadiliko ya kipekee katika Taifa letu la Tanzania hasa katika Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitumie fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu. Kwanza nimeletee salaam kutoka kwa wananchi wa Busanda, hasa kwa kutupatia Hospitali Katoro pale ambapo kumekuwa na changamoto ya siku nyingi, alipokuja kwenye maazimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika. Yeye mwenyewe amesema hospitali itajengwa na tayari anashughulikia suala la fedha ili ziweze kwenda kwa ajili ya kuanza kufanya shughuli za ujenzi wa hiyo Hospitali ya Katoro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi binafsi kwa niaba ya wananchi na wananchi wenyewe wamenituma nikupongeze kwa kweli kwa kazi hiyo na kwamba tuko tayari kuunga mkono Serikali kwa ajili ya shughuli zinazoendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa. Ahsante sana. Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad na Mheshimiwa Marwa Rioba Chacha ajiandae.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nami napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenjalia kusimama katika Bunge hili na kuungana na Wabunge wenzangu katika kujadili bajeti ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijafanya hivyo, naomba kwanza niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote katika Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, naomba niseme kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajadili bajeti ya mwaka 2019/2020, tunajadili Makadirio ya Mapato na Matumizi katika kipindi hicho cha 2019/2020, lakini tukiwa tunafanya hivyo, tumepitisha bajeti mbalimbali huko nyuma. Nimesimama hapa kwa ajili ya kutaka kumkumbusha Mheshimiwa Waziri, tukiwa tunataka kupiga hatua katika mwaka wa fedha huu 2019/2020, ni vizuri tukaangalia bajeti hizo za nyuma, ni mambo gani tuliyajadili hapa lakini hayakupata ufanisi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo mbalimbali ambayo tumeyajadili ikiwemo miradi ya maendeleo, lakini kwenye miradi ya maendeleo yako maeneo hatukufanya vizuri. Sasa ni jukumu letu kama Serikali, kujipima na kuona sasa tunapotaka kupita hatua, ni lazima tuangalie yale mambo ambayo tumeyapitisha huko nyuma na hayakufanya

vizuri. Kwa mfano, tulijadili masuala mbalimbali yanayohusu ujenzi wa madarasa, ujenzi wa zahanati na majengo mbalimbali ambapo wananchi wetu wamekuwa wakijitolea. Wamefanya hizo kazi lakini iko miradi mpaka hivi nilivyo simama hapa, bado hatujafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, ni vizuri tukajipima kwa kuangalia kile tulichokifanya. Kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu katika hiyo miradi yako maeneo mengine ambayo wananchi wetu wamekuwa wakidai fidia mbalimbali. Niseme tu, katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, yako maeneo ambayo wananchi wetu wamekuwa wakipisha miradi hiyo ifanyike na miradi hiyo imekuwa ikigusa makazi yao. Kwa mfano, tulikuwa tunatekeleza mradi wa barabara kwa kiwango cha lami, barabara ambayo illkuwa inaanzia Namtumbo – Kilimasela – Tunduru - Nakapanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza miradi hii wako wananchi ambao walitakiwa wapate fidia zao lakini mpaka hivi ninavyosema hawakupata fidia na ninaomba nieze, wananchi wale wako katika makundi yasiyopungua manne, naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize. Liko kundi la kwanza ambapo wananchi walilipwa fedha katika kutekeleza mradi ule wa barabara kwa kiwango cha lami, lakini walihisi kwamba wamepunjwa, Serikali ilitoa tamko kwamba hawasitahili kulipwa walichopata ni kile kile ambacho ni halali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lipo kundi la pili, wananchi walivunja nyumba kabla ya kupewa *notice*, Serikali ilisema kwa kuwa walivunja kwa hiari yao haiwezi kuwalipa. Liko kundi la tatu ambapo wananchi walipewa *notice*, kabla ya kufanyiwa tathmini walivunja nyumba zao. Serikali ilitoa tamko kwamba wangeweza kupata kifuta jasho au kifuta machozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo kundi lingine la nne ambalo mimi binafsi nimesimama hapa na linanisikitisha zaidi

na ninaomba Serikali ilifanyie kazi. Kundi hili, wananchi walifanyiwa tathmini, walipofanyiwa tathmini, walionekana kwamba wanastahili kulipwa na waliingia kwenye mpango wa kulipwa, lakini wakati wa malipo walirukwa. Sasa nimesimama katika kuwasemea hawa wananchi. Nafahamu tuko hapa, pamoja na kazi zote za Mbunge, lakini ni pamoja na kuwasemea wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia Serikali, kama wapo ambao wanastahili kulipwa basi walipwe. Kwa sababu kila siku wanapokuja kufuatilia, wakati mwingine wanaambiwa anayestahili kulipwa mmoja. Wakati mwingine wanaambiwa wanastahili kulipwa wawili, wakati mwingine wanaambiwa wote hamstahili kulipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, kwa sababu wale walikubali kufanya hivyo, nami nafahamu wakati tunatekeleza miradi ya maendeleo, iko miradi ambayo inategemea fedha za ndani, lakini iko miradi ambayo inategemea fedha za wafadhili. Katika fedha za wafadhili kunakuwa na masharti ambayo wanayaweka katika mikataba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia barabara hii wakati inajengwa, maelekezo ilikuwa kwamba suala la fidia ni suala la Serikali yenyewe, kwa maana ya mapato yetu ya ndani. Sasa kinachosikitisha zaidi, barabara hiyo tayari imeshafunguliwa. Mheshimiwa Rais bahati nzuri alitembelea kule kwetu karibuni, katika Mkoa wetu wa Ruvuma, alipokuja kule wananchi walijandaa pale kutaka kushika mabango, lakini viongozi wakawaambia msishike mabango, wakakubali wakaacha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba, kwa kuwa tunakusudia kupiga hatua, ni vuzuri tukaangalia viporo tulivyoviacha nyuma. Wananchi wangu wamekuwa wakilalamika, na siyo barabara hiyo tu, yako maeneo mengine wananchi wanapisha mashamba yao, wanaacha mashamba yao wanapisha Serikali miradi iendelee, lakini

mwisho wa siku wanahangaika kila siku maofisini, wanadai fidia zao na hawapati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, nami nimepata habari kwamba mionganoni mwa vitu ambavyo Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango havipendi ni kutokulipwa wananchi wetu. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, kama kweli tathmini imefanyika na wako ambao wanastahili kulipwa, basi ni vizuri jukumu la Serikali kuwalipa wale wananchi ili tuwatie moyo. Mwisho wa jambo hili ni mwanzo wa jambo lingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuongea hayo, kwa kweli nilisema kama sitaongea hayo inawezekana ningepoteza fahamu, kwa sababu nilikuwa na hamu kweli ya kuongea jambo hili kwenye Bunge ili lifanye utekelezaji na wananchi wale naamini watakuwa wanansikia, kwa sababu ndicho walichotuagiza tuje kuwasemea. Kuwasemea siyo tu kuhimiza miradi ya maendeleo, lakini kuwasemea pia na kuangalia kero zile ambazo wanazipata wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba nizungumzie suala la Halmashauri. Mimi kabla sijawa Mbunge, nimekuwa Diwani katika vipindi vinne kwenye Halmashauri. Naelewa vizuri sana masuala ya Halmashauri. Halmashauri zilizopo leo kwenye maeneo yetu ni tofauti na huko nyuma. Hali za Halmashauri zetu siyo nzuri. Tulifuta baadhi ya vyanzo vya mapato, tukawa tumeahidi kwamba Serikali itakuwa inafidia vile vyanzo. Kwa sasa ni kama haviendi kabisa. Kwa maeneo ambayo tunapeleka hivyo vyanzo, basi haviendi kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba vile vyanzo ndivyo ambavyo Halmashauri wanakaa wanapanga bajeti kupidia vile vyanzo. Wanaangalia miradi ya maendeleo. Kutopeleka fedha kwa wakati maana yake ni kuzifanya zile Halmashauri zizidi kudidimia na kutoendelea na ile miradi ambayo wameipanga kwenye Halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, sisi ni Wabunge, lakini tukiwa kwenye Halmashauri sisi pia ni Madiwani. Tunaona matatizo ambayo wanayapaya Madiwani wetu kwenye Halmashauri. Ziko Halmashauri, Diwani inafikia mpaka miezi kumi hajapata posho yake wala hajapata stahili yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linakatisha tamaa. Sisi tunakaa huku miezi mingi, lakini shughuli nydingi za kwenye Halmashauri wanafanya Madiwani wetu. Ni vizuri sasa Serikali ione uwezekano wa kupeleka fedha kwa wakati ikiwepo kuwatia moyo hao Madiwani nao wawe wanapata posho kama tunavyppata sisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme, sisi tunao utaratibu, ikifika siku ya Jumanne, mtu anaangalia kama kuna chochote kimeingia, Jumatano, Mbunge anaangalia kama kuna chochote kimeingia, lakini kama hakikingia tunaanza hapa; hatujapata, hatujapata, posho, hajatoka, hajatoka. Sasa kama jambo lile linakuuma wewe, lazima urudi umwangalie na mwenzio nyuma kwamba naye linamuumma. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumetangulia, tumesimama mbele lakini huko nyuma wako wenzetu wanaotufuata. Wanaotufuata ni pamoja na Madiwani. Kwa hiyo, nilikuwa nirombe Serikali, tuangalie Madiwani, hali zao siyo nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la Madiwani, walilingia hata kwenye bima za afya. Naomba nikwambie, ziko Halmashauri mpaka sasa zinashindwa kulipa hata bima za afya za wale Madiwani. Wanakwenda kutibiwa wanaambiwa bima yako haisomi. Sasa vitu kama hivi vinakatisha tamaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeyasema haya kwanza nikwa naamini kwamba mimi ni sehemu ya Madiwani. Pia kuna suala la mikopo, wamekopa ile mikopo, kwenye mabenki hawalipi. Sasa mwisho wa siku kile ambacho

walistahili kukipata hawatakipata na wanafanya hivyo siyo kwamba Wakurugenzi hawapendi kufanya, uwezo unashindikana, kwa sababu tulichukua vile vyanzo, lakini katika kuchukua vile vyanzo tuliahidi kwamba tatarudisha, hatupeleki kwa wakati, hali imekuwa ngumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona niyaseme haya na ninarudia tena mimi ni sehemu Madiwani, lakini yako mambo ambayo tunajadili kwenye Halmashauri kama hivyo nilivyosema miradi ya maendeleo, kama hatupeleki fedha kwa wakati ile miradi haiwezi kufanikiwa. Haiwezi kufanikiwa kabisa na Wabunge wenzangu wameyasema haya; zahanati, vituo vya afya, madarasa, na miradi mingine, wananchi wamefyatua tofali kwa nguvu zao, lakini leo tofali zimegeuka kuwa vichuguu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inatia huruma sana kama Serikali, kama Wawakilishi, wasingeweza kuja wote, sisi tumekuja kuwasemea. Naiomba Serikali yangu sikivu isikie maneno haya ninayoyasema hatimaye itekeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, atafuatiwa na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha na Mheshimiwa Shally Raymond, ajiandae.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na nimshukuru Mwenyezi Mungu nami kunipa fursa hii ya kupata kuchangia angalau mawili matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuja kufanya majumuisho, atujibu masuala au mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni mambo ambayo yamekuwa yakileta mkanganyiko na utata katika

taarifa mbalimbali ambazo zinatoka hususan kwenye vyombo vya habari na kwenye mitandao ya kijamii. Sasa ili tujiridhishe, naye kwa sababu ndiye msemaji wa Wizara ya Fedha, basi atakapokuja ana wajibu wa kutuweka wazi ili tujue kipi ni kipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni mgao wa Zanzibar kwenye mapato ya Muungano, kwa sababu kila siku tunapiga kelele hapa kwamba kuanzishwe *account* ya pamoja ya fedha ili suala hili lisiwe na utata. Ikianzishwa *account* ya pamoja ya fedha ina maana ni kusema kwamba mgao utakuja kwenye bajeti na itaonekana kwamba haya ndiyo makusanyo ya Muungano na huu ndiyo mgao kwamba Tanzania Bara ilipata hiki na Zanzibar ilipata hiki, kwa hiyo hilo ni suala la kwanza ambalo namuomba sana Waziri wa Fedha atakapokuja aje atujibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, ni hilo la mgao lakini sasa kupitia mikopo ya nje, kwamba suala la mikopo ya nje ni suala la Muungano sasa aje atuambie Tanzania, Mwaka 2018/2019 na 2019/2020 inategemea kukopa nini na ilikopa nini na Zanzibar ilipeleka nini. Ninachomuomba sana aje awe mweli kwa sababu ilitokea mwaka jana kusema katika ile *1.5 trillion* kuna bilioni kadhaa zilikwenda Zanzibar, baada ya kutamka hivyo Waziri wa Fedha wa kule akasema kwamba huku hakuna shilingi tano ambayo imekuja sasa utakapokuja Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Mpango uje utuambie uhalsia na ukweli ulivyo kwenye mikopo ya nje inayohusu Muungano, umekopa kiasi gani na Je, katika mkopo uliokopa ile *4.5 umeipeleka?* Uje utuambie na utuambie ukweli kabisa katika jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, jana Zanzibar kuliwasilishwa bajeti na katika bajeti iliyowasilishwa Zanzibar kukatajwa miradi mitatu na bajeti ile ikasema wazi kwamba katika miradi hii mitatu imekwamishwa na upande wa pili wa Muungano kwamba haijatekelezwa kwa sababu mkwamo huu umetokana na upande wa pili wa Muungano:

Mheshimiwa Naibu Spika, moja; suala la barabara ya Wete-Chake ambayo ina mradi wa *BADEA*. Hii barabara ina udhamini na ufadhilli wa *BADEA* na bahari mbaya sana tunapofuatilia tunakuta kwamba miradi ya *BADEA* kwa upande wa Bara hata ukienda Mkoa wa Kagera kuna miradi kadhaa ambayo imefadhiliwa na *BADEA* lakini barabara hii moja kutoka Wete-Chake ambayo ni kilometa hazizidi 40 mradi huu Mheshimiwa Mpango umeletewa barua ukakumbushwa unatakiwa uweke *sign* tu kwa ajili ya utekelezaji wake lakini umeshindwa kuweka *sign*. Umeshindwa kwa sababu hauna *interest* na hii barabara, lakini wewe ujue Mheshimiwa Mpango wewe ni Waziri wa Fedha inawezekana Wizara ya Fedha siyo ya Muungano lakini unasimamia fedha ambazo ni za Muungano, unasimamia Benki Kuu ambayo ni ya Muungano, unasimamia Hazina ambayo inadhibiti fedha ambayo ni jambo la Muungano. Waziri unapojivua ukasema kwamba mlimi ni Waziri wa upande mmoja wa Tanzania Bara na ukajaribu kujikita zaidi kwenye mambo yanayohusiana na Tanzania Bara hapa utakuwa unapotea Kaka yangu na siyo sahihi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati unasimamia jambo linalohusu pande mbili za Muungano lazima ulisimamie kama vile ni Waziri unayehusiana na pande zote mbili. Unapokuja mradi upo Zanzibar na unataka *sign* yako kwa nini unapata kigumumuzi? Mheshimiwa Waziri suala moja ni hilo uje utujibu sasa kwamba barabara hii pamoja na kukumbushwa siyo mara moja, wala mbili, wala tatu, ufadhilli upo unataka *sign* yako kwa nini unakwama uje utujibu. (*Makofi*)

Mbili; suala jingine ni *Airport* ya Zanzibar *Terminal II*, kwa kweli tunasikitika sana na tunasikitika sana Mheshimiwa Mpango kuwa ni sehemu ya mtu ambae unakwambisha maendeleo ya Zanzibar. *Airport* hii inataka kupatiwa mkopo kwa ajili ya kufanyiwa *finishing*. Imeshajengwa, takribani imeshakamilika inataka kufanyiwa *finishing* inahitaji fedha kidogo tu, inahitaji mkopo lakini bado Wazanzibar na kuitia bajeti ya jana Baraza la Wawakilishi imesema wazi kwamba wewe ndiyo umekwamisha mradi huu. Kwa maana tunaposema ni wewe tunasema ni Serikali ya Jamhuri ya

Muongano imekwamisha kwa sababu Serikali ya Jamhuri ya Muungano inakopa kwa niaba ya pande mbili za Muungano, suala la mikopo ni suala la Muungano sasa wewe unapokopa kwa uoande mmoja ukasahau upande mwingine lawama zinakuja kwako, hilo ulijue.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo suala hili nalo ukija uje utujibu mkwamo uko wapi, maana yake kuna taarifa kwamba hawa watu walikula hela, wataje! Kama mlipeleka hela zikaliwa watajwe mbona humu Bungeni wanatajwa waliokula hela? Watajwe ili tujue nini cha kufanya lakini usijibebeshe wewe msalaba ambaao haukuhusu, kama haukuhusu, kama unakuhusu basi hapa tutakusulubu wewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu na muhimu sana ni suala la Bandari ya Mpigaduri. tatizo la Zanzibar ni uchumi, tatizo hasa la Wazanzibar ni uchumi na tatizo la Zanzibar ni umaskini, kinachotukwaza sisi ni umaskini sasa umaskini huu wa Zanzibar unanasibishwa kwamba umesababishwa na upande mwingine wa Muungano. Kwamba upande mmoja wa Muungano unaweka vipaumbele vyake, unaweka miradi yake, unaweka taratibu zake zinakwenda lkini upande wa pili kule unakwamba. Kwa mfano, Bandari ya Mpigaduri ipo ni mwaka zaidi ya 10 na wafadhili wapo, wahisani wapo, wawekezaji wapo ambaao wako tayari kuwekeza katika Bandari ya Mpigaduri hata Wachina karibuni miaka miwili, mitatu walikuja pale kufanya survey kutaka kuwekeza Bandari ya Mpigaduri lakini ukija ukiombwa sasa na bahari nzuri sana deni la Zanzibar ni bilioni tano, Zanzibar nzima inadaiwa bilioni tano. Bilioni mbili ni mikopo ya ndani, bilioni tatu tu ni mikopo ya nje hata tukichanga wenyewe tuna uwezo wa kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mpango unadaiwa trillioni 50 na bado unakopa tunadaiwa bilioni 300, tukikuambia huu hapa mkataba sasa unataka kujazwa mara umeandikwa kwa kiarabu, ulisema ufadhili huu wa Serikali ya Oman, Bandari ya Zanzibar kwa asilimia 80 ilikuwa idhaminiwe na Serikali ya Oman ukataba ukaingiwa,

uliandikwa kwa kiarabu, ulipoletewa ukasema umeandikwa kwa kiarabu ukatafsiriwa kwa Kiingereza umeletwa huna jibu hivi tufanye nini? tatizo hasa nini? Miradi imekuja imeikuta miradi kama hii lakini imetekelezwa upande mmoja wa Muungano upande ule kule visingizio haviishi, hivi ninyi hamna watu wa tafsiri wa Kiarabu katika Serikali nzima ya Jamhuri ya Muungano siyo kweli hilo nalo linahitaji jibu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari kwa upande wa Zanzibar ni uchumi, Bandari kwa upande wa Zanzibar ni suluhisho na ni ajira. Bandari ambayo ilikuwa ijengwe na Serikali ya Oman ilikuwa na uwezo wa kuweza kuchukua meli 16 kwa mara moja. Meli kubwa, meli za kisasa ambazo wanaziita wenyewe ni 4G meli ambayo inaweza kubeba makontena 400 mpaka 800 lakini kisingizio chako na Wizara yako na wataalam wako na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha hili analizungumza wazi wazi kwamba eti ikijengwa Bandari ya Zanzibar itaua Bandari ya Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mpango, Mheshimiwa Waziri wa Fedha anasema kwamba kujenga Bandari ya Zanzibar itaua Bandari ya Tanzania Bara lakini kuimarisha Bandari ya Tanzania Bara haitaua Bandari ya Zanzibar ambayo ndiyo uchumi wa Zanzibar, hivi ninyi Watanzania Bara mna mangapi ambayo mnaimarisha? Mna madini, mna ardhi kubwa, mna kilimo, mna ufugaji, mna uvuvi, hivi kujenga Bandari Zanzibar ni kosa kwamba kuimarisha uchumi wetu leo ni kosa? Huo umuhimu wa kuwa ndugu, umuhimu wa kuimarisha Muungano uko wapi? Hivi mnatueleza nini, mnajenga taswira gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika sana na hili niseme wazi kwamba ndani ya Bunge hili kuna Wabunge wanatokea Zanzibar na walikuwa ni viongozi wakubwa kule inafika mahali mtu ni Mtendaji Mkuu wa Serikali anasimama Bungeni humu anatumia dakika 10 anaona aibu na anaona haya kuitaja Zanzibar halafu kesho na keshokutwa mwaka 2020 eti anajinasibu anagombea Urais! Wazanzibar siyo mapoyoyo kiasi hicho watakuhukumu. Unaona haya kwa sababu unategemea Urais!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma Kombo Hamad kila Mbunge ana haki ya kuchangia aonacho ni bora, huwezi ukaanza kusema mtu anaona haya unajuaje aliona haya? Kwa sababu bajeti hii ni Bajeti Kuu na Wabunge wengi tu wanazungumza habari za Majimbo yao hamna mtu anawakataza lakini wakati wa kuzungumzia Majimbo ulishapita, ni kwenye ajeti za kisekta ndiyo tunazungumzia Majimbo, sasa hivi unazungumza Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mbunge, wewe ukiamua kutaja Zanzibar ni sawa lakini kiongozi mwagine akiamua kutokutaja usitake wewe kumuwekea maneno kana kwamba yeye amekosea sana mchango wake kwa sababu wewe mawazo yako ndiyo bora, siyo sawasawa. Mheshimu kama yeye anavyokushimu wewe, heshimu mawazo yake na mchango kuhusu Mbunge huyo mwagine aliyechangia unaondoka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. (*Makof*)

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, suala la bandari ambalo kwa mujibu wa takwimu itazalisha ajira karibu 80,000 kwa Zanzibar ni jambo kubwa sana, bandari ambayo itajengwa Zanzibar ile dhana kama kuna dhana, kama kuna tongo za masikio watu zinawatoka wanasema itaua bandari ya Tanzania Bara siyo kweli. Bandari ambayo inaenda kujengwa Zanzibar ni kisaidizi cha bandari ya Tanzania Bara au ni *partner* wa bandari ya Tanzania Bara. Nchi hii si ni moja? Si tunashirikiana kwenye masuala ya biashara? Si tunashirikiana kwenye masuala ya uchumi? Tunategemeana kwa masuala ya uchumi? Hivi kwa nini huku ni sawa huku siyo sawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mpango kwa dhana hiyo ya umoja na juzi tumejitisha sheria hapa kwamba mtukopee, sheria ile ikapitishwa humu kwenye Bunge walioipitisha ni sawa, walioikataa ni sawa, sasa leo kama kutukopea hamtaki mnachokihitaji ni nini? Baraza la Wawakilishi sasa hivi kule Zanzibar lina Wajumbe wa CCM

watupu lakini inafika mahali Mheshimiwa Dkt. Mpango unaambiwa bajeti ya Zanzibar ndiyo umekwamisha miradi hii, hivi tukueleweje? Maana kama ni mpinzani ni sawa, lakini bajeti ya nchi, bajeti ya Zanzibar inaenda kukusulubu wewe kwamba hawa ndiyo waliokwamisha miradi, hivi hamna haya? maana yake lazima tufike mahali tuambiane ukweli siyo sisi ni bajeti ambayo ilisema kuwa miradi hii minne imekwamishwa na hawa. Bandari ya Mpigaduri, barabara ya Wete-Chake na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kudumisha umoja wetu, kwa kudumisha Muungano wetu haya mambo lazima yaondoke, lazima yashughulikiwe ipasayyo. Mheshimiwa Dkt. Mpango huna budi ushughulike kama Waziri unayehusika na pande zote mbili hata kama Wizara ya Fedha siyo ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo inashangaza umetuletea bajeti, juzi nchi za Afrika Mashariki zimewasilisha bajeti zote zimewasilisha bajeti, nikashangaa nilikuwa najiuliza, humu haujataja Zanzibar umetaja mara mbili wakati unampongeza Dkt. Shein na umekuja kuitaja tena Zanzibar wakati unazungumzia VAT ya umeme, nadhani uliitaja ili ioneokane tu umeitaja, lakini haujazungumzia chochote kingine! Sasa mimi nikajuliza, Zanzibar haiwasilishi bajeti kwa sababu siyo nchi mionganoni mwa nchi za Afrika Mashariki ni sawa, lakini basi tunawasilisha bajeti ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania basi hata kutaja angalau hicho ambacho kinapatikana kule Zanzibar, kwa nini kisiwemo ndani ya hii bajeti? Kwa hiyo Mheshimiwa Mpango mimi nakuomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la utalii na hili niseme kwamba suala la utalii siyo suala la Muungano kiukweli, lakini nimestuka wakati tunalalamikia masuala ya biashara tulilalamika kwamba biashara Zanzibar...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa Juma Kombo Hamad ahsante sana. Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba ajiandae.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Naomba nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa neema ya kuondoka CHADEMA kuja CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua nilikuwa kule ng'ambo kumbe nilikuwa sjui tulichokuwa tunakifanya kule, tulikuwa tunasema uwongo kwa kile tusichokiamini. Nimekuwa nikisawakiliza Wabunge wa CHADEMA na wa kule ng'ambo kwa ujumla wanasema Serikali ya CCM inafanya maendeleo ya vitu na siyo maendeleo ya watu, nawasikiliza nasema hawa vipi hawa au wamerogwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Ayoub 13:4 inasema "lakini ninyi hubuni maneno ya uwongo, ninyi nyote ni matabibu wasiofaa". Isaya 9:15 inasema "Mzee mwenye kuheshimiwa ndiye kichwa na Nabii afundishae uongo ndiye mkia", Manabii wafundishao uongo ndiyo mikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nina llani ya CHADEMA hapa. Nilikuwa Mbunge wa CHADEMA, nillinadi hii wakati nikiwa mgombea ninajua na wanajua. Leo nataka nipite humu tuangalie maendeleo ya vitu kwamba kweli Serikali ya CCM inafanya maendeleo ya vitu na siyo maendeleo ya watu, nitaangalia baadhi ya maeneo, naomba nianze na Bandari. Wao wanapinga ujenzi wa bandari na wanasema ukiangalia kwenye ukurasa wa 40 wa llani yao watafanya nini:

Kwanza ni kujenga reli mpya na kukarabati zilizopo kwa viwango vya kisasa kwa kuzingatia maslahi ya nchi. wanaopinga reli ya kisasa ya *standard gauge* ni akina nani?

**WABUNGE FULANI:** Wao.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuboresha zilizopo na kujenga mpya kama vitega uchumi vya Taifa. Tatu, ni kujenga Shirika la Ndege la Taifa linaloijidesha kwa misingi ya faida. Ndege zimenunuliwa wa kwanza kupinga ndege ni watu gani?

**WABUNGE FULANI:** Hao hao.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ukurasa wa 41 unasema Shirika la Ndege la Taifa Air Tanzania.....

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Kuhusu utaratibu

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha subiri kidogo. Mheshimiwa Selasini naomba ukae kidogo. Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha pamoja na kwamba umenukuu kitabu cha dini kwamba kinawaita pengine watu wa aina fulani kwamba wao ni mikia na kitu kama hicho, lakini kwa kuwa sehemu hii Waheshimiwa Wabunge siyo kwamba vinakatazwa vitabu vya dini kunukuu, lakini pale ambapo ile lugha iliyotumika kwa sababu hatuna uwezo wa kuanza kutoa mahubiri na kutoa maana halisi ya hayo maneno humu ndani, yale maneno yako uliyoyachukua mwanzo, uliyoyanukuu kwenye kitabu cha dini Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha matumizi yake kwenye kusema nani ni mkia na nani siyo mkia hayataweza kutumika humu ndani kwa sababu siyo lugha ya Kibunge.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nimekuelewa lakini maana yangu ni kwamba, Ilani ya CHADEMA iliongelea ndege lakini wakija humu ndani wanakataa kwa nini? Ni watu wa namna gani hawa, tuwaite jina gani? Mimi acha niende. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ukurasa wa 41 wa Ilani yao inasema: "mizigo yote mizito kusafirishwa kwa njia ya reli na meli" leo wanageuka hapa, tuwaite jina gani? hawa watu wa ajabu sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ukurasa wa 45 wa llani yao wanasema kupiga marufuku uuzaaji wa korosho ambazo hazijabanguliwa na kuhakikisha kwamba asilimia 100 ya korosho zote tunazozalisha zaidi ya tani 200,000 zinabanguliwa hapa Tanzania. Rais Magufuli amesema hakuna kuza nje Korosho nini? ambazo hazijabanguliwa na akasema Wanajeshi, bangua hata kwa midomo yenu kabangue tuuze korosho zilizokuwa *processed* wanakataa. Wewe ngoja nipite kwenye llani tulia kwani mnaisomaga basi ninyi! Hawa wanaambiwaga fanya hivi wanafanya hata bila kufikiria. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 53 unasema: "vipaumbele havijawekwa kwenye uendelezaji wa vyanzo vya uzalishaji wa umeme wa bei nafuu vilivyopo nchini, mfano *Stigler's* kwenye Bonde la Mto Rufiji". Wanasi mama hapa wanaplinga mradi wa umeme wa *Stigler's* hawa tuwaite vipi, kwenye llani yao ipo hapa? (*Makofii*)

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Tulia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka nataka kuamini umezingatia matakwa ya Kanuni ya 68(8).

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimezingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafurahi sana kuona mzungumzaji pale anakubali kwamba kweli CHADEMA tumeandaa llani sahihi kabisa kwa ajili ya kuendesha Taifa hili na Serikali ya CCM imeyachukua na sasa hivi inayatumia kuhakikisha kwamba inatekeleza majukumu yote ambayo tulikuwa tumeweka kwenye llani yetu. Tunashukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, hapo sasa ni ufanuzi wa jambo gani uliloeleza? Kila wakati nawakumbusha matumizi ya Kanuni.

Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, endelea na mchango wako.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru leo baada ya kusoma hili andiko wamekubali kwamba CCM inafanya kazi, ahsante sana. Leo ndiyo wamekubali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia ukurasa wa 57 pia wameongelea, Serikali ya CHADEMA sio ya UKAWA, Serikali ya CHADEMA itaupa uzalishaji mkubwa wa umeme wa maji kipaumbele namba moja, yaani nyie vigeugeu kweli kweli sijawahi kuona. Imeandlikwa kwamba kipaumbele cha kwanza cha uzalishaji wa umeme, cha kwanza maji, wameandika kwenye llani. Leo akisimama pale anasoma huwa nakaa nawaangalia hivi hawa wako sawasawa hapa kweli? Serikali ya CHADEMA itaupa uzalishaji mkubwa wa umeme wa maji kipaumbele namba moja, umeme wa makaa ya mawe kipaumbele namba mbili, umeme wa gesi asilia kipaumbele namba tatu, muende mkasoma llani yenu vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi namshukuru Mungu kwa kuniipa neema ya kutoka kule. Unajua wale watu ukisema moja ongeza moja ni mbili, CCM akisema moja ongeza moja ni mbili wao watasema ni saba.

## **TAARIFA**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Goodluck.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka nimpe taarifa Mheshimiwa

anayeongea kuwa CHADEMA walikopa kwetu mgombea pamoja na llani. (*Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hebu...

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee.

**NAIBU SPIKA:** Subiri kwanza Mheshimiwa Ryoba.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni hizi zinatutaka tutumie wakati wetu vizuri. Kwa hiyo, zinavyosema taarifa unakuwa unatoa ufanuzi kwenye jambo analochangia mtu mwillingine, kwenye hoja yake. Mheshimiwa Ryoba Chacha.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, unaona ukurasa huu kwenye hii llani, Mheshimiwa Mlinga alisema Lowassa ndiye aliyeandika llani wakakataa, ona kwenye huu ukurasa picha ya Lowassa hii hapa. Kwa hiyo, Lowassa alivyotoka CCM aliondoka na ile llani ya CCM aka-copy akapeleka kule.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)*

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Ndiyo, huo ndiyo ukweli.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)*

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Hii hapa, anayebisha asimame apinge, mimi ninayo hii hapa, hakuna wa kupinga wanajua ni ukweli. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya CHADEMA na UKAWA ilikuwa ni ujisadi, Mheshimiwa Magufuli

ameshughulika na ujisadi. Unawasikia wanaongelea ujisadi sasa hivi, kimya, hola hamna kitu, yaani sasa hivi hawana hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine wanasema ukurasa wa 37, sekta ya bandari imegubikwa na rushwa pamoja na utendaji mbovu kiasi kwamba mrundikano wa mizigo umekuwa mkubwa sana bandari na kupelekeea mapato yake kuwa madogo kulingana na fursa za usafirishaji. Mheshimiwa Magufuli alivyoingia tu madarakani ziara zake za kwanza zile alienda wapi?

**WABUNGE FULANI:** Bandarini.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Bandarini akaenda akafumua, kuna watu walijifanya Miungu, eeh Mheshimiwa Magufuli ni mwanaume, haki ya mama. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, nilikuwa nataka kuwakumbusha tu kwamba waiunge mkono Serikali ya CCM maana inafanya mambo mazuri kama mimi nilivyofanya ukienda Serengeti sasa hivi mambo safi kabisa. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, muda wako umekwisha. Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

Tunaendelea na Mheshimiwa Shally Raymond atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba na Mheshimiwa Zainab Katimba ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kipekee kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa muda huu kunipa tena pumzi ya kuweza kuchangia mambo ya maendeleo katika nchi yangu, nchi yenye amani, huru na ambayo inaheshimuraia wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue muda huu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango

kwa kutuletea bajeti nzuri tofauti na bajeti zote na hata huko nje wanasema walizoea kusikia nyongeza kwenye pipi, karanga, kilevi, mafuta, leo mambo ni tofauti kabisa. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wangu huyo, Dkt. Philipo Mpango, Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Ashatu Kijaji na mimi nasema kwa kweli hizo *PhD* zao ni za uhakika. Nampongeza Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu na timu yao yote. Zaidi sana nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliosimama na kuchangia bajeti hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijaitendea haki nafasi yangu kama sitakishukuru chama changu cha CCM Kilichopitisha jina langu mara kilipopokea jina hilo kutoka kwa wanawake wa Kilimanjaro. Nawashukuru sana wanawake hawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumzia keki ya Serikali. Keki hii sasa iko kwenye mgawanyo lakini inapatikanaje? Bajeti ya Serikali au bajeti yoyote ile ina pande mbili, ina makadirio ya mapato na matumizi, kwenye mapato tuna kodi, mikopo, misaada na pia kwenye bajeti ya Tanzania tunayo pia nafasi ya kupata gawio kule Serikali ilipowekeza. Hapa niwapongeza sana *CRDB* kwa kutoa gawio la shilingi bilioni 9.9 zikiweko shilingi bilioni 6.7 za Serikali na zile nyingine kwenye taasisi. Pia *NMB* walitoa na nadhani mashirika mengine machache yametoa. Naomba huo uwe ni mwendelezo. Upande mwingine wa bajeti una matumizi yanayotumika kwenye *social services*, vichocheo vya maendeleo ikiweko mindombinu kama barabara lakini yote hayo ni kwa ajili ya maendeleo na mambo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, walipa kodi ni wananchi wote tukiwemo sisi na wale wa chini na ili kodi iongezeke inabidi wale wafanyabiashara wadogo wasaidiwe ili waweze ku-*graduate* wawe wafanyabiashara wakubwa. Tumeona Serikali yetu imetoa vitambulisho kwa wafanyabiashara wadogo ili ikifika mahali sasa na wao watakuwa wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kutoa vitambulisho ni moja lakini waendelee kutoa elimu kwa watu hawa ili waweze kuja kuwa wafanyabiashara wakubwa. Hata hivyo, niiombe Serikali yangu sikuvi, katika kuwalea hawa wafanyabiashara wadogo na kati wawalipe pia wazabuni, hao ni wafanyabiashara wa kati wanaoenda kuomba mikopo benki, wanatoa huduma Serikalini lakini wakati wa kulipwa inachukua muda sana na watu wale wengine wanakata tamaa au wanaondoka kabisa kwenye biashara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, niiombe Serikali yangu sikuvi ilipe pia madeni ya wale wanaotumia *utility*, wanaotumia huduma za maji na umeme, walipe yale mashirika yanayotoa huduma hizo. Hapa nawaombea sana Mamlaka za Maji ikiwemo Mamlaka ya Maji ya Moshi (*MUWSA*), deni lake sasa ni takribani shilingi billioni 2, limeshahakiliwa lakini bado hawajalipwa; *DAWASCO* imelipwa na pia Arusha imelipwa. Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Fedha ametenga fedha, naomba katika ile awamu ya kwanza ya kulipa watu hawa waweze kulipwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme wazi kwamba naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri ili nisije nikasahu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nina mambo mawili ambayo ni maombi sasa. Naomba ili wafanyabiashara hao katika kuwafanya mambo yawe rahisi kibiashara, wa kati na wakubwa, ile *Blue Print* tulioambiwa hapa sana chonde chonde iletwe na tufanyiwe semina na wananchi waeleweshwe ili wajue jinsi gani watarahisisha mambo yao kwenye biashara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo linasumbua sasa hivi, mwaka jana tuliliona ni zuri tukashereheke ni kuhusu *sanitary pads* za wanafunzi au wahitaji ambao ni mabinti. Kweli hakuna jambo ambalo ni bure na sisi kila tukisimama hapa tumeona ambavyo Wizara hiyo imepata shida na ilipo-*test*imeona kwamba jambo hilo halikuwa kwa

manufaa ya wahusika. Basi nami nije pia na pendeleko langu, naomba kuwepo na vocha, tunasema kuwe na tozo kama tulivyofanya kwenye chandarua (hati punguzo), ikiwezekana taulo hizi za kike kwa wanafunzi wetu zipatiwe hati punguzo. Tuliona jinsi ambavyo awamu iliyotangulia ilishughulikia malaria ikatoa hati punguzo kwenye chandarua, kiwanda kikaweza kupata msamaha kiasi lakini pia mhitaji anakwenda na hati punguzo kununua. Hawa ni wanafunzi, wapatiwe vocha waende wakapatiwe hati punguzo hiyo waweeze kununua pungufu ya bei, kwa ujumla wake tutakuwa tumechangia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda mtauliza kwa nini haswa? Mimi ni jinsi ya (K), ni mwanamke, najua shida tunazozipitia toka utoto mpaka kufikia hapa. Kuanzia miaka 15 mpaka kufikia miaka 55, hilo jambo halikwepeki lakini hatuangallii kwa wote tunaangalia kwa wanafunzi na hasa wanafunzi wale ambao wanatoka katika mazingira duni. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wanafunzi ambao kwa siku tano hawaendi darasani kwa vile ila hali inakuja na mambo mengi, kichwa kitauma, maumivu ya tumbo, kichefuchefu, lakini sio hiyo tu hata ile kutoka ni shida. Kwa hiyo, ili nisifafanue zaidi kwa sababu wote wanaelewa, naionomba Serikali yangu sikivu iangalie itakachowezza kufanya ili watu hao wanufaike. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kuhusu bajeti hii ni kwenye kilimo. Kweli kila aliye humu ndani amepitia eneo la kilimo. Mimi nimetokea eneo ambalo kahawa ndiyo zao la biashara lakini pia kuna ndizi na mazao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema nini kuhusu kahawa? Wako waoteshaji kahawa wenyewe mashamba makubwa pembeni yake yuko mtu wa kawaida ambapo shamba lake dogo lakini shamba la mtu yule ni choka mbaya yaani limekata tamaa, shamba na mwenyewe wamekata tamaa. Naiombala Serikali yangu iweze kuzungumza na hawa wakulima wakubwa kama wataweza kuungana sasa na

wale ambao wanawazunguka kama inavyofanyika Kilombero kwa *out growers* wa miwa ifanyike hivyo Kilimanjaro kwa wale wakulima wa kahawa ili tuweze kuwa na kahawa nzuri na tuongeze pato la Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye utalii, nataka nizungumzie tu kwamba kuna kodi ambazo wamepunguziwa lakini pia kuna kodi ambazo bado zipo lakini wale waliokuja kama wadau kwenye Kamati ya Bajeti shida yao siyo ile tozo ya kodi. Juzi Mheshimiwa Waziri amepunguza ule ukiritimba wa kwenda kulipa tozo nyingi. Namwomba ikiwezekana kwenye utalii aangalie ili kuwaweka kwenye *one stop center* wakifika walipe ili watalii hawa wapate tena hamu ya kurudi Tanzania na kuja kutembea bila kufikiria shida zilizopo za kuanza mahangaiko hapa na pale. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha, kengele ya pili imeshagonga.

Tunaendelea na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Katimba na Mheshimiwa Rose Kamil Sukum ajiandae.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti kuu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salome, una dakika saba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza, nimsaidie kaka yangu Marwa Ryoba, kaka yangu wa zamani kwamba ukitembea na llani ya Uchaguzi ya CHADEMA ujitalidhi upate na vitabu vingine vitatu vitakusaidia sana. Najua una kazi kubwa sana uko ulipo, tafuta Sera ya CHADEMA ambatanisha na Mpango wa Utekelezaji wa Bajeti na bajeti kivuli ya CHADEMA. Hapo utakuwa umefanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muugano wa Tanzania ....

## **TAARIFA**

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salome, kuna taarifa, Mheshimiwa Ryoba

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa, kwa wale tuliogombea kupitia CHADEMA....

**MBUNGE FULANI:** Yeye hajagombea.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Document tuliyopewa ni llani, CHADEMA haikuwa na Sera, juzi tu ndiyo wametengeneza Sera, hawajawahi kuwa na Sera, wana hii llani.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Yeye hajagombea.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Huyo ni Viti Maalum hajawahi kugombea Ubunge.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 8(b) inasema: "Serikali ili kuhakikisha kwamba inatekeleza majukumu yake ni lazima ihakikishe inaweka ustawi wa watu". Nasema hivi, Mbunge yejote aliyemo humu ndani

ambaye ataunga mkono bajeti hii ya Mheshimiwa Dkt. Mpango halafu akajiita mzalendo nitamshangaa. Nasema hivyo kwa sababu zifuatazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii ya Mheshimiwa Dkt. Mpango imekwenda kupeleka asilimia 39% ya bajeti yote kujenga *Stigler's* na *SGR*, maendeleo ya vitu. Bajeti hii inakwenda kinyume na dunia inayokwenda, dunia kwenye *Sustainable Development Goals Stigler's* kwa maana ya miundombinu na nishati ni kipaumbele Na.7 na Na.9. Kipaumbele Na.1 ni kufuta umasikini; Na.2 ni kuhakikisha hakuna njaa kwenye nchi; Na.3 ni afya; Na.4 ni elimu bora; Na.5 ni usawa wa kijinsia; Na.6 ni maji safi na salama, sasa ndiyo unakuja Na.7 nishati nafuu kwa maana ya *Stigler's Gorge then* unakuja Na.8 kazi yenye staha na Na.9 ni miundombinu ambayo ndiyo *SGR*. (*Makofi*)

## **TAARIFA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba, kuna taarifa, Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumpa taarifa mzungumzaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati jana nachangia nilisema kwamba asilimia 65% ya watu wetu wanategemea sana kilimo na nikaainisha moja ya matatizo ya kilimo ni miundombinu ambayo ingewezesha wakulima wetu kufikisha mazao yao kwenye masoko. Nikazungumzia suala la reli na barabara. Sasa anaposema kwamba Serikali hii inaingiza fedha nydingi kwenye miundombinu inaacha maendeleo ya watu hapo namshangaa. Maendeleo ya watu yanakuja baada ya kuimarisha miundombinu ili wakulima wawewe kutoa mazao yao mashambani na kuyafikisha kwenye masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa hiyo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, unilindie muda wangu, tafadhali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa lugha nyingine msemaji aliyetoka kunipa taarifa anamaanisha kwamba Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, Serikali ya wanyonge imepeleka ile shilingi triliioni 33.1 ambayo leo tunatamba ndiyo bajeti ya Serikali, hayo anayoyasema ye ye ni shilingi triliioni nane tu, pesa nyingine yote wamekwenda kuboresha miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba kununua dawa tunapambana kwenye triliioni nane, Wabunge 395 tulipo humu ndani dawa ni triliioni nane hiyo tunagombania, kupunguza udumavu wa wananchi triliioni nane, kwenda kumtua mama ndoo kichwani kelele zote triliioni 8 na kuinua kilimo triliioni nane; kwa mwaka huu wote wa fedha na mambo mengine yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa nyingine yote ambayo iliyopo inakwenda kulipa deni la Taifa triliioni tisa, kwenye mishahara triliioni saba triliioni tatu matumizi mengineyo na kwenye pesa ya maendeleo hiyo triliioni nane usisahau ndiyo tunapoenda kutoa hela ya Stiegler's na *SGR*yaani reli ya katika na huo mtambo wa kufua umeme wa Mto Rufiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Serikali inaturudisha nyuma ambako hatukuwahi kufikiria. Hivi jiulize swalii, mwaka jana wamesemba *projection* zao ilikuwa ni kukusanya triliioni 1.4, wakakusanya triliioni 1.2. Na hiyo pesa wamekusanya alisema hapa Mheshimiwa Lwakatare, walitumia mizinga ya aina zote; matrafiki wakapanda juu ya mti, *DPP* akapeleka kesi, huku wajasili amali vitambulisho 20,000, kila aina ya mbini wakaishia 1.2 triliioni. Sasa angalia sasa hivi wana-*projection* ya kukusanya 1.6 triliioni, tutapona kweli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele vyao sasa nya kufikisha 1.6, wanaenda kuweka kodi kwenye peremende, wanahangaika na mawigi, wanakwenda chocolate waweke kodi, leo wametoa VAT kwenye taulo za kike. Hiyo ndio aina ya wataalam tulionao kwenye nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, atakayeunga mkono bajeti hii nitamshangaa. Kwanza imewekeza kwenye vitu lakini pili pesa yote ya kuendesha miradi inatokana na wananchi wenyewe...

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** wanasema asilimia 15 ya bajeti watatoa kutoka kwenye...

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa ya mwisho hiyo kwa Mheshimiwa Salome Makamba

## **T A A R I F A**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nataka nimueleweshe ndugu yangu Mheshimiwa Salome Makamba kwa sababu yeye ni mwanasheria, mimi ni *administrator by professional*. Unapotaka kujua pesa kiasi gani imepelekwa kwenye Sekta ya Elimu usiangalie Wizara ya Elimu pekee, nenda kaangalie TAMISEMI, Utumishi na Elimu yenye. Na hata Wizara ya Afya ukitaka ujue pesa kiasi gani imepelekwa kwenye Sekta ya Afya nenda kaangalie TAMISEMI ndio utakuta ujenzi wa miundombinu, vituo nya afya na Hospitali za Wilaya na Wizara ya Afya yenye pamoja na Utumishi mishahara ya madaktari. Kwa hiyo, usiangalie Wizara ya Afya, nenda kaangalie na Wizara nyingine. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapana, naomba niendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasema kwamba asilimia 85 ya makusanyo ya Serikali wanakusanya mapato kutoka kwa wananchi mapato ya kikodi yaani hiso njia walizokuwa nazo na peremende na kila kitu wanatafuta asilimia 85 ambayo mwaka uliopita walifeli. Asilimia 15 wanategemea wafadhili na mikopo nafuu kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa angalia picha inavyokwenda, hawa wafadhili mwaka jana kwa mujibu wa Ripoti ya UNESCO walikata misaada Tanzania kwa zaidi ya asilimia 49. Na haya yote wameyasema kwa nini wamekata mikopo hiyo, wamekata mikopo na wamekata misaada. Hali ya demokrasia nchini siyo shwari, utawala bora hakuna, uhuru wa vyama vyaa siasa hakuna, hivi hao watu mnaotegemea watawapa hiyo asilimia 15 itatoka wapi? Wanakwenda kuwakamua Watanzania kwa kiwango ambacho mzalendo ye yote aliyeo humu ndani hawezi kukubaliana na hii bajeti. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kukubali Mheshimiwa Dkt. Mpango ku-support bajeti yako mpaka utakaponieleza ni vyanzo vipi vya uhakika ulivyojiandaa navyo vya kupata pesa kwa ajili ya kuendesha bajeti yako. Mpaka utakaponieleza ni lini utaboresha *private sector* ambayo ndiyo *engine* ya uchumi wa nchi, utaiboresha lini ili uitoe Serikali kwenye matrillioni ya kununua ndege, kujenga *SGR* na kwenda kujenga sijui mradi wa Mto Rufiji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo yafanywe na *private sector*, ninyi mtekeleze Katiba ya nchi yetu kama livyoapa kuilinda kwa kwenda kufanya maendeleo ya watu badala ya kufanya maendeleo ya vitu. Sitopiga kura ya ndiyo kwenye bajeti hii ya Serikali ya mwaka 2019/2020. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa Salome, ahsante sana. Mheshimiwa Zainab Katimba atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, mheshimiwa Benadeta Mshashu ajiandae.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa niweze kuchangia hoja iliyopo mezani. Kwanza nianze kwa kupongeza sana jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano, jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara katika kuleta maendeleo katika nchi yetu hii ya Tanzania, lakini kwa upekee kabisa na kwa msisitizo mkubwa sana, niishukuru Serikali kwa kuwa sikivu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa katika bajeti ya Wizara ya Fedha nilitaka kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababu ya hoja ile ya kutaka Serikali iweze kutoa grace period ya miezi 6 kwa wafanyabiashara wanaoanza biashara/wafanyabiashara wapya kabla ya kuanza kulipa ile kodi ya mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ukifungua katika ukurasa wa 84 wa hotuba utaona kwamba wamesema hapa kwamba Serikali imesema kwamba itatoa unafuu wa kutolipa kodi kwa kipindi cha miezi 6 kuanzia wakati mfanyabiashara au mwekezaji anapopewa namba ya utambulisho wa mlipa kodi. Kwa hiyo, ina maana Serikali ni sikivu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana kwa sababu hii ilikuwa ni changamoto kubwa sana ya vijana pamoja na wafanyabiashara wengine lakini ilikuwa ni changamoto kubwa sana kwa vijana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ukiangalia pia msingi wa kodi ya mapato (*income tax*). Msingi wa *income tax* upo kwenye faida yaani *income tax* inapatikana kutoka kwenye faida na siyo mtaji. Na hapo awali tuseme tu labda tuzungumzie vijana walikuwa wanakutana na changamoto gani yaani unakuta kijana anakosa ajira, hawezi kuajiriwa inabidi ajajiri yeye mwenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiacha tu kwamba unakuta kijana amesoma miaka 3 Shahada yake ya *Sociology*, miaka yote anafundishwa *theories* za *Marxism* kina Karl Marx wanasema nini na nini halafu anakosa ajira inabidi aingie kwenye biashara ambayo tukiangalia hata katika mfumo wetu au katika mitaala yetu ya elimu, bado hajatengenezwa kiasi ya kuwatengenezea msingi wa kuanzisha na kuendeleza biashara wahitimu wetu, unakuta kwamba kijana hajui anaanzia wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, akipambana na hiyo changamoto, anarudi tena anakutana na changamoto ya kukosa mtaji, akipambana na changamoto ya kukosa mtaji, akipata huo mtaji kwa mkopo bado anakutana na suala kwamba lazima atumie mtaji wake ule kuanza kutoa kodi kabla hajaanza kufanya biashara. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa sababu kwa kutoa nafuu hii ya miezi sita kwa mfanyabiashara mpya kutokulipa hii kodi kwa kweli mmewasaidia vijana sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri katika siku hizo za mbele, tuone kama tunaweza ku-*extend* hii *grace period* ili iweze kufikia hata mwaka mmoja kwa sababu kama nchini wanakuja wawekezaji ambao wanaweza kupewa *grace period/tax holiday* hadi ya 5, 3 years. Kwa hiyo, sisi wazawa wenyewe ili ku-*encourage* watu waweze kuwa na moyo wa kufanya *startups* na kwa sababu tunajua kujenga msingi wa biashara siyo jambo rahisi. Kuna mtu anaweza akaanzisha biashara mwaka mzima lakini akashindwa kuiimarisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba sana Serikali katika hizo siku za mbele tuangalie ni namna gani tutaongeza hiki kipindi ili kiweze kufika mwaka mmoja. Tutawa-*encourage* watu wawe wana moyo wa kuanzisha biashara, wasiwe na uoga lakini hii itawanufaisha sana vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tauzo za kike tumesikia limezungumzwa sana, imechangiwa na Wabunge mbalimbali lakini mwaka jana tuliona kwamba Serikali ilichukua jitihada ya kuondoa VAT katika bidhaa hii ya tauzo za kike. Hata hivyo, tumeona jitihada hii haikuzaa matunda kwa sababu haikuleta punguzo la bei katika bidhaa hii ili kuleta unafuu kwa watoto wetu wa kike hususan wale ambao wako shuleni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme tu kwamba ninaunga mkono maamuzi ya Serikali ya kuirudisha hii VAT kwenye bidhaa hii ya tauzo za kike lakini siyo hivyo tu nina ushauri. ushauri wangu ni upi, pamoja na kwamba VAT imerudishwa katika bidhaa hii ya *sanitary towels* hizi tauzo za kike na kwa kuzingatia kwamba *raw materials* au malighafi zinazotumika kuzalisha bidhaa hii ya tauzo za kike ndani ya nchi na zenyewe zimeondolewa ushuru wa forodha lakini naomba Serikali iweze kuondoa VAT katika *raw materials* zinazotumika kutengeneza hizi *sanitary towels*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja inaweza ikawa kwamba ukiondoa VAT kwenye malighafi za kutengeneza tauzo za kike ndani ya nchi, hizi malighafi zinaweza kutumika pia kwa matumizi mengine tofauti. Sasa kwa hoja hiyo, Serikali inaweza ikaangalia utaratibu wa kuweza kuwa malighafi hizi zinaagizwa kwa *quarter* kama vile inavyofanyika sukari za viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii naamini kwamba ikiondolewa hii VAT kwenye hizi malighafi (*raw materials*) za kutengeneza tauzo za kike itasaidia katika kupunguza gharama ya uzalishaji na itapunguza pia bei, lakini itapunguza bei ya tauzo za kike kama Serikali itawezekuweka

na kutoa bei elekezi na kuelekeza kwamba bidhaa hii ya taulo za kike iweze kuwekewa *price tag* yaani kama vile tunavyoona ukinunua kwenye gazeti, gazeti limeandikwa 1,000. Kwa hiyo, hawesi mfanyabiashara akachukua gazeti akaenda kuuza 1,500 kwa sababu bei ya gazeti imeshaandikwa kwenye lile gazeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali iweze kuona namna gani itaelekeza na ita-*regulate* ili bidhaa hii ya taulo ya kike kwa sababu tunajua tayari *cost of production* itakuwa imepunguzwa na faida itakuwa inapatikana, wafanyabiashara wasitumie misamaha hii ya kodi kujinufaisha na kuongeza wigo wa faida yao na badala yake ile *intention* ya kuondoa hizi kodi iweze kuwa *realized*. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iweze kufanya hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, ushauri wangu mwingine ninaomba Serikali iangalie uwezekano wa kuweka au kutolewa kwa hizi *sanitary towels* katika mfumo wetu wa bima za afya (*health insurance*) kwa sababu sisi sasa hivi tunaelekea katika utaratibu wa kuhakikisha kwamba kila mtanzania anaweza kuwa na bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika mfumo wa bima ya afya, kinachoweza kufanyika sisi tunajua bima za afya zina madaraja na hata kwa mfano leo hii *National Health Insurance Fund (NHIF)* yenye ina kadi ya kijani, nyekundu, njano na kadi za Kibunge, hayo yote ni madaraja ya bima ya afya. Kwa hiyo, sasa yale madaraja kwa sababu tunataka hizi taulo za kike (*sanitary towels*) ziweze kupatikana kwa wale wenye uhitaji ambao tumeshasema hapa wenye uhitaji ni watoto wetu wa kike ambao wapo shulenii wanakosa hizi taulo za kike na kuna siku wanakosa masomo shulenii kwa kukosa vitu vya kujihifadhia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa muktadha huo huo, hii bima ya afya unaweza kutengenezwa utaratibu ambapo kuna madaraja ya hizi bima za afya ambayo *beneficiaries* wake ndio wanaweza ku-*benefit* kwa kupewa *sanitary towels*. Na kwa sababu hizi bima za afya anaweza

akakata bima mzazi na *beneficiaries* wakawa familia nzima au anaweza akawa mnufaikaji mmoja yule aliyekata bima. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye ngazi ya familia inajulikana na hata zile kadi za bima, kila muhusika anapewa na *particulars* zake zinajulikana. Kwa hiyo, ule umri wa kuwa ni mwanafunzi na vielelezo vya kwamba huyu ni mwanafunzi vinaweza vikajulikana na Serikali na hawa wenye sifa wakawa wana utaratibu wa kupewa hizi *sanitary towels* kwa kila mwezi labda unasema wanapewa *piece mbili*. Mimi na... (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga, ahsante sana. Mheshimiwa Rose Kamili Sukum atafuatiwa na Mheshimiwa Benardetha Mushashu, Mheshimiwa Ahmed Ngwali Juma ajlandae.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Fedha lakini kabla sijaenda huko nipende kusema kwamba sisi kama wapinzani mnavyotuita, sisi kazi yetu ni kueleza yale maeneo ambayo hayajaka sawasawa lakini yale yaliyokaa sawasawa sisi hatuna haja ya kumpaka mafuta Mheshimiwa Waziri au Rais, tunaangalia yale mabovu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mpokee maoni ya Kambi ya Upinzani kwa sababu tunaeleza hayo. Sasa Mheshimiwa Dkt. Mpango wewe unapakwa *lubricant* halafu *then* wanaweza kukuangalia saa nyingine mambo yakaharibika. Kwa hiyo, yale mabaya tunapokueleza usikatae naomba uyapokee. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine pia vijana wameeleza leo mambo mazuri sana, nimefurahi sana au nimefurahishwa sana na Mheshimiwa Mlinga alipokuwa

anasema kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa anatumia llani ya CHADEMA, natoa pongezi nyingi sana kwa sababu ile llani iliandikwa vizuri sana na ilifanyiwa kazi na watalaam vizuri sana, haikuwa hovyohovyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la picha ambazo anazisema mwenzangu Mheshimiwa Marwa Ryoba, picha zipo hata mahali popote hata kwenye vitabu vyetu hivi vya Mheshimiwa Dkt. Mpango vina picha, picha siyo tatizo la mtu. Yule hakwenda kuandika llani bali Lowassa alihamia CHADEMA kama yeche aliivyo hamia CCM. Kwa hiyo, siyo suala la kwamba alienda kufanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niwaeleze kwamba hakuna kitu kibaya kama kujifunua uwemo wako wa kutumia akili. Kwa hiyo, hawa vijana wasipende kujifunua funua, huyu anayekuwa huku anakwenda kule muogopeni sana mtu wa namna hiyo, lakini kubwa zaidi, hata usemi wa Mheshimiwa Rais siku moja aliwakaribisha akasema ng'ombe aliyekatwa mkia hata kwenye zizi ng'ombe wenzake wanamuona. Kwa hiyo, kwa kuwa wamekatwa mikia, mnawaona kwa hiyo, muendeleo kuwatumia vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naona mnapiga makofi, wakati huohuo mlipozungumwa nyie kuhusu mkia mlitaka kunyanyuka hapa. Mheshimiwa Rose Kamili hayo maneno nadhani ulikuwa umekaa hapo wakati nikiyatolea maelezo. Kwa hiyo, hakuna mtu anatakiwa kuzungumzwa kana kwamba yeche ana mkia au yeche ni mkia. Kama nilivyokataa kuhusu ninyi, hivyo na ninyi huku nawakataza kuita wenzeni wamekatwa mikia au wamekatwa chochote ama wao ni mikia.

Kwa hiyo, na ninyi ndio mnapenda sana kutumia neno linaitwa *double standard*. Kwa hiyo, ndio muelewe maana ya *double standard* ndiyo hii. Namna ambavyo yeche

nimemkataza na nyie msitumie, nashangaa wanaoshangilia wakati wao walitaka kunyanyuka wakati Mheshimiwa Ryoba Chacha alikuwa anachangia.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nimenukuu usemi wa Mheshimiwa Rais Magufuli... (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rose Kamili yehe hakunukuu kitabu, si alinukuu Biblia ama hukumsikia? Alinukuu kitabu cha Biblia na nimemkatalia, wewe unasema umenukuu maneno ya Mheshimiwa Rais, aah! Si sawasaw na ndiyo maana nimesema nawashangaa wa upande wako wanaokupigia makofi kwa sababu wao walitaka kuonesha kujisikia vibaya wakati Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha akichangia, kwa hivyo nashangaa sana. Tafadhalii, hayo maneno yasitumike kama ambavyo nimeyakataa upande wa Chama cha Mapinduzi, na ninyi msiyatumie CHADEMA ama chama chochote humu ndani.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba unilindie muda wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda kwenye hotuba aliyo tupatia Mheshimiwa Dkt. Mpango, nataka kunukuu maneno ya Mheshimiwa Dkt. Mpango ya ukurasa wa 95 aliyesema kwamba anawasihi wananchi wachague wenye sifa mpaka tisa. Sasa nachukua kimoja tu kile cha kwamba awe mwepesi kuona, kusikiliza na kuguswa na shida za wananchi wake tena awe jasiri kupigania haki za wanyonge na awe na uwezo wa ubunifu katika kutatua kero za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa usemi wake huu mzuri Mheshimiwa Dkt. Mpango, nakwenda moja kwa moja kwenye Wizara ya Kilimo na Mifugo. Wizara ya Mifugo kwa kweli imenisikitisha sana, kama kweli usemi wake wa kiongozi awe hivyo, imekuwaje Wizara hii ya Mifugo ipewe fedha za maendeleo sifuri wakati Bunge hili liliidhinisha bilioni nne, tena hela ndogo sana, bilioni nne, lakini hawakupata hata senti

tano. Kwa hiyo masikitiko yangu ni kwamba, sasa kauli yake ambayo amesema kiongozi anatakiwa awe anasikiliza wanyonge na kutatua kero imekuwaje hata ile bajeti isitekelezwe. Pia hiyo bajeti hata sasa hivi inaonekana kwamba ni ndogo sana kwa kupelekwa Wizara hiyo ya Mifugo. Naomba hebu aiangalie sana; hii Wizara inadhalilika au haifai au ni kitu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha anapeleka mshahara tu lakini mambo ya maendeleo hayajulikani na hii Wizara ndiyo anayoitegemea kwenye viwanda ambapo anasema ndiyo kipaumbele chake sasa hivi kwenye kitabu chake, kwenye ukurasa wa 31, kwamba watahakikisha viwanda vinaendelezwa na kilimo ambapo kilimo hicho kuna kilimo, mifugo na uvuvi. Sasa ataendelezaje kama hapeleki hata shilingi moja, kwa kweli hilo waliangalie sana, wametudhalilisha. Ndiyo maana nasema kumpaka mafuta siyo sahihi kwa sababu kuna jambo ambalo ni kubwa sana linatakiwa lifanyiwe kazi. Hii Wizara itaendeshwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwangalie Mheshimiwa Mpina, amechoka. Anakimbiakimbia na visu na rula na nini, ni taabu kwa sababu hakuna hela za miradi. Amuonee huruma, tunaomba hii Wizara aiangalie kwa jicho la huruma, kwa kweli hii ni hali mbaya sana. Sisi kama Upinzani tunaona kwa kweli hajafanya *fair* na hawa ndio watu wengi walioko huko ambaao anawategemea wapige kura, atawapataje na kura ataipataje? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Wizara ya Kilimo; Wizara hii 2018 tuliidhinisha bilioni 150.2, lakini hadi Machi imetolewa bilioni 16.5; hivi kweli ndiyo anasema atafungua viwanda, vya nini, viko wapi? Atamhamasisha nani wakati Waziri hakupeleka fedha inavyotakiwa? Wakati anapeleka fedha nytingine nytingi Wizara ya Mambo ya Ndani, zote mpaka sijui asilimia mia moja na kitu, lakini Wizara ambayo ina watu wengi haipelekewi kitu chochote. Nadhani hapo tufikirie sana kitu cha kufanya ili usemi wake aliousema kiongozi anayechaguliwa ni wa namna gani, basi aliangalie hilo. Nadhani kiongozi bora anafaa achaguliwe kutoka

CHADEMA kwa sababu ndio wanaomuuliza maswali na hawampaki mafuta, nafiki hiyo ilani nyingine tuiache sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la wazee; habari ya wazee haionekani kabisa kuzungumzwa. Ni kweli analeta habari ya kufuta tozo ya pedi lakini habari ya wazee kama akina Rose Kamili hajaiona, hebu aliangalie hilo, tunafanyaje kuhusu wazee? Mheshimiwa mama Jenista alikuwa Mwenyekiti wetu wa Kamati, tulikuwa tumelilia sana wazee waweze kulipwa 20,000 kwa mwezi ili waweze kukimu maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee wanahangaika wanaombaomba, wanapita barabarani wanawaona. Sasa je, tunawasaidiaje? Nyumba za wazee ziko ngapi, kila mkoa una nyumba ya wazee, hakuna; anafanyaje kuhusu wazee? Naomba sana hata Wabunge hilo wallone, hata wao watazeeka hakuna ambaye atabaki...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Benardetha Mushashu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Shaabani Shekilindi ajiandae.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye bajeti hii. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri, Dkt. Philip Mpango, nampongeza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Makatibu Wakuu na watendaji wote kwa kazi nzuri na kwa bajeti nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaposikia hapa tunakuja tunatamba kwamba kuna mafanikio makubwa ndani ya Sekta ya Afya, tumpata mafanikio makubwa ndani ya elimu, tumeweza kutengezea miundombinu mikubwa ya barabara,

ndege, ni kwa sababu Wizara ya Fedha inafanya kazi nzuri. Wameweza kukusanya kodi, wametafuta fedha wakaweza kusimamia, nafikiri kule hakuna mchwa na miradi yote ikaweza kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hii bajeti ni nzuri kwa sababu inalenga wananchi na inalenga maendeleo ya wananchi. Vilevile inalenga kuboresha mazingira ya kufanya biashara na namna ya kuwashawishi wawekezaji waweze kuja katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri kwa kuweza kuhakikisha kwamba bajeti yake inaondoa sasa tozo zaidi ya 54 ambazo zilikuwa ni kero kwa wafanyabiashara. Nikitoa mifano tu; mnakumbuka hapa wakulima walikuwa wanahangaika wanashindwa kuuza karanga zao, wanashindwa kuuza mahlindi kwa sababu yanaingiliwa na sumu kuvu, lakini sasa hivi kwa kuondoa VAT kwenye vifaa vyta kukaushia ina maana kwamba basi wataweza kukausha hayo mazao na kuyauza yakiwa vizuri na yakiuzika vizuri kwenye masoko ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tauzo za watoto (*baby diapers*) ushuru umepungua kutoka asilimia kumi mpaka sifuri, ina maana kwa akina mama wengi ambao wanaendelea kuzaa watakuwa wamewapunguzia matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mashine za *EFD* wamezipunguzia ushuru kutoka asilimia 10 mpaka sifuri, kwa maana hiyo wafanyabiashara wengi watapenda kununua hizi *EFDs*, kwanza zinakusaidia kutunza hata kumbukumbu za biashara yako. Kwa hiyo wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashangaa watu ambao wamesimama hapa wanasema kwamba bajeti hii haijapunguza tozo kwenye mifugo na uvuvi. Naomba waende wakaangalie kwenye hotuba ya Waziri, ukurasa wa 78 na wa 79, zimetolewa tozo zaidi ya 15 kwenye mifugo na uvuvi na zote zina mashiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa zamani mtu ulikuwa unajichimbia kisima chako nyumbani lakini unatakiwa kulipa ada ya maji ya 100,000; sasa imefutwa. Wanaoanza biashara wamepewa angalau miezi sita waanzee kuijandaa tangu unapopewa *T/N* unakaa miezi sita unaandaa biashara yako ndiyo uanze kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri vilevile katamka kwamba tangu sasa hakuna mfanyabiashara kufungiwa biashara yake kwa sababu labda hajalipa kodi, labda kwa kibali maalum. Kwa hiyo nasema nawashangaa wote wanaosema hii bajeti siyo nzuri, naomba wote tuiunge mkono kwa sababu ni bajeti ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushuru wa Forodha umeongezwa kwenye bidhaa kutoka kwenye asilimia 25 mpaka 35 kwenye vibiriti, peremende, chokoleti, *chewing gum*, soseji, hata ushuru wa maji umeongezeka kutoka kwenye asilimia 35 mpaka 60. Nawashangaa ambao wanabeza juhudhi hizi za Serikali, hawajaelewa Serikali inataka kutuambia nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaulize Wabunge wenzangu; tuna miti kibao ndani ya Tanzania, kwa nini tuagize njiti za vibiriti, kwa nini tuagize vibiriti kutoka nje? Vilevile tunafuga ng'ombe, kuku, nguruwe; kwa nini tuagize soseji kutoka nje? Tunalima kokoa, tunalima kahawa, tuna maziwa, tuna jibini, tunalima miwa kwa maana hiyo tuna sukari; kwa nini tuagize pipi na chokoleti kutoka nje? Pia tuna unga wa mihogo, tuna unga wa ngano, tuna unga wa mtama, tuna maziwa, tuna mayai; kwa nini tuagize biskuti ambazo tunaona akinamama sasa hivi wanatengeneza kwa kutumia unga wa muhogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali inachotaka kutuambia kwa kuongeza ushuru kwenye hivi vitu ni kwamba tusiagize hivi vitu kutoka nje. Inajaribu kulinda viwanda vyatani, inajaribu kuwashawishi Watanzania tuweze kuanzisha hivi viwanda, tutengeneze peremende, biskuti na tutengeneze hizo soseji hapahaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwamba Serikali sasa akinamama hizi biashara wanaziweza, kwa kuitia Mabaraza na Mifuko ya Uwezesaji wanawake wako kwenye vikundi mbalimbali wawezeshwe, wapewe utaalalm, wapewe mitaji, waweze kuanzisha viwanda vidogovidogo, waweze kutengeneza hizi bidhaa ndani, hakuna haja ya kuagiza hizi bidhaa kutoka nje. Kwa hiyo nawapongeza kwa kuongeza huo ushuru wa forodha kwenye hizo bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta Binafsi ni sekta muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi. Kwenye Sekta Binafsi hukohuko ndiko tunapotegemea viwanda tunavyosema vijengwe, vitakuwa hukohuko, hukohuko ndiko tunapotegemea ajira za vijana wetu, hukohuko ndiko Serikali inakotegemea kupata kodi kwenye Sekta Binafsi. Ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba sasa inawatengenezea mazingira mazuri ili waweze kufanya biashara yao katika mazingira yaliyotulia, wawe na mfumo mzuri wa kodi, sera, sheria na taratibu ziwe ni zile zinaoeleweka lakini zile ambazo hazibadiliki mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Rais wetu ambaye ameweza kuita kikao akakutana na wafanyabiashara akasikiliza kero zao na namshukuru Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu wake kwa kuona kwamba sasa kero nyingine zimeanza hata kutatuliwa ndani ya bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka Mheshimiwa Rais aliacha agizo pamoja na Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwamba sasa hii mikutano iende ifanyike kwenye ngazi ya kanda. Napendekeza ianze kufanyika kwenye ngazi za mikoa wafanyabiashara waweze kueleza kero zao. Vilevile kwa sababu tunajua kodi lazima walipe ndiyo, lakini lazima wafanye biashara wapate faida na wao walipe kodi. Kwa hiyo waweze kuleta mapendekezo yao ambayo yatasaidia kuboresha mfumo wa kodi ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa Mkoa wa Kagera wanategemea zao la biashara ambalo ni kahawa na kwa miaka mingi kahawa imekuwa ikichochea na kuleta fedha za kigeni katika Tanzania. Kwa sasa kahawa ilishakuwa tayari imeshakauka, wanayo majumbani, msimu ulishaanza tangu tarehe Mosi, Mei, ni takribani miezi miwili, hakuna kahawa hata moja imeshanunuliwa Mkoa wa Kagera kwa sababu Vyama Vikuu vya Ushirika hawana fedha, Benki ya Kilimo haijatoa hela ya mikopo kwa Vyama vya Ushirika ili waweze kununua hizo kahawa kutoka kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwaso wangu ni kwamba sasa hawa wakulima wana shida, wanazo kahawa ndani, watashawishika wataanza kuzuza *butura*, wataanza kufanya magendo wataharibu kazi nzuri ambayo imeshafanywa na Serikali, ikasimamiwa na wakuu wa wilaya wote katika Mkoa wa Kagera pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Kagera, kazi ya utokomeza magendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe basi Serikali kwamba Benki ya Kilimo iongezewe mtaji na kwa haraka sana wapeleke hela kwenye Vyama Vikuu vya Ushirika Mkoa wa Kagera ambayo ni *Ngara Farmers, KDCU* na *KCU* ili sasa pamoja na kwamba tumeshachelewa miezi miwili, waruhusu kahawa zianze kununulia na mkulima akiuzza kahawa anakuta hela iko pale analipwa palepale, kutakuwa hakuna manung' uniko. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri atueleze hizo hela za Benki ya Kilimo kwenda kwenye Vyama Vikuu vya Ushirika Mkoa wa Kagera zitaenda lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nawasilisha kilio cha wazabuni. Wazabuni hawa walitoa huduma ya vyakula katika shule mbalimbali, labda hata katika hospitali na nini, lakini tangu mwaka 2011 leo hii ni mwaka 2019, wengine hawajalipwa kwa maana ya Mkoa wa Kagera, wanadai zaidi ya milioni 600 na kitu, haya ni madeni ya wazabuni ambayo yalishahakikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wazabuni walifanya makosa gani? Walitoa huduma kwa Serikali, na Serikali wale

watoto kama ni shuleni wakala, wakaendelea kusoma; hawa wazabuni walikopa hela kutoka kwa watu mbalimbali kwamba labda niamini hela nitaleta, hawakuleta, kwa hiyo hawaaminiki tena. Hawa wazabuni walikopa katika mabenki...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pli imeshagonga. Nakushukru sana.

Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, atafuatiwa na Mheshimiwa Shaabani Shekilindi, Mheshimiwa Lucy Magereli ajiandae.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, lakini niombe Waziri wa Fedha hayupo lakini na Naibu wake anaendelea kufanya mazungumzo kwa hiyo hana *concentration* ya hiki ambacho nataka kuzungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwekezaji yejote ili awekeze katika nchi lazima awe amepata mambo mawili; malighafi au soko. Mheshimiwa Rais ametembea Tanzania nzima kuhamisha watu wajenge viwanda, Mheshimiwa Rais ana nia nzuri sana na mapinduzi ya viwanda, lakini tuna mifumo Tanzania ambayo Mheshimiwa Rais anahamasisha viwanda lakini hiyo mifumo inaua viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tuna mfumo wa stakabadhi ghalani, mfumo huu unaendeshwa kwa utaratibu wa *auction* kwa maana ya mnada, lakini ule mnada unaruhusu hata wanunuzi kutoka nje wanunue ile malighafi, kwa mfano korosho. Sasa unapokuwa na *international* mnada ule ukawachukua watu waliojenga viwanda, ukawahuisha na wanunuzi wa nje, watu waliojenga viwanda hawawezi kununua malighafi kwa sababu hawawezi kushindana bei na mnunuzi wa nje. Kwa hiyo viwanda vinajengwa lakini malighafi ile kwa mfano

korosho inachukuliwa inakwenda nje. Sasa maana yake nini; maana yake viwanda vinakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni lazima tutafute utaratibu, na nashauri tutafute utaratibu ambao tutakuwa tuna minada miwili ambapo mnada mmoja utawahusisha kupata malighafi viwanda vyta ndani lakini mnada wa pili utahusisha viwanda vyta nje na mambo mengine. Hilo jambo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kahawa, mwaka jana tu walijaribu kutaka ku-*adapt* mfumo wa stakabadhi ghalani, uliwagharimu sana. Viwanda vilijengwa, viwanda vipo vipyta kabisa wakati wa ununuzi wa kahawa, kahawa ikanunuliwa na Vyama vya Ushirika, walipokwenda kutaka kununua kahawa wakaambiwa waende kwenye *auction*, walipokwenda kwenye mnada wanataka kuuziwa kahawa iliyokobolewa. Sasa nini maana ya kujenga hivi viwanda? Kwa hiyo tunaposema mapinduzi ya viwanda tuwe na utaratibu sasa wa kulinda hivi viwanda ili hizo malighafi zinazozalishwa Tanzania tuzipate.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, tunataka kukusanya kodi, kumetokea wajanja wachache wametengeneza programu inaitwa *PVoC*, *PVoCn* programu ya kufanya ukaguzi wa bidhaa nje ya nchi, programu hii ilianza mwaka 2012 kama sikosei. Programu hii inamfanya *TBS* ambaye ndio Wakala wa Serikali katika ukaguzi huo imechukua mawakala, imeingia mkataba na mawakala, *Bureau Veritas*, *CoC*, wameingia na *Intertek*, wameingia na *SGS*. Hawa wanakagua bidhaa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba bidhaa zile hazikaguliwi nje ya nchi. Mimi nimekwenda Japan, nimekwenda China, ukaguzi hakuna, lakini ili ukaguliwe lazima upate *certificate* ya *TBS* ya nchi husika. Sasa kinachofanyika, wao wakishapata ile *certificate* ndiyo wanakuandikia zile *documents* kwamba umekaguliwa lakini ukweli hawakaguliwi na unalipa dola 800. Sasa kwa nini tulipe

dola 800 nje tusifanye *direct inspection* hapa Tanzania tukalipa dola 800 hapa? Wale mawakala wa kazi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nadhani kama huu unaweza kuwa ni mradi wa mtu. Kuna watu wana miradi yao na hakuna kontena ya biashara inayokuja Tanzania ambayo haina *certificate* ya *CoC*. Kwa hiyo hebu chukua *containers* elfu tatu kwa mwezi na kwa mwaka ni *containers* ngapi halafu hizo fedha zinalipwa nje ya nchi. kwa hiyo tunakosa mapato, Serikali inakosa mapato bila sababu na dhamira ya *PVoC* ilikuwa ni kuzuia bidhaa bandia zisiingie nchini, lakini bidhaa bandia zimeongezeka baada ya huo mfumo. Kwa hiyo hata hiyo dhamira hajipo na fedha zinapotea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, Mheshimiwa Waziri, amekuja ni vizuri; *East African Comon Tariffwamefanya* jambo jema sana; wamekwenda wameweka kodi kwa ajili ya kulinda viwanda vya ndani lakini kukuza biashara katika Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, wanapofanya hivyo wanasaahau kitu kimoja; Zanzibar inategemea *exportation* asilimia 95, maana yake ni kwamba waki-copy kodi ambazo zimewekwa Afrika Mashariki maana yake Zanzibar hawawezi kuingiza bidhaa. Kwa hiyo ushauri ni nini; wanapofanya haya mambo Mheshimiwa Waziri wachukue walau Waziri wa Fedha wa Zanzibar wakae pamoja, otherwise Zanzibar ni lazima wafanye magendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tano, nimetazama katika vitabu vya Mheshimiwa Waziri vya miradi ya maendeleo, vya mipango sikuona kitu kimoja; tumejenga *flyover* ile pale *TAZARA* tumeondoa foleni pale tumepeleka foleni kule Vingunguti.

Mheshimiwa Spika, tutafungua *Terminal Three* kesho kutwa; tuna *Terminal One, Terminal Two na Terminal Three*; bora utoke South Afrika inaweza kuwa ukafika mapema kuliko kutoka pale mpaka Hyatt Regency Kilimanjaro. Sasa kwa nini Serikali isitoe *Branch* ya *Standard Gauge* ikapeleka moja kwa moja *Airport* ili tufanye usafiri wa kwenda Airport

ukawa rahisi? Kwa sababu kwa sasa ikifunguliwa na hiyo *Airport*mpya maana yake *traffic*itakuwa ni kubwa sana. Kwa hivyo niiombe Serikali itafute utaratibu wowote unaona ambaao unafaa lakini tuhakikishe safari za kutoka katikati ya mji kwenda *Airport* ni rahisi kiasi kwamba kila mmoja anaweza kwenda kwa wakati ambaao anautaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho; sitaki niseme mengi; kwanza natambua uwepo wa *Comrade Shamsi Vuai Nahonda Waziri Kiongozi* wa zamani wa Zanzibar; lakini niseme kwamba tuna miradi ya maendeleo yanayohusu watu wa Zanzibar. Mheshimiwa Waziri Wizara ya Fedha imekuwa kikwazo sana kwa sababu hata wewe mwenyewe; Mheshimiwa Waziri wa Fedha sijui kwa nini hatupendi Wazanzibar. Kuna barua hii aliandikiwa kabisa na *Saudia Fund for Development*; hii ni *original* kabisa. Napenda Mheshimiwa; mpe aone ubaya wa Mheshimiwa Waziri Mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiisoma utaona namna gani alivyokuwa hatupendi, ana roho mbaya kabisa. Mradi wa billioni 26 *BADEA* walishasaini kwa miaka mitano nyuma, barua umeletewa hata kujibu hujajibu, basi si ujibu kwamba haiwezekani? Au kama haiwezekani basi tukopesheni ninyi Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Mnajua kwamba Zanzibar hawawezi kukopa kwa sababu hawana *sovereign guarantee*, wanaokopa ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa niaba ya Zanzibar, wewe unajua hilo. Kwa hiyo Mheshimiwa Mpango hebu tukuombe, hii barabara ni barabara muhimu sana kwa sababu Pemba kule tuna barabara moja tena imebomoka. *Phase one* mmefanya vizuri mmetutengenezea barabara tuwanashukuru, lakini tukubali hii barabara ya Wete Chake imalizike usitufanyie hivyo bwana. Mheshimiwa Mpango nitizame maana unaandika hunitizami kama vile kwamba hili jambo hulitaki kulichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Sasa akikutazama wewe ataandika vipi Mheshimiwa Ngwali? Mbona leo umekuja kiaina? Ndiyo

maana Waheshimiwa Wabunge kanuni huwa zinasema uongee na kiti ili usipate tabu naye kwa sababu yeye atapata tu hayo maelezo ukisha kiambia kiti unachotaka kusema, ukimwambia moja kwa moja ndiyo tabu. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri alikuwa anaandika huwezi kuwa unaandika huku una angalia sura ya mtu.

Waheshimiwa Wabunge tumalizie Wabunge waliobaki Mheshimiwa Shaaban Shekilindi, atafatiwa na Mheshimiwa Lucy Magereli ambaye atachangia kwa dakika saba tutamalizia na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki.

**MHE. SHAABAN O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru na mimi kunipa nafasi niweze kuchangia Wizara hii ya Fedha. Kwanza kabisa nimshukuru mwenyezi mungu mwingu wa rehma kwa kunipa afya na nguvu na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Rais wangu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt John Pombe Magufuli, *then* nimpongeze Waziri Philip Mpango na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Ashatu Kijaji na timu yake ya wataalam kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli bajeti hii ni nzuri na imeenda kujibu matatizo ya Watanzania, ile kiu ya Watanzania naamini sasa imepata suluhu kwa bajeti hii. Wale ambao wanasema kwamba asiyepigia kura bajeti hii basi atamshangaa mimi nataka nisema atajishangaa yeye mwenyeewe, kwa sababu bajeti hii haijawahi kutokea Mwenyezi Mungu anasema: *:Man laa yashkur kalila laa yashkur kathira*"; maana yake usiposhukuru kwa kidogo, basi hata kikubwa hutoshukuru. Ina maana mambo yote yaliyofanyika katika nchi hii hawa ndugu zangu wanataka waniambie hawajayaona? Nataka niseme basi tumwachie Mwenyezi Mungu kwa sababu yeye ndiyo mwenye majibu sahihi, lakini Mwenyezi Mungu anajua ameona na Watanzania wameona

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja katika kuchangia, nianze na barabara. Ni ukweli usiopingika kwamba barabara za vijijiini ndiyo kila kitu ndizo zinazotoa mazao, ndizo ambazo wakulima wanazitegemea kuliko barabara nyingine. Sasa niiombe Serikali yangu Tukufu kwamba badala ya kutenga asilimia 30 kwa ajili ya *TARURA* basi watenge asilimia 40; niishauri Serikali yangu Tukufu; mimi naamini Mheshimiwa Mpango hili linawezekana. Wewe mwenyewe unajua kwamba barabara hizi za *TARURA* ni nyingi kuliko hata hizi za *TANROAD*. Nikuombe Mheshimiwa Mpango hili uliangalie kwa jicho la huruma ili sasa twende kukidhi haja za wananchi wetu, hususan wale waishio vijijiini. Kwa kweli fungu hili la *TARURA* ni dogo sana ambalo kwa kweli haiwezi kabisa kukidhi barabara za vijijiini.

Mheshimiwa pamoja na hayo kuna barabara ambazo zinaunga wilaya hadi wilaya; niishauri au niiombe Serikali yangu sasa ichukue barabara hizi ziingie kwenye *TANROAD*. Kwa mfano barabara zangu za kutoka Mlola, Makanya, Milingano hadi Mashewa, barabara hii ni barabara ya kiuchumi; nikuombe Mheshimiwa Mpango barabara hii ipandishwe hadhi. Bado kuna barabara ya Doch, Ngulwi hadi Mombo kilometra 16; barabara hii siyo ya kiuchumi tu, barabara hii sasa itakuwa ni barabara ya mchepuo, hususan barabara yetu ya kuanzia Mombo, Soni hadi Lushoto. Kwa mfano mwaka juzi iliharibika mafuriko yaliingia kule maporomoko yakaziba barabara zaidi ya takriban wiki mbili na wananchi wale walipata tabu sana mpaka mazao yao yakaharibika. Kwa hiyo nikuombe barabara hii angalau ipandishwe hadhi ili ichukuliwe na *TANROAD* na iweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, niende kwenye kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo wa taifa letu na asilimia 65 ya wananchi wa Tanzania ni wakulima. Kwa hiyo niombe sasa hawa Wakala wa Pembejeo wapeleke pembejeo kwa wakati. Wakati wa palizi anapeleka mbolea za kupandia wakati wa kuvuna anapeleka mbolea ya kukuzia; sasa hii jamani tutafika kweli ilhali tunataka kwenda kwenye uchumi wa viwanda?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo tuangalie na masoko yetu, tuwatafutie wakulima wetu masoko. Mimi naamini kabisa kwamba Serikali hii ni sikiu na inaweza kabisa kutafuta masoko. Ni imani yangu kubwa kwamba kipindi hiki cha 2019/2020 wakulima wetu watapatiwa masoko ya kutosha ili waweze kujikimu katika hali hii, waondokane na hii hali ya kuhangai huku na kule kutafuta masoko wao wenye

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye elimu. Tunaenda kwenye uchumi wa viwanda, uchumi wa viwanda huu naamini kabisa unaendana sambamba sasa na kumalizia maabara zetu. Hizi maabara naamini kabisa zikimaliziwa tutaanza kupata watu amba ni wataalamu kuliko ikifikia hatua tukaenda kutafuta wataalamu nje ilhali sisi wenye tuna watoto wetu amba tukimaliza maabara hizi watasoma elimu kwa vitendo, moja kwa moja wataenda kuhakikisha kwamba wanasi mamia viwanda hivi ambavyo vitafunguliwa; mimi naamini hii inawezekana. Kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Mpango sasa twende kumalizia maabara hizi, lakini sambamba na hayo lazima tuyamalizie pia haya maboma ya madarasa kwa shule zetu. Pamoja na hayo tujenge nyumba za walimu pamoja na hosteli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye pensheni kwa wazee. Wazee hawa wamesahaulika kwa muda mrefu sana, wazee hawa ndio amba wametufanya mpaka leo hii tunasimama mbele yenu hapa tunaongea na nyinyi tunaongea na Bunge lako Tukufu, tunaongea na Watanzania. Niombe sasa kwamba wazee hawa kwenye ile asilimia 10 inayotoka halmashauri na wazee nao wawepo pale inaweza kuwa asilimia tatu kwa vijana, asilimia tatu kwa akinamama, asilimia mbili kwa wale mavu, na asilimia mbili kwa wazee, hiyo inawezekana

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja niende kwenye suala la faini za magari zinazotozwa na *traffic*. Nikuombe Mheshimiwa Mpango; faini hizi ukizilinganisha kati ya basi au pamoja na pikipiki ni vitu viwili tofauti sana.

Nikuombe sasa Mheshimiwa Mpango kwamba hizi faini 30,000 zinazotozwa kwenye bodaboda zipungue, angalau zifikie 10,000 kwa sababu hawa ndugu zangu kipato chao wanachokipata ni kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende tena kwenye suala la kitengo cha manunuzi. Hiki nilikielezea kipindi cha nyuma lakini ikawa nimeishia katikati. Kitengo hiki kwa kweli kinakwamisha sana maendeleo. Ninaomba, ikiwezekana kitengo hiki kama si kufutwa basi kirekebishwe; kwa sababu mradi ambao unahitaji milioni 500 ukipeleka kwenye kitengo cha manunuzi utaambibi labda bilioni 1.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitengo hiki kwa kweli mimi ni imani yangu kabisa kwamba kinazalisha rushwa moja kwa moja. Kwa mfano unaweza ukarabati wa *gate valve* ya shillingi 50,000, lakini wao wakileta *quotation* yao wanakwambia hii inauzwa shillingi 500,000 sasa kweli utafika, kwa hiyo niombe tuangalie ikiwezekana tutumie *force account* katika suala hili; na hiki kitengo ikiwezekana kifutwe kabisa maana naamini kabisa kinakwamisha juhudzi za Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niende moja kwa moja kwenye suala la viwanja vya ndege. Ni imani yangu kubwa sana kwamba Serikali hii imejitahidi kwenye ukarabati wa viwanja vya ndege. Niombe kwamba kile kiwanja cha ndege; kwa kuwa Tanga sasahivi imefunguka kibia shara basi ongeza fedha. Naamini umetenga fedha lakini fedha zile hazitosh; ongeza fedha sasa ziende zikatengeneze uwanja ule kwani uwanja ule sasa hivi ndege haziwezi kutua usiku kwa sababu hauna taa. Kwa hiyo ni imani yangu kubwa; nikuombe uhakikishe kwamba unapeleka fedha za kutosha ili kwenda kujenga uwanja ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la watumishi. Watumishi wetu wana...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa ahsante sana, Mheshimiwa Lucy Magereli atachangia kwa dakika saba, tutamalizia na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki

**MHE. SHAABAN O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na nianze kwa kumshukuru mwenyezi mMungu muumba wa Mbingu na ardhi aliyetuajaalia uzima wa kuwepo ndani ya nyumba hii, kujaribu kusema kwa niaba ya Watanzania, kushauri na kuwasaidia wenzetu wa Serikali kuona pale ambapo macho yao hayajaweza kufika au kuona yale ambayo wameyatazama katika namna ambayo Watanzania wengi hawayatazami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamechangia na bahati nzuri leo tunakaribia mwisho wa bajeti ya Serikali, wamezungumza mambo mengi kuhusu sekta ambazo zinaajiri Watanzania wengi na namna ambavyo hazijatazamwa. Hata hivyo mimi leo nataka nianze kwa kuwazungumzia ndugu zangu wengine ambao wanachangia sana ustawi wa nchi hii lakini hawapewi kipaumbele, watu hao ni waandishi wa habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninyi ni mashahidi wote kwamba bila waandishi wa habari nchi hii ingelikuwa iko gizani. Ninyi kama watu wa Serikali mnajua kabisa namna ambavyo mnaongozana nao masaa 24 ili yale mnayoyatekeleza yawafikie wananchi, lakini mpaka leo maslahi ya waandishi wa habari ambao wanasaidia na kuchangia maendeleo na upashanaji wa habari mikataba yao ya ajira na maslahi bado ni duni sana. Bahati mbaya Waziri wa Habari hayupo lakini Naibu Waziri yupo, hebu rudini Wizarani mkaangalie namna ambavyo mnawenza mkasaidia tasnia ya habari muwasaidie ndugu zetu wanaotoa mchango wao nao wafaidi na wajisikie Watanzania ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la usiri ambao unalinyonya Taifa. Mwaka 2017 tulipitisha sheria ya ulinzi wa rasilimali za nchi. Sheria hiyo illetwa Bungeni kwa mbwembwe, tena ikajadiliwa ndani ya muda mfupi, ikapitishwa, ikaungwa mkono kwa nguvu. Hata hivyo hatimaye mpaka leo ninavyozungumza bado kuna usiri mkubwa sana katika mambo yanayohusu leseni, mikataba na malipo ya Serikali yanayotokana na madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulijua ya kwamba sheria ile ilipopitishwa basi ilikuwa ndio mwarobaini na chanzo cha ulinzi wa rasilimali zetu, na ya kwamba katika katika kifungu cha 12 cha Sheria ya Milki ya Kudumu ya Utajiri na Rasilimali za Asili ya mwaka 2017; katika kifungu kile kinaruhusu ya kwamba mikataba yote inayohusu maliasili na madini na utajiri wa nchi hii kuletwa na kujadiliwa Bungeni lakini mpaka tunavyozungumza leo mikataba hiyo haijawahi kuja na hata hakuna dalili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri wetu, hiki ndicho kati ya vyanzo vya uhakika kabisa vya mapato, lakini hatujapata fursa ya kujadili na kuona ya kwamba Serikali inapata kiasi gani katika mirahaba na mambo mengine yanayohusiana na maliasili na utajiri wa Tanzania

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye suala la viwanda. Katika ukurasa wa 31 wa kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ameelezea vizuri mipango yake. Nilipoanza nilisema nitakusaidia kuona pale ambako haujaona. Mheshimiwa Waziri wa Fedha hatuwezi kujenga viwanda wala hatuwezi kushindana na nchi zinazochipukia kiuchumi kwa mkakati huu tulionao. Tumeikiacha kilimo nyuma sana, lakini hata viwanda vyenyewe bajeti kiduchu tunayowapatia haiwezi kuwasaidia kutoka walipo.

Mheshimiwa Mwenyekti, mfano halisi ni bajeti ya mwaka 2018/2019 ambapo waliidhinishiwa shilingi 90 bilioni lakini wakapewa shilingi bilioni 5.4 tu ambayo ni asilimia sita. Mnazungumza habari ya uchumi wa viwanda wa nchi hii

utokee wapi kwa asilimia sita ya fedha ya maendeleo unaotolewa? Namwelewa sana Mheshimiwa Mwijage na kilichomkuta, kwa sababu kwa asilimia sita unafanya nini? Bora utumbuliwe ukae benchi kama alivyo leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kuuliza swali; tunazungumzia Tanzania ya viwanda na uchumi wa viwanda; hivi ni nani katika nchi hii leo anayehangaika na kuangalia *manpower, labour force*, aina ya ajira na kazi tunazozizalisha kwenye vyuo vyetu ambavyo hatimaye vitakwenda kuchangia kuwa rasilimali watu katika Tanzania ya viwanda? Hatushughuliki na hilo kabisa. Vyuo vya VETA vinasuasua, havina fedha havina utaratibu, hata na mitaala yao nayo ni ya kuungaunga wanafundisha mapishi, wanafundisha vitu ambavyo kwa kweli tukizungumza Tanzania ya Viwanda bado mkakati wetu hauwezi kutufikisha tunapotaka kwenda

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie suala lingine la miradi mikubwa ambayo inasifiwa sana hapa ndani, ya *Stiegler's Gorge, SGR*na vinginevyo. Kuna namna ambavyo hii miradi inakwenda kuifilisi nchi na tunakwenda kuibawa mno kupitia hii miradi mikubwa. Nimesema leo nitawaambia yale ambayo hamja yaona. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Waziri wa Miundombinu hawa wawekezaji ni wajanja sana, wanatuletea *BOQ* ambazo zina *specification* za vifaa ambavyo hapa kwetu havipatikani. Nasi kwa sababu tunaharakia tunatafuta *10 percent* tunasaini mikataba haraka wanachukua kazi. Mnajua kabisa ya kwamba sisi hatuwezi kujenga na hiyo *Stiegler's Gorge*. Reli yetu tukijenga pesa zinakwenda nje, *Stiegler's Gorge* pesa zinakwenda nje, upanuzi wa viwanja vya ndege pesa zote zinakwenda nje, ndege tunazonunua pesa zinakwenda nje. Kwa hiyo hii miradi mnaposimama na kuisifia fikirini ya kwamba Tanzania yenyewe inanufaika namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, na bahati mbaya sana hii ni miradi ambayo haina ile inaitwa *high rate of return* siyo miradi ambayo inakwenda kurudisha ile fedha yetu haraka ni miradi ambayo itachukua muda mrefu sana, na pesa zote

zinakwenda nje. *On top of that* fedha tunayo jengea hiyo miradi tunakopa kutoka nje na hatima yake hata tukianza kuzalisha au kutokana na kuwakamua wananchi wetu tutawalipa tena watu wale wale ambao waliojenga ile miradi. Kwa hiyo mimi naiita miradi ambayo inaiibia taifa na kututia hasara

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la ujasusi wa kiuchumi. Unajua kuna jambo ambalo tukijaribu kuliangalia nashangaa sisi hatuwezi kuyaona kama ambavyo wanayaona wengine. Matajiri katika maeneo mengine wanapewa fursa za kuwa matajiri zaidi ili walipe kodi na wazalishe ajira lakini huku kwetu sisi tunataka wawe mashetani. Jama...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga nakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge tutamalizia na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu kuhusiana na hoja hii iliyio mbele yetu ya Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Naibu Waziri wake kwa sababu ya nguvu na akili walizoweka kwenye kuandaa bajeti ya mwaka huu. Kusema ukweli wameweka nguvu na akili kubwa, lakini pia wametoka na kitu ambacho ni cha manufaa na kina leta matumaini kwa Watanzania wengi sana. Kwa hiyo niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri Mheshimiwa Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii, kwa kuja na bajeti ambayo inatoa matumaini makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapinduzi ya viwanda ya nchi ya Uingereza yalisababishwa na mambo mawili tu. Cha

kwanza ni nishati, na hiyo ilikuwa ni nishati ya makaa ya mawe. Halafu cha pili mapinduzi kwenye usafiri na uchukuzi, na njia kubwa iliyokuwapo ni njia ya reli. Mambo hayo mawili yalisababisa Waingereza wakafanya mapinduzi ya viwanda na wakaanza kuzalisha bidhaa nyingi. Mpaka ilipofika mwaka wa 1884 na kuendelea wakaanza kutafuta masoko ya bidhaa zilizokuwa zikilizalishwa kwenye viwanda vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakaanzia Ulaya wakafika mpaka kwetu Afrika na huku wakaona ili waunze bidhaa zao vizuri lazima watutawale; lakini chanzo ilikuwa ni nishati ya umeme walioyoipata kwa njia iliyokuwa rahisi lakini pia mambo ya usafiri, uchukuzi na mambo mengine. Kwa hiyo tunaponzungumza nchini kwetu juu ya kuzalisha umeme wa kutosha bado tupo sahihi. Nchi yetu tunapozungumza reli ya kisasa na kuboresha njia za usafiri nyingine zote, barabara na viwanja vya ndege pamoja nakuwa na ndege zetu bado tupo sahihi. Mheshimiwa Rais yupo sahihi, wasaidizi wake wanaomshauri, Makamu wa Rais Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wengine wote tupo sahihi na tupo kwenye njia sahihi. Kwa hiyo ninaamini baada ya miaka michache hawa wanaopotosha na kubeza watakuja kukubali ya kwamba tulipata kiongozi kwenye miaka hii ambaye alitupeleka mahali kulipokuwa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa ushauri kwa mambo mawili au matatu. La kwanza ni kuhusu Shirika letu la *TPDS*. Shirika hili limeboreshwa sana sasa hivi, limeunda kampuni mbili zingine, yaani kampuni inayoshughulika na gesi na kampuni nyingine inashughulika na mafuta. Shirika hili limepewe majukumu mbalimbali lakini jukumu mojawapo ni kuhakikisha kwamba linaendeleza matumizi ya gesi kwenye nchi yetu. Kwa kutimiza jukumu hilo, shirika hili limeweza kupeleka gesi kwenye viwanda 41 na lipo mbioni kupeleka gesi kwenye viwanda vingine 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hivyo tu shirika hili pia limeweza kuunganisha kwenye magari zaidi ya 200 ili yaweze kutumia gesi pamoja na *petrol*; sasa magari haya ni mengi sana. Pamoja na mambo hayo shirika hili limeweza

pia kuunganisha gesi kwenye baadhi ya kaya katika jiji la Dar es Salaam ili gesi hiyo iweze kutumika majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba sana Serikali ijaribu kuangalia kulipa nguvu shirika hili ili liweze kuendelea na mpango wake hasa ule wa kutumia gesi kwenye magari kwa sababu mpango huu una faida kubwa kwa nchi yetu. Kwa mfano magari haya 200 kama yangekuwa ni ya serikali. Serikali ingeweza kuokoa pesa nyingi kwa sababu kwa mujibu wa maelezo yao kutoka Dar es Salaam kuja hapa Dodoma mtungi unaoweza kutumika kwa gari linalotumia *petrol* ni mtungi wa kil 15 ambaو unagharimu kama shilingi 40,000 au na kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maana yake kutoka Dar es Salaam kuja hapa Dodoma unaweza kufika kwa shilingi sana nyingi 50,000 balada ya shilingi 150,000 mpaka shilingi 200,000. Kwa hiyo ikiwa shirika hili litawezeshwa likajenga vituo vya kuweka gesi hapa Dodoma na pengine Manyoni au Singida na mahali pengine Shinyanga au Mwanza, mtu anaweza akatoka Dar es Salaam mpaka Mwanza akatumia gesi, kitu ambacho kitamgharimu hela kidogo mpaka kufika Mwanza. Na kwa maana hiyo nchi inaweza ikaokoa hela nyingi sana za kigeni ambazo tunatumia kununua mafuta *petrol* na *diesel*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nchi inaweza ikaokoa hali zetu za mazingira kwa sababu gesi ni rafiki ya mazingira. Kwa hiyo nilikuwa nashauri kwamba shirika hili liwezeshwe na liweze kugharimia au liweze kutoa gesi kwenye magari mengi zaidi. Mimi nilikuwa nashauri pengine Serikali ingefikiria sasa kuleta magari yake yanayotumia njia mbili, njia mojawapo iwe ya gesi ili kwamba magari hayo mengi ya Serikali yatumie gesi badala ya kutumia *petrol* au *diesel*, hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka kushauri; sasa hivi dunia yetu inaendeshwa kmtandao. Kuna kitu ambacho kinaitwa *Digital Economy*, na duania yote sasa mwelekeo ni huo. Sasa ukijaribu

kuangalia sisi tunatumia mifumo hii kwa uchache sana. Naelewa serikali imeweka mifumo ya *TEHAMA* mbalimbali, inayo, lakini bado hatujamia fursa hii kwa ukamilifu wake. Kuna mambo mengi ambayo yanatumiwa kwenye uchumi huu wa ki-dijitali. Kwa mfano siku hizi kuna mikopo unaweza ukapata kwa kupitia simu yako ya mkononi, lakini pia kuna namna nyingi zinatumika kuanzisha mitandao mbalimbali ambayo kupitia mitandao hiyo watu wanalipa pesa na wanapata bidhaa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikuwa nashauri kwamba sisi kama nchi hebu tunanze kufikiria kuchukua hii fursa ambayo iko wazi sasa hivi kwanza kwa kuwa na sera ya *TEHAMA*. Kwa sababu sera ya *TEHAMA* pia hatuna; tuwe na sera ya *ICT* halafu baada ya hapa tuwe na sheria zitakazotu-guide namna ya uwendeshaji wa uchumi huo ambao dunia inakimbia haraka kuelekea huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikuwa nashauri kwamba sasa sisi kama nchi tunapopanga mipango yetu ya uchumi tuanze kufikiria jambo hili ambalo hatuwezi kuliepuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie jambo la tatu kuhusiana na masoko ya mazao yetu; jambo ambalo limezungumza na Wabunge wengine. Mwaka jana Serikali ilifanya uamuzi mzuri, Wizara ya Kilimo ikanunua korosho kutoka kwa wa kulima kwa bei nzuri lakini korosho ile hatujaweza kuiiza kwa sababu shida ni masoko. Pia sasa hivi tupo kwenye msimu wa kuuza pamba, pamba yetu sasa hivi inapelekwa tu kwenye magodauni ya vyama vya mashirika lakini hakuna mnunuzi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mashimba Ndaki kengere ya pili imeshagonga.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ahsanteni sana kwa michango yenu mizuri. Tumefika mwisho wa uchangiaji kwa siku ya leo.

Niwakumbushe kwa kifupi tangazo la michezo kesho ambalo ratiba tulishasomewa asubuhi, kwa hivyo sitairudia, lakini mnakumbushwa kwamba kesho siku ya Jumamosi kutakuwa na matembezi kuanzia hapo kwenye geti kubwa la Bunge mpaka Jamhuri. Pia usiku mnaalikwa kwenye mchaparo, ukumbi mpya makili *Cape Town Kisasa Complex* matembezi yataanza saa 12.30 asubuhi. Baada yakusema hayo naairisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.50 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 24 Juni, 2019, Saa Tatu Asubuhi)*